

**M A P**

# **MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA**

Nguvu ya Kuwa na Mkakati

**I N D**

**GARY KEESEE**

**U Z I**



**M**

**A**

**P**

# MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA

Nguvu ya Kuwa na Mkakati

**I**

**N**

**D**

**GARY KEESEE**

**U**

**Z**

**I**

**Your Financial Revolution**

*Power of Strategy*, Kiswahili By Gary Keesee

© Gary Keesee, 2023

Originally published in English

ISBN: 978-1-945930-03-4

Faith Life Now

P.O. Box 779

New Albany, OH 43054, USA

You can reach Faith Life Now Ministries on the Internet at

[FaithLifeNow.com](http://FaithLifeNow.com)

**Mapinduzi yako ya Kifedha**

*Nguvu ya Kuwa na Mkakati*, Kiswahili na Gary Keesee

© Gary Keesee, 2023

Awali kilichapishwa katika lugha ya Kiingereza

ISBN: 978-1-945930-03-4

Faith Life Now

P.O. Box 779

New Albany, OH 43054, USA

Unaweza kufikia Faith Life Now Ministries kwenye mtandao kupitia

[FaithLifeNow.com](http://FaithLifeNow.com)

Nataka kuweka wakfu kitabu hiki kwa mke wangu, Drenda, kwa sababu ni kutia moyo kwake, shauku yake ya mambo ya Mungu, na upendo wake kwangu na kwa familia yetu ambavyo vimenitia moyo kwa miaka hii yote. Pamoja tumethibitisha kwamba ndoto kweli hutimia!

Gary Keesee



# YALIYOMO

<b>UTANGUL IZI</b> .....	ix
<b>SURA YA 1:</b> Eti Unataka Tufanye Nini?.....	1
<b>SURA YA 2:</b> Ufalme .....	17
<b>SURA YA 3:</b> Mshangao .....	25
<b>SURA YA 4:</b> Mambo Ya Kimsingi: Usitoke Nyumbani Bila Hili .....	39
<b>SURA YA 5:</b> Ushahidi Wa Kimaandiko .....	55
<b>SURA YA 6:</b> Je! Wote Huomba Katika Ndimi? .....	63
<b>SURA YA 7:</b> Sanduku La Hazina .....	73
<b>SURA YA 8:</b> Mahali Pagumu Pa Kupandishwa Cheo .....	87
<b>SURA YA 9:</b> Sauti Ndogo, Tulivu .....	95
<b>SURA YA 10:</b> Maono Na Ndoto .....	107
<b>SURA YA 11:</b> Roho Mtakatifu Husikika Kama Bosi Wangu .....	119
<b>SURA YA 12:</b> Jinsi Ya Kuomba Kupokea Roho Mtakatifu .....	131





# UTANGULIZI

Kitabu *Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kuwa na Mkakati* ndicho cha tatu katika mfululizo wa kitabu ninachoita Mapinduzi ya Kifedha. Kutakuwa na vitabu vitano vitakapokamilika, na vyote ni matoleo yaliyopanuliwa ya mkutano niliokuwa nao nchini Albania mwaka wa 2005. Ilikuwa katika mkutano huu ambapo mwelekeo wa maisha yangu ulibadilika sana. Ikiwa umesikia hadithi hii, unaweza kutaka kuruka utangulizi na kuanza katika sura ya kwanza. Lakini kama hujaisikia, basi tafadhali acha nikuambie kuhusu ukungu wa rangi ya samawati. “Ukungu wa rangi ya samawati ni nini?” labda unauliza. Ninaelewa swali lako. Nilipouona, sikujua ni kitu gani pia, nilihisi uwepo mkuu ajabu wa Mungu, na nikafahamu ukungu huo ulitoka Kwake. Hebu nikusimulie hadithi hiyo.

Mimi na mke wangu tulianza ndoa yetu tukiwa na madeni na tulikaa kwa madeni kwa miaka tisa. Sio madeni tu, bali tulitaabishwa na shinikizo lililotudhoofisha na tulihofu kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Ingawa hatukukusudia kuharibu maisha yetu kifedha, hivyo ndivyo tulivyofanya. Tulianza na kadi moja tu ya mkopo ya petroli, kisha kadi moja ya Visa, kisha zikawa kadi kumi za Visa. Tuliposhindwa kulipa madeni ya kadi za Visa, tulikopa kutoka kwa kampuni za kifedha kwa riba ya asilimia ishirini na nane hadi thelathini na tatu ili kujumlisha malipo yetu. Lakini tulitumia kadi hizo isivyofaa pia na madeni yakaendelea kuongezeka! Hatimaye, tulimilki kadi kumi za mkopo zilizokuwa zimeghairiwa maana tulizitumia kupita kiwango kilichostahili, mikopo mitatu ya kampuni za fedha, na mashtaka kutoka kwa shirika la malipo ya kodi ya makumi ya maelfu ya dola, pamoja na madeni mengine mengi madogo. Tulidaiwa na daktari wetu wa meno, wasafishaji kavu, wazazi wetu makumi ya maelfu ya dola, malipo ya magari yetu mawili, malipo ya kodi ya nyumba, na orodha inaendelea. Wakati huo riziki yetu ilitoka kwa kamisheni nilizolipwa kazini

tu, na kusema kweli shinikizo lilikuwa zito kwangu. Mashambulio ya hofu yalitaka kunimaliza, jambo ambalo lilifanya nianze kunywa madawa ya kupunguza huzuni, wala hayakusaidia.

Kila kitu tulichokuwa nacho kilikuwa kimeharibika. Tulikuwa tumetumia magari yetu yote kwa zaidi ya maili 200,000. Nyumba yetu ndogo na nzee ya mwaka wa 1856, tuliyokodisha kwa \$300 kila mwezi, ilikuwa na matatizo. Madirisha yake mengi yalikuwa yamevunjika, na kwa kuwa hatukuwa na pesa za kuyakarabati, tuliweka mkanda wa kuunganisha juu ya nyufa. Lakini hilo halikufaa. Mimea kutoka nje ilikuwa ikimea kupitia nyufa za fremu. Mke wangu, Drenda, alikuwa akiikata kidogo kisha kuiacha iwe kama sehemu ya mapambo ya nyumba. Tuliokota zulia la chumba cha kulala cha wana wetu kutoka kando ya barabara kwenye rundo la takataka. Magodoro yao tuliokota kutoka kwa rundo la godoro nzee za nyumba ya watu wazee, zilizokuwa zimetupwa. Tulinunua kila samani kwa bei rahisi kutoka kwa wauzaji wa vitu ambavyo tayari vimetumiwa au kuokota kutoka kwa rundo la takataka la mtu fulani.

Maisha sio ya kufurahisha unapoamka kila siku na kujiuliza utailishaje familia yako. Hofu ilitawala maisha yangu, na furaha na tumaini vilikandamizwa na machafuko ya unusuru. Mimi na Drenda tuliishi hivyo kwa miaka tisa mirefu! Miaka tisa mirefu! Naweza kuelewa ikiwa ni mwezi, au mwaka ikiwa ni vibaya zaidi, lakini miaka tisa? Baada ya miaka tisa ya mashinikizo kama hayo, hisia zako huwa kidonda wala subira haipo tena.

Katika miaka hiyo tisa, tulikuwa washirika katika kanisa nzuri ambapo tulifundishwa kwamba umaskini haukuwa mapenzi ya Mungu kwa watu Wake. Tulitoa zaka na matoleo mara kwa mara, lakini bado fedha zetu hazikudhihirisha uaminifu wa Mungu na kile Neno la Mungu lilichosema. Nilikuwa na digrii katika mafunzo ya Agano la Kale na pia nilikuwa nimehudhuria shule ya Biblia kwa zaidi ya mwaka mmoja. Nilijua kwamba mambo hayakuwa sawa lakini niliendelea kutumaini kwamba, hatimaye, mambo yangegeuka. Lakini hilo halikufanyika kwa miaka tisa. Wakusanyaji wa malipo ya bili walikuwa wakipiga simu karibu kila siku, na mimi na Drenda tulikuwa karibu kupoteza matumaini kabisa.

Kando na hayo, madaktari walisema nilikuwa na dalili zote za mwanzo wa kuwa na ugonjwa wa kisukari, huku nikikabiliwa na matatizo ya kiafya yaliyodhoofisha. Hatukuwa na pesa, kila kadi ya mkopo ilikuwa imeghairiwa, wala hakukuwa na chakula nyumbani. Hofu ilinitesa kiasi cha kuogopa kuondoka nyumbani kwangu. Mke wangu alikuwa ameanza kupanga akilini mwake jinsi yeye na watoto wangelivyohitaji kurejea

nyumbani kwa wazazi wake maana alifikiri mume wake angekufa. Hata hivyo, ilikuwa katika hali hii ya kuwa chini kabisa ambapo maisha yangu yalibadilika.

Wakili mmoja alikuwa amenipigia simu mara nyingi, na nikaendelea kumuahidi kwamba tungelipa bili, jambo ambalo nilitumaini tungefanya, lakini pesa hazikuja kamwe. Kwa hivyo asubuhi moja alinipigia simu, na hakuwa na subira yoyote. “Unapaswa kufanya malipo haya kabla ya siku tatu kuisha kama sivyo nitafungua mashtaka dhidi yako kwa sababu ya pesa unazomwia mteja wangu.” Hapo ndipo nilipogundua kujifanya kumekwisha. Sikuwa na pesa, na hata familia yangu haikutukopesha pesa zaidi. Na moyo uliokata tamaa, nilipanda ngazi kuelekea chumbani kwetu katika ile nyumba yetu ndogo kule mashambani, nikalala juu ya kitanda changu, na kumlilia Mungu. Cha kushangaza ni kwamba, kutoka kwa roho yangu, nilisikia jibu mara moja. Kwanza, alinikumbusha Andiko ambalo nilikuwa nimesikia na kusoma mara nyingi, Wafilipi 4:19:

*“Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri Wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.*

“Bila shaka, ninajua Andiko hili,” nikamwambia Bwana kisha nikasema, “lakini hilo halifanyiki maishani mwangu. Mahitaji yangu yote hayatimiziwi.” Bwana alinijibu, “Sina uhusiano wowote na janga lako. Janga lako limesababishwa na ukosefu wako wa kujifunza jinsi Ufume Wangu unavyofanya kazi.” Aliendelea kuniambia mambo mengine machache, lakini nilipata ufahamu wa kile alichokuwa akisema: Madeni hayakuwa mapenzi Yake kwangu. Ingawa nilifurahi kwamba nilisikia kutoka kwa Mungu, itabidi nikiri kwamba sikujua alichomaanisha aliposema Ufalme. Nilikuwa na digrii katika mafundisho ya Biblia na nilihisi kwamba nilijua Biblia vyema, lakini kumbe nilikosea. Kitu cha kwanza nilichokifanya baada ya kusikia maneno hayo ni kumtafuta Drenda na kutubu kwake kwa kutuingiza katika masumbuko. Kisha sote wawili tulisali kwa Mungu na kumwomba atufundishe kuhusu utendaji wa Ufalme Wake. Pia tulitubu kwa kutegemea madeni na tukaazimia kwamba hatungetegemea madeni kuwa mtindo wa maisha yetu tena. Lakini, kwa kweli, ingawa nilikuwa na digrii katika mafundisho ya Biblia, Ufalme wa Mungu bado ulikuwa fumbo kwangu wakati huo. Wakati pekee ambao niliweza kukumbuka neno ufalme likitumika katika Agano Jipya ni katika Sala ya Bwana.

*“Ufalme Wako uje, mapenzi Yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.”* (Mathayo 6:10)

Kwa kweli hatukuelewa Mungu alikuwa akijaribu kutuambia nini, lakini tulipoanza kumtafuta, alianza kutufundisha mambo makuu. Jambo la kwanza tulilopaswa kufahamu ni maana ya ufalme na ni kwa nini Mungu alitumia neno hilo. Alikuwa akijaribu kutuambia nini? Baada ya kufanya utafiti, nilijifunza kwamba ufalme haukuwa kundi la watu tu. Ni kundi la watu wanaoishi chini ya mamlaka ya serikali na mfalme. Kihalisi neno ufalme linamaanisha utawala wa mfalme. Utawala wa mfalme, au mamlaka yake na sheria zake, hutekelezwa kwa kila raia katika milki yake kupitia kwa serikali yake. Kwa hiyo, jambo muhimu kwangu lilikuwa hili: Ufalme wa Mungu ni serikali.

Na serikali zina sheria!

Wajua, nilimwona Mungu kama Wakristo wengi wanavyomwona, na ufahamu potofu kuhusu uwezo Wake. Nilidhani kwa sababu Yeye ni Mungu kwamba angeweza kufanya chochote alichotaka wakati wowote alipotaka. Najua hapa utasema kwamba nimekosea, lakini acha niendeleo. Kwa sababu niliamini hivyo kumhusu Mungu, niliona sala isiyojibiwa kama ombi ambalo Yeye amelikataa. Huku kutokuwa na hakika kuhusu maombi kuliniifanya niwe na matumaini tu kwamba angejibu. Kwa hivyo, mtindo wa maombi yangu mengi ulikuwa wa kusihi na kulilia rehema, huku nikiwa na tumaini kwamba hoja yangu ilisikika kuwa nzito vya kutosha kuvutia usikivu wa Mungu. Lakini Mungu alipoanza kunifundisha kwamba Ufalme Wake wote ni serikali yenye sheria ambazo tunaweza kujifunza na kutumia, nilisimka. Nilijifunza kwamba nilipokuja kwa Kristo nilipata kuwa mrithi na raia wa Ufalme wake mkuu.

*“Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani Mwake Mungu.”* (Waefeso 2:19).

Nakumbuka niliposoma Andiko hili niliwaza, *nina haki za kisheria katika Ufalme Wake! Je, inaweza kweli kuwa rahisi hivyo? Kama raia wa Marekani, sihitaji kuomba na kusihi kupata kile ambacho tayari ni changu kama raia. Sihitaji kuwa na hisia nyingi za kuthibitisha kuwa mimi ni raia. Nilizaliwa hapa. Nilipozaliwa upya katika Ufalme wa Mungu, nilifanyika raia wa Ufalme Wake. Hiyo inamaanisha nina haki kisheria kupata manufaa*

*ambayo yameandikwa katika sheria za Ufalme Wake.* Ulimwengu wangu ulibadilika sana Mungu alipoanza kunionyesha jambo hili. Wajua, mimi na Drenda, kama Wakristo wengi, hatukuelewa swala la Ufalme na sheria zake.

Mtu anapokabiliwa na wakati mgumu, utasikia Wakristo wengi wakisema mambo kama vile, “Mungu ndiye aliyeliruhusu, ndiye mjuzi wa vyote, ndiye mdhibiti, au ndiye mwenye enzi.” Dhana hizi zinaonyesha imani kwamba Mungu ana uwezo wa kutoa jibu lakini hataki au hajaamua kuhusika. Maoni haya mapotofu kuhusu Mungu ni matokeo ya kutojua tabia ya Mungu au kuelewa jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi.

Acha nifafanue ninachosema. Ikiwa ungekuwa na dola bilioni kwenye benki, ungesema, “Nina dola bilioni.” Lakini ukweli ni kwamba huna dola bilioni mfukoni unaposema hivyo, bali una dola bilioni katika taasisi fulani, ambazo lazima ufuate utaratibu wa kisheria ili kuzihamisha kutoka kwa taasisi hadi mikononi mwako. Ndivyo ilivyo katika Ufalme wa Mungu. Sisi kama raia na washiriki wa nyumba ya Mungu, ni warithi wa yote Mungu aliyo nayo. Lakini kuna sheria na taratibu tunazohitaji kutumia ili kunyakua kile kilicho chetu tayari kisheria.

Kwa kuwa watu wengi hawaelewi Ufalme wa Mungu, wala taratibu na sheria za utendaji wake, jambo lisipotokea kama Neno la Mungu linavyosema, watu hufikiri kwamba kosa liko upande wa Mungu, si upande wao.

Hili ndilo jambo nililogundua. Hebu tuseme kwamba umeamua kuruka kutoka kwa jengo refu, bila kianguishio, au kitu chochote, lakini una hakika kwamba ukipigapiga mikono yako haraka kama mbawa unaweza kufika chini salama. Nafikiri utakuwa na ufahamu kuhusu matokeo ya upumbavu huo. Utajua matokeo kwa sababu unaelewa sheria ya mvuto wa ardhi. Utakuwa na uhakika kuhusu matokeo kwa sababu unafahamu kwamba sheria ya mvuto wa ardhi haina ubaguzi wala vipendeleo, na inafanya kazi kwa njia ile ile kila wakati. Vivyo hivyo, unapowasha kibonyezi cha taa, unatarajia taa iwake kwa sababu unaelewa sheria za umeme. Ninaposafiri kwa ndege, ninatarajia ipae kwa sababu ninaelewa sheria ya kuinuliwa juu. Ndege na taa hufanya kazi kila wakati kwa sababu utendakazi wao unategemea sheria ambazo tunaweza kujifunza na kurudia ili kupata matokeo na utendaji sawa kila wakati. Ufalme wa Mungu unafanya kazi kwa kiwango hicho hicho cha hakika.

*Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu*

*sawasawa na mapenzi Yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.*

—1 Yohana 5:14-15

Huu ndio ujasiri wetu. Tukiomba kitu sawasawa na mapenzi ya Mungu, twajua kwamba atusikia, na ikiwa twajua atusikia, tunajua kwamba tuna yale tuliyomwomba. Nina uhakika kuhusu matokeo kwa sababu Mfalme ndiye aliyetunga sheria ya Ufalme Wake. Yeye ataiunga mkono sheria Yake mwenyewe. Maandiko yanaposema anatusikia, hayarejelei kusikia maneno yetu, bali yanarejelea jinsi hakimumu anavyosikiliza kesi ili kutoa haki. Hakimumu hahukumu kwa kutegemea hisia zake, bali yuko pale ili kuhakikisha kwamba sheria inatekelezwa kwa manufaa ya raia wa ufalme huo. Tayari najua matokeo ya kesi mahakamani kabla haijaanza.

Drenda nami tuliona mambo ya ajabu yakitukia tulipoanza kutumia sheria za Ufalme maishani mwetu. Tulitoka kabisa kwa madeni chini ya miaka miwili na nusu. Tuliacha kugawanya chakula kati ya watoto watatu kwenye hoteli na kuanza kulipia magari mapya pesa taslimu, na kujenga nyumba ya ndoto zetu kwa ekari 55, na kuilipia. Tulianzisha kampuni ambazo baada ya miaka mingi zingali zinazalisha mamia ya maelfu ya dola kila mwaka kama faida halisi. Kisha tukaanzisha kanisa katika mji yetu ili kushiriki na watu yale tuliyoyagundua kuhusu Ufalme wa Mungu. Na tulitambua kwamba watu wengi wanataka kujua mambo tuliyojifunza ili waweze kuishi maisha mazuri ya Ufalme wa Mungu. Kwa sababu ya habari hii njema ya Ufalme, kanisa limekua na lina maelfu walio thabiti.

Ingawa nilikuwa nikifundisha mtu yeyote ambaye angesikiliza kuhusu Ufalme karibu kila siku, nilikuwa na hamu ya kufikia kikundi cha watu ambao hawakuwa wamewahi kusikia kuhusu hapo awali ili kuona matokeo yake. Nilifahamu kwamba ili kuona mabadiliko katika maisha ya mtu inapohusu kuelewa kwake kuhusu Ufalme, ningehitaji zaidi ya kikao kimoja ili kueleza ufahamu wa kimsingi wa Ufalme. Wazo nililofikiri lingefua dafu lilitokana na uzoefu wangu nilipokuwa nikilelewa katika kanisa la kimethodisti. Nilipokuwa kijana, tulikuwa na mikutano ya uamsho ya wiki nzima jioni. Kwa hivyo nilikuwa na ndoto ya kuwa na mikutano ya uamsho wa kifedha yaa wiki nzima. Niliona kwamba labda ningehitaji vikao vya jioni tano. Sikuwa nimewahi kufundisha moja kwa moja kuhusu Ufalme hapo awali, na nilikuwa nikijiuliza jinsi ya kuandaa mafundisho. Lakini nilikuwa na hamu ya kujua matokeo ya kufundisha

vikao hivyo vitano vya moja kwa moja maishani mwa watu. Nilianza kusali na kumwomba Mungu anipe fursa ya kuwa na mkutano kama huo. Sharti langu lilikuwa kufundisha kundi la watu ambao hawakuwa wamesikia kuhusu Ufalme hapo awali.

Alasiri moja, nilikutana na rafiki yangu ambaye alikuwa mmishonari huko Albania. Mazungumzo yetu yalihusu vipengele vingi vya kanisa na huduma, na, hatimaye, mazungumzo yetu yalielekea kwa yale ambayo Mungu alikuwa akinionyesha. Larry alikuwa na kongamano lake la huduma la kila mwaka nchini Albania baadaye wakati wa msimu wa vuli na akanialika niwe mmoja wa wanenaji. Sikumwambia nia yangu ilikuwa kufanya vikao vitano, lakini nilifurahi aliposema ningekuwa na vikao vitatu huko. Alisema nilipaswa kujilipia nauli yangu ya kwenda huko na vilevile ya wachungaji wengi waliotaka kuja kwa kongamano, kwa kuwa wakati huo nchi ya Albania ilikuwa maskini sana. Nilikubali na nikafanya mipango ya kuwasili Albania katika msimu wa vuli mnamo 2005.

Hatimaye siku ya safari ilifika, nami nilisisimka sana kuweza kufundisha kikundi cha watu ambao kwa kweli walikuwa wakijifunza maana ya kuwa Mkristo. Nilipofika Albania, Larry alikutana nami kwenye uwanja wa ndege na kusema kwamba mnenaji wake mmoja alikuwa ameghairi mpango wake wa kuja na kwamba sasa nilikuwa na fursa ya kufanya vipindi vitano. Nilitambua kwamba huu ulikuwa usanidi wa Roho Mtakatifu kwa hakika! Nilikuwa na mafundisho ya vipindi vitatu lakini niliomba haraka na kuandika vipindi vingine viwili. Nilikuwa na wasiwasi kidogo kuhusu mwitikio wa wachungaji kwa sababu umaskini wao ulikuwa mwingi na ufsadi ulikuwa kila mahali katika taifa lao.

Niliweza kuona wakati wa kipindi cha kwanza kwamba walikuwa wakisitasita kidogo, lakini nilipoendelea kufundisha yale ambayo Mungu alikuwa amenifundisha, pamoja na hadithi zilizothibitisha kile nilichokuwa nikifundisha, wachungaji walifurahi na kuisimka zaidi. Kufikia kikao changu cha nne, walikuwa wakicheka na kufurahia sana kile walichokuwa wakisikia kiasi kwamba wengine walianza kupiga makelele. Ajabu ni kwamba nilihisi Bwana akiniambia nipokee matoleo katika kipindi cha tano. Nasema ajabu kwa sababu nilikuwa nimelipia wengi wao nauli kuja kwa mkutano na nilijua kwamba walikuwa na pesa kidogo sana au hawakuwa na chochote. Lakini baada ya kutafakari kuhusu jambo hilo, nilitambua kwamba ilibidi wachungaji hawa waitikie yale waliyokuwa wamesikia. Nilikuwa na wasiwasi kidogo kuhusu kumwambia Larry jambo hili, lakini haraka alikubali nipokee matoleo. Bila shaka, sikuwa nikipokea

matoleo kwa manufaa yangu binafsi; sadaka ingebaki huko Albania kwa manufaa ya makanisa yao.

Kipindi cha mwisho kilikuja, na nilikuwa nikifundisha kuhusu imani na jinsi ya kuiachilia, huku nikifafanua baadhi ya sheria nilizokuwa nikifundisha. Mwishoni mwa ibada nilipopokea matoleo, mambo yalilipuka. Watu walianza kupiga makelele na kucheza na upako wa Mungu ulijaa ukumbini. Watu wanne waliokuwa wamesimama mbele na vikapu hawakuweza kusimama. Walikuwa wakilia na kutetemeka chini ya uwepo wa Mungu wakati watu walikuwa wakileta matoleo yao. Sikuwa nimewahi kuona mkutano kama huo, hasa kuhusu pesa!

Mimi na Larry tulipotoka kwa mkutano, tulizungumza kuhusu jinsi tulivyoshangazwa na upako wenye nguvu na mwitikio wa watu jioni hiyo. Baada ya kufika kwa nyumba ya Larry, alikuwa na hamu ya kuhesabu pesa kwa sababu hakuwa amewahi kuwa na mifuko miwili iliyojaa matoleo. Robo ya begi ilikuwa kiasi cha kawaida alichokuwa akipokea wakati wa matoleo katika nyakati za nyuma. Larry alipokuwa akimimina matoleo kwenye meza yake sebuleni, ghafula ukungu mwepesi wa samawati ulijaa chumbani, na upako ambao sikuwa nimewahi kuuhi awali ulitujia. Hatukuweza kufanya lolote ila tu kuanguka kwa viti vyetu. Nilipotazama rundo la pesa lililokuwa mezani mbele yetu, niliona pete ya harusi ya mwanamume katikati ya rundo hilo. Nilijua pete hiyo ilitolewa na mtu ambaye hakuwa na pesa lakini alitoa kila alichokuwa nacho. Nilipoiona pete, Bwana alizungumza nami.

“Ninakuita kwa mataifa ili uwafundishe kuhusu agano Langu la baraka za kifedha, na popote nitakapokutuma, nitalipa gharama yake.”

Nilipigwa na mshangao. Sikuweza kulala kwa siku tatu. Upako huo ulikaa juu yangu kwa majuma kadhaa. Wakati wowote nilipokutana na mtu kutoka kwa taifa lingine, nilihisi upako huo tena. Ingawa matoleo yalibaki kwa manufaa ya makanisa kule Albania, baada ya kufika nyumbani, Larry alinipigia simu na kusema kwamba Bwana alimwambia anitumie ile pete. Nilisisimka sana. Ingawa sikuwa nimemwambia Larry chochote kuhusu shauku yangu ya kuwa na pete hiyo, alisikia kutoka kwa Mungu na akaituma kwangu. Nilitaka pete hiyo iwe ukumbusho wa yale ambayo Bwana aliniambia, na leo nimeiweka kwa ukuta wangu.

Nilipofika nyumbani Ohio, mchungaji mmoja rafiki ya Larry, ambaye ni mchungaji wa kanisa dogo huko Utah, alisikia yaliyotukia Albania na akawasiliana nami nitembelee kanisa lao kama ingewezekana. Alikuwa mchungaji katika eneo walipokaa Wahindi wengi, na akasema



walikuwa maskini sana. Alisema kanisa lake lilikuwa na watu 60 tu, lakini nikamwambia hiyo ilikuwa sawa; na kwamba ningenda kuwatembelea.

Nilikuwa na vikao vitano kama nilivyofanya nchini Albania. Sikuona ukungu wa rangi ya samawati huko, lakini upako ulikuwa na nguvu sana tena.

Sadaka wakati huu ilikuwa ya huduma yangu, kwa hivyo nilibeba mfuko wa matoleo na kurudi nyumbani kule Ohio. Nilipofika ofisini kwangu, nilimkabidhi katibu wangu ule mfuko ili wahesabu matoleo na kuyaweka kwenye benki, kisha nikaelekea kula chakula cha mchana. Ghafula simu yangu ya rununu ililia, na nikaona nambari ya simu ya katibu wangu ikijionyesha kwenye skrini. Nilipoiibu, sikusikia mtu yeyote kwa simu. Nilipokuwa karibu kukata simu, nafikiri nilisikia mtu akilia. “Tracy?” Nikasema. Tracy alijibu huku akijaribu kudhibiti hisia zake. “Mchungaji,” alisema, “nini kilitokea huko Utah na pesa hizi?” “Unamaanisha nini kwa kusema hivyo?” “Vema,” akasema, “nilipoufungua ule mfuko na kumwaga matoleo kwenye meza yangu ili kuyahesabu, ghafla upako wa Mungu ulinjia kwa nguvu sana kiasi cha kuniangusha chini. Katibu mwingine aliyesikia zogo hilo alitoka ofisini kwake kuangalia ni kitu gani kilichokuwa kinaendelea, na nguvu za Mungu zikampiga vivyo hivyo! Ni nini kilifanyikia pesa hizi, Mchungaji?” Nilimweleza kilichotokea Utah na upako mkali uliokuwa pale nilipokuwa nikipokea sadaka, lakini zaidi ya hayo, hakuna kingine kilichotokea. Lazima nikubali kwamba nilivutiwa sana na kile kilichokuwa kikiendelea maana sikuwa nimewahi kusikia au kuona kitu kama hiki hapo awali. Ingawa sikuelewa, lakini ilikuwa dhahiri kwamba upako wa mkutano ulikuwa juu ya pesa hizo! Kweli!

Tulianza na kile tulichoita Kongamano za Mapinduzi ya Kifedha kote nchini, katika makanisa makubwa na madogo, popote ambapo mtu angesikiliza. Ingawa tuliona ukungu wa rangi ya samawati mara kadhaa, upako ulikuwa na nguvu sana kila wakati. Kama ilivyokuwa huko Albania na matoleo ya kanisa la Wahindi huko Utah, upako ulidumu katika matoleo yenyewe. Niliona kwamba baada ya mikutano, wakati matoleo yalikuwa yakihesabiwa, ikiwa ungeshika sarafu kutoka kwa matoleo mkononi mwako ungeanza kutetemeka chini ya nguvu za Roho Mtakatifu. Jambo lingine la kushangaza tulilogundua ni kwamba kila sadaka ilikuwa tofauti. Sadaka hazikuwa na kiwango sawa cha upako juu yao. Nilijifunza baadaye kwamba hii ilikuwa ni matokeo ya imani iliyoachiliwa na mtu binafsi wakati wa matoleo. Ajabu!

Vitabu hivi vitano vya mfululizo wa *Mapinduzi Yako ya Kifedha*

vinahusu vikao vitano nilivyokuwa navyo katika mkutano ule wa kwanza nchini Albania. Vitabu, bila shaka, vimepanuliwa zaidi kuliko kongamano la kwanza. Ninaamini unapoanza kujifunza kuhusu Ufalme kama mimi na Drenda, hilo litabadilisha mtazamo wako wa kila kitu kama ilivyotufanyikia sisi. Kitabu hiki cha tatu katika mfululizo huu, awali kiliitwa *Utajiri kupitia kwa Roho Mtakatifu* nilipokifundisha huko Albania. Ninaamini kauli hiyo bado ni kweli hadi leo. Itakuwa ni mikakati iliyoongozwa na Roho Mtakatifu itakayokufanya ufanikiwe. Ninatumai kwamba kupitia kwa kitabu hiki utajifunza jinsi Roho Mtakatifu anavyofanya kazi ulimwenguni ili kufanikisha mikakati hiyo.

## SURA YA 1

# ETI UNATAKA TUFANYE NINI?

Niliporudi nyumbani kutoka Albania nilikuwa nimepigwa na butwaa. Nilitishwa kidogo na yale Bwana alikuwa amefanya katika maisha yetu na jinsi alivyokuwa ameniambia kwamba nilipaswa kuupeleka ujumbe huu kwa mataifa. Mataifa? Nilikuwa nimemwambia Drenda tulipooana kwamba sitawahi kusafiri, na sikutaka kamwe kwenda kwenye safari ya umisheni kwa mataifa mengine. Lakini bila shaka Mungu alikuwa na mipango mengine. Nilipaswa kwenda kwa mataifa, lakini kwa jinsi gani? Nilikuwa na biashara kubwa Marekani, kanisa la kuongoza, familia ya kulea, na majukumu mengine mengi. Sikuona jinsi ingewezekana kwenda kwa mataifa. Lakini Mungu alikuwa na mpango, mpango ambao haukuhitaji nisafiri, mpango ambao singewahi kuufikiria, wala sikutaka kuufikiria—runinga.

Mimi na Drenda hatukujua lolote kuhusu runinga. Wakati huo, hatukuwa hata tukirekodi ibada zetu kwa video. Lakini Mungu alianza kutuonyesha yale yatakayokuja na jinsi ya kuyashughulikia, na tulikuwa tukihisi msukumo wa kutumia runinga. Jambo la kwanza nililojifunza ni kwamba inagharimu pesa nyingi sana kutumia runinga. Yote yalipojumlishwa, ingegharimu takriban \$300,000 kuzindua mwaka huo wa kwanza wa runinga. Lazima nikubali kwamba nilishtuka kidogo kujua jinsi runinga ilivyokuwa ghali. Shida ni kwamba kanisa lilikuwa tayari limetumia pesa nyingi kujenga jengo la huduma yetu linaloitwa *The Now Center*, na hakukuwa na pesa za ziada za kulipia runinga. Hivyo ndivyo

nilivyomwambia Bwana, kwamba hakukuwa na pesa za kuanzisha huduma ya runinga wakati huo. Nakumbuka alikubaliana nami na kusema, “Sawa, hiyo ndiyo sababu wewe na Drenda mtailipia!”

Kusema tulizidiwa kidogo ni kupuuza, maana tulikuwa katikati ya kujenga jengo lililogharamu kanisa dola milioni sita hadi saba. Kwa kweli mradi wa *The Now Center* wenyewe ulikuwa kazi kubwa ya imani na ulikuwa ukichukua rasilimali zote zilizokuwa zikija kwetu. Zaidi ya hayo, mimi na Drenda tulikuwa tumetoa ahadi ya kuchangia \$250,000 kwa mradi huo, na wakati huo bado hatukuwa tumepata pesa hizo zote. Kutoa \$300,000 za ziada katika mwaka huo huo, lilionekana kama jambo lisilowezekana.

Nilifahamu kwamba hii ilikuwa safari ya Bwana, na ahadi Yake ya kunipa pesa popote aliponituma ilikuwa bado inasikika rohoni mwangu. Lakini kiasili haikujalisha jinsi nilivyoitazama gharama, sikuwa na uwezo

**NILIFAHAMU KWAMBA  
MUNGU NI MWAMINIFU  
KUTIMIZA NENO LAKE,  
NA NILIJUA KWAMBA  
INGENIBIDI NIWE NA IMANI,  
HUKU NIKIMTUMAINI YEYE  
ANIONYESHE LA KUFANYA.**

wa kutambua jinsi mimi na Drenda tungeweza kulipa \$300,000 juu ya kila kitu kingine tulichokuwa tukifanya. Nilifahamu kwamba Mungu ni mwaminifu kutimiza Neno Lake, na nilijua kwamba ingenibidi niwe na imani, huku nikimtumaini Yeye anionyeshe la kufanya. Ningependa kukwambia kwamba nilikuwa na ujasiri na sikuwa na wasiwasi juu ya

uamuzi huu, lakini huo utakuwa uongo. Kanisa lilikuwa likitumia kila senti iliyokuja kwa ajili ya jengo hilo. Pesa zangu zote za kibinafsi zilikuwa zikitumika kulipia ahadi yangu ya dola 250,000, na maeneo mengine mengi katika biashara yangu pia yalihatiji kufadhiliwa mwaka huo. Hakukuwa na pesa zozote za kugharamikia uzinduzi wa huduma ya runinga!

Mimi na Drenda tulikuwa katika likizo ya wiki mbili huko Hawaii, na nilipaswa kutia saini kwa mikataba ili kuanzisha huduma yetu ya runinga mara tu tuliporudi nyumbani. Hakika napenda Hawaii, lakini lazima nikubali ilikuwa vigumu kidogo kustarehe kabisa maana uzito wa uamuzi huu ambao ningekabiliana nao nilipofika nyumbani ulikuwa mgumu kuondoa akilini mwangu. Kando na suala la kutokuwa na pesa, sikuwa tayari kabisa kuhudumu kwenye televisheni kwa sababu nilihisi aibu kuzungumzia kamera. Ningeweza kuzungumza na maelfu ya watu kwenye mkutano, lakini mbele ya kamera ya runinga, nilikuwa nikiingiwa na hofu. Kuwa na hayo yote kichwani na rohoni mwangu, kulinifanya nipambane

na roho ya woga kuhusu kufanya uamuzi huo.

Ingawa nilifahamu kwamba nilikuwa nimesikia kabisa kutoka kwa Bwana, bado nilikuwa nikikabiliwa na ukweli kwamba hakukuwa na pesa. Biashara yangu tayari ilikuwa imeshinikizwa hadi mwisho kifedha, na sikuwa na uwezo wa kuona jinsi jambo hili lingelivyowezekana. Ndio, ilikuwa hofu, ndio, ilikuwa kutoamini. Najua hilo. Nasema ukweli mtupu hapa. Nilijua ilinibidi nishikilie Neno na kuyatoa macho yangu kwa kile nilichokuwa nacho na kuendelea kuitazama ile pete. Alisema atalipa gharama ya kwenda kwa mataifa! Wakati huo, tulipata sarafu ya dhahabu katika moja ya matoleo yetu. Kusema kweli, sikuwa nimewahi kuona sarafu ya dhahabu hapo awali. Nilipokuwa nimeishika mkononi, Bwana alinena nami. “Kama vile nilivyomwonyesha Petro mahali ambapo sarafu ya kulipa kodi ilikuwa, nitakuonyesha mahali pa kupata pesa za kulipia runinga.”

Nilibeba sarafu hiyo ya dhahabu tulipoenda kwa likizo yetu kule Hawaii, na nilikuwa nikitembea kando ya ufuo na kusali, huku nikiwa nimeishikilia ili kunikumbusha kwamba Mungu alikuwa amegharamikia huduma ya runinga. Ziara zangu za maombi nilipokuwa nikitembea ufukweni zilikuwa kitu kama hiki. Baada ya kuomba katika Roho kwa muda, amani kuhusu kutia saini kwa mkataba ingeongezeka kisha ningeanza kurudi chumbani, lakini baada ya kutembea kama futi 20 hadi 50 juu ya kilima kilichokuwa hapo, akili yangu ingeanza kunipigia kelele tena kwamba haingewezekana kiasili kupata fedha hizo. Ukweli ni kwamba hatukuwa na pesa, hatukujua jinsi ya kuhudumu kwa runinga, hatukuwa na vifaa vyovyote, na kadhalika. Lakini katika roho yangu, niliendelea kusikia kile ambacho Bwana aliniambia huko Albania, kwamba popote aliponituma, Yeye angelipia gharama. Hili lilikuwa likifanyika katika mwezi wa Mei, na, kwa kweli, ilitubidi kuwa na \$300,000 kufikia mwisho wa mwaka ili kuweza kufaulu, jambo ambalo lilifanya tuwe na mlima mkubwa zaidi wa kupanda.

Roho ya woga pia ilikuwa ikinisemesha, huku ikijaribu nia yangu ya kushikilia kile ambacho Mungu alikuwa ameniambia. “Huwa unafundisha uadilifu wa kifedha, na itaonekanaje usipoweza kulipa bili zako?” Kwa hivyo tena ningerudi ufukweni moja kwa moja, huku nikiomba na kufanya upya akili yangu kulingana na Neno la Mungu hadi nilipopata amani. Nilienda mbele na nyuma, na mashindano katika akili na roho yangu kuhusu mkataba huu kwa muda wa wiki moja hadi nilipohisi kwamba yote yangekuwa sawa, na hofu haingeweza kunitesa tena na mawazo mabaya. Mimi na Drenda hatukujua pesa hizo zingetoka wapi, lakini tulijua tulikuwa tumemsikia Mungu. Kwa hivyo tuliporudi nyumbani, nilitia saini kwa mkataba, kisha

tukaenda kufikiria jinsi ya kuendesha huduma ya runinga.

Kuhusu pesa, cha kushangaza ni kwamba, nilipigiwa simu kutoka Atlanta na mtu ambaye sikumjua, miezi michache kabla ya likizo yetu ya Hawaii. Alisema alikuwa amesoma kitabu changu kuhusu fedha na alikuwa amekipenda. Wakati huo, nilikuwa nikijichapishia vitabu vyangu na havikuwa vimeuzwa nje ya jiji letu. Lakini inaonekana mmoja wa wafanyakazi wangu alipokuwa akienda likizoni kule Atlanta alikutana na mtu huyu kwa nasibu kwenye uwanja wa ndege, kisha wakaanza mazungumzo kuhusu ile kazi aliyioifanya. Ilitokea tu kwamba mfanyakazi wangu alikuwa na kitabu changu ambacho alimpa.

Kwa hiyo baada ya kukisoma, alisema kwamba alipendezwa nacho sana kiasi kwamba ilimbidi azungumze nami. Tulizungumza kwa muda mrefu, naye akataja kwamba mwito wake mkuu kama mwinjilisti ulikuwa kusafiri kwenda kwa nchi za kigeni kufanya huduma. Aliuliza ikiwa tungeweza kukutana wakati fulani, nami nikasema kwamba ningekuwa katika uwanja wa ndege wa Atlanta baada ya mwezi mmoja nikiwa katika safari ya kwenda kwa kongamano, ambalo lingekuwa baada ya likizo yangu. Tulikubaliana kukutana. Hatimaye tulipokutana tulikuwa na mazungumzo mazuri. Nilifurahia sana kusikia hadithi zake zote za miujiza na hatari ambazo mara nyingi alipaswa kukabiliana nazo katika safari zake. Lakini mada ya fedha ilitufanya tuunganike kweli kweli. Ilionekana alivutiwa na kitabu changu na hadithi yangu ya kutoka kwa madeni.

Wakati wa mazungumzo yetu, aliniambia kwamba alikuwa amerudi kutoka Charlotte, ambako alikuwa mgeni wa kipindi cha televisheni, na alihisi hadithi yangu ya kifedha ingekuwa hadithi nzuri katika kipindi hicho. Alisema alitaka kuwapatia kitabu changu na kuwafahamisha kunihusu. Nilishtushwa kidogo na yote hayo.

Hata sikuwa nimesikia kuhusu kipindi cha televisheni alichotaja, lakini hakika, baada ya wiki chache, nilipokea simu kutoka kwa mkurugenzi wa kipindi hicho ambaye aliniuliza ikiwa ningependa kuwa mgeni katika kipindi hicho. Moja ya mahitaji ya kuwa kwenye kipindi hicho ni kuwa na bidhaa ambazo wanaweza kutangaza hewani. Kwa hivyo nilimwaambia nilikuwa na CD tano za mafundisho yangu ya Mapinduzi ya Kifedha. Walisema hiyo ilikuwa sawa, kisha tukakubaliana bei ambayo wangetangaza. Bila shaka niliwapa mfululizo huo wa CD kwa bei ya jumla, lakini hata hivyo, niliruhusu faida fulani kuingia kwa huduma yetu. Ajabu ni kwamba, kipindi kilifanikiwa sana, na tuliua maelfu na maelfu ya CD hizo. Hilo pekee lilileta maelfu ya dola kwa bajeti yetu ya huduma ya runinga kutoka

mahali ambapo sikupafahamu kamwe nilipotia saini kwa mkataba huo.

Kisha tukio lingine la kushtua. Mtu katika kanisa langu ambaye alikuja akiwa na matatizo ya kifedha na alikuwa karibu kufukuzwa kutoka kwa nyumba yake miaka michache awali, alikuja kwangu na kusema alitaka kusaidia kufadhili vipindi vya runinga. Alikuwa akifanya yale aliyosikia yakihubiriwa kuhusu Ufalme na hakuwa maskini tena. Alinipa dola 120,000 kwa ajili ya huduma yetu ya runinga!

Tulipohesabu mauzo ya CD, fedha kutoka kwa rafiki yangu kanisani, na zawadi nyinginezo zilizokuja, haikutubidi mimi na Drenda tutoe pesa zetu zozote katika mwaka huo wa kwanza wa huduma ya runinga! Mungu alikuwa mwaminifu kwa neno Lake. Alisema angelipa gharama, na alitimiza hilo. Sawa, nusu ya shida ilikuwa imeshughulikiwa, lakini nilikuwa na shida nyingine kubwa kama ile ya fedha ambayo ilihitaji kutatuliwa. Kama nilivyosema hapo awali, sikujua chochote kuhusu huduma ya runinga!

Mwaka huo katika msimu wa vuli, Drenda alipokuwa akihudhuria kongamano kubwa la Kikristo la wanawake, alialikwa kuungana na wageni waliokuja kwa kongamano katika chumba fulani cha mapumziko katikati ya mikutano. Ilikuwa ni heshima kubwa kwa Drenda kualikwa huko, na alifurahi kwenda. Baada ya kikao kimoja, alipokuwa ameketi kula chakula cha mchana, mwanamke mmoja ambaye hakuwa amewahi kukutana naye awali aliketi karibu naye. Baada ya kusemezana kidogo kujihusu, mwanamke huyo aliuliza ghafula, “Kwa hivyo, mmeanza huduma ya runinga?” Drenda alishtuka kidogo, lakini akajibu, “La, lakini tumekuwa tukifikiria juu yake.” Mwanamke huyo akasema, “Vema, ikiwa mtaanza, mpigie simu jamaa huyu, naye anaweza kuwasaidia.” Drenda aliandika na kuiweka kwenye mkoba nambari na anwani ya barua pepe ambayo mwanamke huyo alimpa.

Wiki kadhaa zilipita pale nyumbani, na kwa kweli alisahau kipande cha karatasi alichokuwa ameweka kwenye mkoba wake. Lakini usiku mmoja, baada ya kukipata, aliamua kumtumia kijana huyo barua pepe ili aone angesema nini. Ilionekana alipendezwa maana alimwomba amtumie CD zangu za mafundisho ya *Mapinduzi ya Kifedha*, jambo ambalo tulifanya. Baada ya juma moja hivi, msaidizi wake alitupigia simu tena kisha akasema kwamba bila shaka bwana huyo alipendezwa na alitaka kukutana nasi kwenye kongamano la kila mwaka la Watangazaji wa Kitaifa wa Kidini, ambalo lingefanyika baada ya majuma machache. Tulimwambia tungehudhuria.

Mimi na Drenda tulikuwa katika likizo ya wiki mbili huko Hawaii, na nilipaswa kutia saini kwa mikataba ili kuanzisha huduma yetu ya

runinga mara tu tuliporudi nyumbani. Hakika napenda Hawaii, lakini lazima nikubali ilikuwa vigumu kidogo kustarehe kabisa maana uzito wa uamuzi huu ambao ningekabiliana nao nilipofika nyumbani ulikuwa mgumu kuondoa akilini mwangu. Kando na suala la kutokuwa na pesa, sikuwa tayari kabisa kuhudumu kwenye televisheni kwa sababu nilihisi aibu kuzungumzia kamera. Ningeweza kuzungumza na maelfu ya watu kwenye mkutano, lakini mbele ya kamera ya runinga, nilikuwa nikiingiwa na hofu. Kuwa na hayo yote kichwani na rohoni mwangu, kulinifanya nipambane na roho ya woga kuhusu kufanya uamuzi huo.

Ingawa nilifahamu kwamba nilikuwa nimesikia kabisa kutoka kwa Bwana, bado nilikuwa nikikabiliwa na ukweli kwamba hakukuwa na pesa. Biashara yangu tayari ilikuwa imeshinikizwa hadi mwisho kifedha, na sikuwa na uwezo wa kuona jinsi jambo hili lingelivyowezekana. Ndio, ilikuwa hofu, ndio, ilikuwa kutoamini. Najua hilo. Nasema ukweli mtupu hapa. Nilijua ilinibidi nishikilie Neno na kuyatoa macho yangu kwa kile nilichokuwa nacho na kuendelea kuitazama ile pete. Alisema atalipa gharama ya kwenda kwa mataifa! Wakati huo, tulipata sarafu ya dhahabu katika moja ya matoleo yetu. Kusema kweli, sikuwa nimewahi kuona sarafu ya dhahabu hapo awali. Nilipokuwa nimeishika mkononi, Bwana alinena nami. “Kama vile nilivyomwonyesha Petro mahali ambapo sarafu ya kulipa kodi ilikuwa, nitakuonyesha mahali pa kupata pesa za kulipia runinga.”

Nilibeba sarafu hiyo ya dhahabu tulipoenda kwa likizo yetu kule Hawaii, na nilikuwa nikitembea kando ya ufuo na kusali, huku nikiwa nimeishikilia ili kunikumbugha kwamba Mungu alikuwa amegharamikia huduma ya runinga. Ziara zangu za maombi nilipokuwa nikitembea ufukweni zilikuwa kitu kama hiki. Baada ya kuomba katika Roho kwa muda, amani kuhusu kutia saine kwa mkataba ingeongezeka kisha ningeanza kurudi chumbani, lakini baada ya kutembea kama futi 20 hadi 50 juu ya kilima kilichokuwa hapo, akili yangu ingeanza kunipigia kelele tena kwamba haingewezekana kiasili kupata fedha hizo. Ukweli ni kwamba hatukuwa na pesa, hatukujua jinsi ya kuhudumu kwa runinga, hatukuwa na vifaa vyovyote, na kadhalika. Lakini katika roho yangu, niliendelea kusikia kile ambacho Bwana aliniambia huko Albania, kwamba popote aliponituma, Yeye angelipia gharama. Hili lilikuwa likifanyika katika mwezi wa Mei, na, kwa kweli, ilitubidi kuwa na \$300,000 kufikia mwisho wa mwaka ili kuweza kufaulu, jambo ambalo lilifanya tuwe na mlima mkubwa zaidi wa kupanda.

Roho ya woga pia ilikuwa ikinisemesha, huku ikijaribu nia yangu ya kushikilia kile ambacho Mungu alikuwa ameniambia. “Huwa unafundisha



uadilifu wa kifedha, na itaonekanaje usipoweza kulipa bili zako?” Kwa hivyo tena ningerudi ufukweni moja kwa moja, huku nikiomba na kufanya upya akili yangu kulingana na Neno la Mungu hadi nilipopata amani. Nilienda mbele na nyuma, na mashindano katika akili na roho yangu kuhusu mkataba huu kwa muda wa wiki moja hadi nilipohisi kwamba yote yangekuwa sawa, na hofu haingeweza kunitesa tena na mawazo mabaya. Mimi na Drenda hatukujua pesa hizo zingetoka wapi, lakini tulijua tulikuwa tumemsikia Mungu. Kwa hivyo tuliporudi nyumbani, nilitia saina kwa mkataba, kisha tukaenda kufikiria jinsi ya kuendesha huduma ya runinga.

Kuhusu pesa, cha kushangaza ni kwamba, nilipigiwa simu kutoka Atlanta na mtu ambaye sikumjua, miezi michache kabla ya likizo yetu ya Hawaii. Alisema alikuwa amesoma kitabu changu kuhusu fedha na alikuwa amekipenda. Wakati huo, nilikuwa nikijichapishia vitabu vyangu na havikuwa vimeuzwa nje ya jiji letu. Lakini inaonekana mmoja wa wafanyakazi wangu alipokuwa akienda likizoni kule Atlanta alikutana na mtu huyu kwa nasibu kwenye uwanja wa ndege, kisha wakaanza mazungumzo kuhusu ile kazi aliyofanya. Ilitokea tu kwamba mfanyakazi wangu alikuwa na kitabu changu ambacho alimpa.

Kwa hiyo baada ya kukisoma, alisema kwamba alipendezwa nacho sana kiasi kwamba ilimbidi azungumze nami. Tulizungumza kwa muda mrefu, naye akataja kwamba mwito wake mkuu kama mwinjilisti ulikuwa kusafiri kwenda kwa nchi za kigeni kufanya huduma. Aliuliza ikiwa tungeweza kukutana wakati fulani, nami nikasema kwamba ningekuwa katika uwanja wa ndege wa Atlanta baada ya mwezi mmoja nikiwa katika safari ya kwenda kwa kongamano, ambalo lingekuwa baada ya likizo yangu. Tulikubaliana kukutana. Hatimaye tulipokutana tulikuwa na mazungumzo mazuri. Nilifurahia sana kusikia hadithi zake zote za miujiza na hatari ambazo mara nyingi alipaswa kukabiliana nazo katika safari zake. Lakini mada ya fedha ilitufanya tuunganike kweli kweli. Ilionekana alivutiwa na kitabu changu na hadithi yangu ya kutoka kwa madeni.

Wakati wa mazungumzo yetu, aliniambia kwamba alikuwa amerudi kutoka Charlotte, ambako alikuwa mgeni wa kipindi cha televisheni, na alihisi hadithi yangu ya kifedha ingekuwa hadithi nzuri katika kipindi hicho. Alisema alitaka kuwapatia kitabu changu na kuwafahamisha kunihusu. Nilishtushwa kidogo na yote hayo.

Hata sikuwa nimesikia kuhusu kipindi cha televisheni alichotaja, lakini hakika, baada ya wiki chache, nilipokea simu kutoka kwa mkurugenzi wa kipindi hicho ambaye aliniuliza ikiwa ningependa kuwa mgeni katika

kipindi hicho. Moja ya mahitaji ya kuwa kwenye kipindi hicho ni kuwa na bidhaa ambazo wanaweza kutangaza hewani. Kwa hivyo nilimwaambia nilikuwa na CD tano za mafundisho yangu ya Mapinduzi ya Kifedha. Walisema hiyo ilikuwa sawa, kisha tukakubaliana bei ambayo wangetangaza. Bila shaka niliwapa mfululizo huo wa CD kwa bei ya jumla, lakini hata hivyo, niliruhusu faida fulani kuingia kwa huduma yetu. Ajabu ni kwamba, kipindi kilifanikiwa sana, na tuliua maelfu na maelfu ya CD hizo. Hilo pekee lilileta maelfu ya dola kwa bajeti yetu ya huduma ya runinga kutoka mahali ambapo sikupafahamu kamwe nilipotia saini kwa mkataba huo.

Kisha tukio lingine la kushtua. Mtu katika kanisa langu ambaye alikuja akiwa na matatizo ya kifedha na alikuwa karibu kufukuzwa kutoka kwa nyumba yake miaka michache awali, alikuja kwangu na kusema alitaka kusaidia kufadhili vipindi vya runinga. Alikuwa akifanya yale aliyosikia yakihubiriwa kuhusu Ufalme na hakuwa maskini tena. Alinipa dola 120,000 kwa ajili ya huduma yetu ya runinga!

Tulipohesabu mauzo ya CD, fedha kutoka kwa rafiki yangu kanisani, na zawadi nyinginezo zilizokuja, haikutubidi mimi na Drenda tutoe pesa zetu zozote katika mwaka huo wa kwanza wa huduma ya runinga! Mungu alikuwa mwaminifu kwa neno Lake. Alisema angelipa gharama, na alitimiza hilo. Sawa, nusu ya shida ilikuwa imeshughulikiwa, lakini nilikuwa na shida nyingine kubwa kama ile ya fedha ambayo ilihitaji kutatuliwa. Kama nilivyosema hapo awali, sikujua chochote kuhusu huduma ya runinga!

Mwaka huo katika msimu wa vuli, Drenda alipokuwa akihudhuria kongamano kubwa la Kikristo la wanawake, alialikwa kuungana na wageni waliokuja kwa kongamano katika chumba fulani cha mapumziko katikati ya mikutano. Ilikuwa ni heshima kubwa kwa Drenda kualikwa huko, na alifurahi kwenda. Baada ya kikao kimoja, alipokuwa ameketi kula chakula cha mchana, mwanamke mmoja ambaye hakuwa amewahi

**WAZO MOJA RAHISI  
KUTOKA KWA ROHO  
MTAKATIFU LILIBADILISHA  
MAISHA YETU MILELE!  
NAAM, ILITUBIDI  
TULIFANYIE KAZI, LAKINI  
MUNGU ALITUONYESHA  
JINSI YA KUFANYA HIVYO.**

kukutana naye awali aliketi karibu naye. Baada ya kusemezana kidogo kujihusu, mwanamke huyo aliuliza ghafula, “Kwa hivyo, mmeanza huduma ya runinga?” Drenda alishtuka kidogo, lakini akajibu, “La, lakini tumekuwa tukifikiria juu yake.” Mwanamke huyo akasema, “Vema, ikiwa mtaanza, mpigie simu jamaa huyu, naye anaweza kuwasaidia.” Drenda aliandika na kuiweka kwenye

mkoba nambari na anwani ya barua pepe ambayo mwanamke huyo alimpa.

Wiki kadhaa zilipita pale nyumbani, na kwa kweli alisahau kipande cha karatasi alichokuwa ameweka kwenye mkoba wake. Lakini usiku mmoja, baada ya kukipata, aliamua kumtumia kijana huyo barua pepe ili aone angesema nini. Ilionekana alipendezwa maana alimwomba amtumie CD zangu za mafundisho ya *Mapinduzi ya Kifedha*, jambo ambalo tulifanya. Baada ya juma moja hivi, msaidizi wake alitupigia simu tena kisha akasema kwamba bila shaka bwana huyo alipendezwa na alitaka kukutana nasi kwenye kongamano la kila mwaka la Watangazaji wa Kitaifa wa Kidini, ambalo lingefanyika baada ya majuma machache. Tulimwambia tungehudhuria.

Mimi na Drenda tuliendesha gari letu hadi kwa mkutano tukiwa na wasiwasi kidogo. Nilikuwa nimenunua suti mpya nyeusi kwa ajili ya mkutano huo na hakika sikujua cha kutarajia. Alikuwa ametuambia tukutane naye katika chumba chake cha hoteli ili kujadili suala la huduma ya runinga. Tulipokuwa tukielekea kwa chumba hicho, nakumbuka tulipanda na kushuka ukumbini mara kadhaa kabla ya kufika kwa chumba kilichokuwa na milango miwili. Tulipoingia chumbani, tulishangaa kukuta kundi zima la watu waliokuwa wakisubiri kuzungumza nasi. Viti vilikuwa vimepangwa katika nusu duara, na mimi na Drenda tuliketi tukivitazama viti. Hatukuwa tumewahi kukutana na yeyote kati yao hapo awali, lakini wote walikuwa wamevalia kitaalamu sana.

Tulianza na mazungumzo mafupi, kisha wakaanza kuuliza maswali kuhusu shauku yetu ya kufanya huduma ya runinga. Bado nakumbuka swali la kwanza, “Kwa nini mnataka kufanya huduma ya runinga?” Ingawa sikujua wakati huo, watu waliokuwa katika chumba hicho walikuwa watendaji wa ngazi za juu kutoka nyanja mbalimbali za vipindi vya runinga. Bila shaka yule mtu tuliyezungumza naye alikuwepo, lakini pia kulikuwa na watengenezaji wa vipindi, waenezaji wa habari, na wengineo ambao waliuliza maswali magumu. Kwa ujumla, nilihisi kwamba mkutano ulikuwa mzuri. Tulikuwa peke yetu tu mimi na Drenda, na tulishiriki hadithi yetu ya kile Mungu alikuwa ametufanyia bila kujaribu kumshawishi mtu yeyote. Ilionekana kwamba wote walifurahia maono na shauku yetu, na hivyo wakatuambia kwamba wangetupigia simu tena baada ya wiki chache ili kujadili maelezo zaidi.

Kwa hiyo baada ya wiki kadhaa, tulizungumza tena; na wakati huu, sote tuliamua kuwa na kikao halisi cha kupanga kipindi chetu cha runinga. Tulikuwa tumefanya uamuzi kwamba tungerekodi vipindi hivyo nyumbani

kwetu, kwa hiyo yule bwana ambaye Drenda alikuwa amekutana naye aliomba kwamba mkutano uliofuata ufanyike nyumbani kwetu. Alitaka kuona nyumba yetu ili kujua ikiwa hilo lingewezekana kweli.

Basi siku ilifika naye akaja nyumbani kwetu, na tukaketi sote kuzungumza. Hadi wakati huo, kwa kweli sikujua mengi kuhusu historia yake katika kazi ya televisheni, ila tu kwamba yule bibi kwenye mkutano aliohudhuria Drenda alikuwa amempa nambari yake ya simu. Lakini tulipoketi, alianza kutueleza vipindi vyote vya televisheni alivyokuwa amevitayarisha na vile alivyokuwa akivitengeneza wakati huo. Majina yote ya watu aliwataja yalikuwa yalikuwa majina maarufu sana! Niliketi pale kwa mshangao, “Mungu, ulimletaje mtu huyu, kutoka Los Angeles, hadi kwa nyumba yangu iliyo kwenye barabara ndogo yenye vumbi, katikati ya mahali patupu?” Alikubali kazi ya kuandaa vipindi vyetu vyote, kukiwemo kurekodi video, kuhariri, vna kuvitayarisha kwa bei nafuu sana. Pia sote tulikubali kwamba mwanzoni tungerekodi vipindi hivyo sebuleni mwetu.

Siku ya kwanza ya kurekodi ilifika, na nitakubali nilikuwa na wasiwasi kuhusu hilo. Kama nilivyosema, sikuwa na uzoefu wa kuhudumu katika runinga. Sikujua jinsi kipindi cha televisheni kilivyopaswa kupangwa, wala kuzungumzia kamera tu hapo awali; yote yalikuwa mambo mapya. Nilikuwa na msisimko wa kueneza hadithi yangu kuhusu Ufalme, lakini kufanya hivyo kupitia kwa televisheni lilikuwa jambo la kutisha kwangu na nilihitaji kupata ushindi juu yake.

Cha kuhuzunisha sana ni kwamba siku ya kurekodi vipindi hivyo jambo gumu zaidi lilitukia. Yule mtu aliyepaswa kurekodi vipindi vyetu kwa wiki nzima aliondoka usiku wa manane. Mtoto wake mdogo alikuwa amekanyagwa na kuuawa na gari la jirani lilipokuwa likirudi nyuma. Msaidizi wake alitueleza kilichokuwa kimetokea, na tukaamua kutomwambia mtu yeyote hadi baada ya kumaliza kurekodi vipindi hivyo. Haikuwa rahisi lakini kwa jinsi fulani tuliweza kupata nguvu ya kupitia hilo. Tulirekodi vipindi vitatu siku hiyo, na tukawa rasmi kwenye televisheni. Ajabu!

Mara vipindi vyetu vilipoanza kupeperushwa kwenye televisheni, hatukujua jinsi ya kuendelea kuvilipia. Lakini Mungu alianza kutufundisha kwamba hangetoa dola 300,000 tu tulizohitaji ili kuanzisha huduma ya televisheni, lakini pia kwamba angeendelea kuvilipia. Tulikuwa na mengi ya kujifunza. Wajua, hatukuwa tumefikiria kwamba watu wangetaka kutoa matoleo ya kifedha kama mbegu katika huduma yetu ya runinga; ndivyo tulivyokuwa wajinga.

Nakumbuka Tracy, katibu wangu, alinipigia simu kutoka ofisini mara

baada ya vipindi vyetu kuanza kupeperushwa. Nilipomjibu nilihisi alikuwa na mshtuko. Sauti yake ilikuwa ikitetemeka. “Mchungaji,” akasema, “mtu aliyetazama kipindi chako ametutumia hundi ya dola 500. Na Mchungaji, nilipoiokota, nilihisi upako ule ule uliokuwa kwenye zile pesa ulizorudi nazo kutoka kwa mkutano wa kanisa la Wahindi.” “Una uhakika?” Nikagugumiza. “Hakika mtu alitutumia pesa?” Sikuwa nimewahi kufikiria kwamba watu wangetutumia pesa za kusaidia kupeperusha vipindi vyetu hadi hundi hiyo ilipojitokeza. Lakini, Mungu asifiwe, watu wamekuwa wakituma tangu wakati huo, na tumekuwa tukipeperusha vipindi vyetu kote ulimwenguni kila siku! Bili zimeongezeka hadi mamilioni kwa mwaka, lakini Mungu daima ametimiza neno Lake kwangu. Yeye huzigharamikia kila wakati.

Kitabu hiki kinahusu kusikia na kuongozwa maishani na Roho wa Mungu. Hadithi yetu kuhusu huduma ya runinga ni mfano mzuri wa jinsi Roho Mtakatifu anavyowaongoza watu kufanya mambo makubwa

**“JE, KUNA YEYOTE  
KATI YENU MWENYE  
MATATIZO? ANAPASWA  
KUOMBA”**

**—YAKOBO 5:13**

nisingejua jinsi ya kumsikia Roho Mtakatifu. Nyakati zingine, sisi sote hukabiliwa na hali ngumu zinazoweza kuonekana kama hazina tumaini. Lakini Mungu ana majibu.

zaidi ambayo hawakuwa wamewahi kuota kuwezekana. Kila kitu ambacho Mungu ametufanyia maishani mwetu kimetokana na uwezo wetu wa kufahamu jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi, na pia kuweza kumsikia anapotupatia mwongozo, hekima, na majibu tunayohitaji. Hadithi ambayo nimekusimulia isingetokea kama

*“Je, kuna yeyote kati yenu mwenye matatizo? Anapaswa kuomba” (Yakobo 5:13).*

Mbona uombe? Kwa sababu unahitaji kusikia jibu, mwelekeo, na suluhisho la tatizo lako. Mimi na Drenda tumegundua mara nyingi kwamba, Mungu anaweza kufanya zaidi ya vile tunavyoweza kuwazia tunapokabiliwa na matatizo. Atakusaidia kwa kukupa masuluhu na mikakati ya kipekee na wakati mwingine ya kushangaza ili uweze kushinda hali unazohisi kwamba haziwezekani. Mara nyingi, uwezo wako wa kusikia jibu unaweza kuwa suluhu kubwa katika jambo linalofanikisha au lisilofanikisha na maisha au kifo. Nitazungumza sana kuhusu kusikia sauti ya Roho Mtakatifu katika

kitabu hiki, lakini kwanza, subiri nikupe kielelezo kingine cha jinsi Roho Mtakatifu anavyoweza kukusaidia katika nyakati ngumu.

Tulipozindua mradi wetu wa kujenga jengo letu tunaloliita *The Now Center*, lililoghharimu dola milioni 6.5, tulikusanya pesa taslimu milioni 2.5 hapo awali na pia tulikopa kutoka kwa benki. Pia tulikuwa na pesa zilizokuja wakati wa ujenzi wenyewe wa kipindi cha miezi 18. Ulikuwa mradi mkubwa kwa kanisa la watu 550 kuanzisha. Tulifanikiwa katika msimu wa vuli wa mwaka wa 2007, na kila kitu kilikuwa sawa hadi msimu wa masika wa mwaka wa 2008. Labda unaweza kukumbuka mdororo wa uchumi wa mwaka wa 2008. Naam, tulikuwa katika harakati za ujenzi katikati yake. Bei ya kila kitu ilipanda kupita kiasi! Bei za chuma zetu ziliishia kuwa zaidi ya \$300,000 zaidi ya bei ya zabuni iliyonukuliwa. Huo ni mfano mmoja tu. Mradi mzima ulipita bajeti yetu bei za bidhaa zilipopanda mwaka huo.

Kuelekea mwisho wa 2008, benki katika eneo letu, na kote nchini, zilikuwa zikighairi mikopo na kuhitaji kulipwa madeni yote maana uchumi ulikuwa ukizidi kuzorota. Mjenzi wetu alitujia siku moja wakati wa kufanya malipo, ambayo tayari yalikuwa yameidhinishwa na benki yetu. Alihitaji kuwalipa wakandarasi wake wadogo na ankara nyingine ambazo hazikuwa zimelipwa, pesa ambazo tayari alikuwa ametumia. Hundi ya dola milioni moja ilipaswa kugharamiwa na ufadhili wa benki uliopangwa awali maana tayari tulikuwa tumemaliza pesa zetu taslimu wakati huo. Lakini hakukuwa na hundi ya dola milioni moja. Tulishangaa kupata kwamba benki ilikuwa imeondoa ofa yao na kughairi mkopo wetu. Tena, haikuwa benki yetu tu; bali benki zote za mji yetu. Vichwa vya habari wiki hiyo katika kurasa za mbele za majarida yetu ya mtaani vilihusu benki yetu. Ilikuwa ameachisha kazi wafanyakazi 550 wiki hiyo hiyo na ilikuwa ikipambana ili kunusurika kutokana na msukosuko huo wa kifedha.

Tena, suala lililokuwepo ni kwamba mjenzi wetu alihitaji kuwalipa wakandarasi wake wadogo na kulipia vifaa ambavyo tayari alikuwa ametumia. Hundi hii ya dola milioni moja haikuwa ya kitu ambacho angehitaji katika siku za usoni. Tayari alikuwa ametumia milioni hiyo! Sasa kulikuwa na kampuni na familia zilizohitaji tumlipe mjenzi wetu ili aweze kuwalipa. Kama sisi, alidhani benki ingeendelea kutimiza ahadi yao. Sasa nini? Mtu hufanya nini katika hali kama hii? Sikuwa na dola milioni moja mkononi, na sikutaka kwenda kuwaomba pesa washirika wa kanisa letu. Kando na hili, huduma ya runinga ilikuwa inazidi kuwa ghali kwa sababu tulikuwa tumeipanua kwenye stesheni nyingi zaidi. Gharama yetu sasa ilikuwa \$50,000 kila mwezi. Tungefanya nini ila kile Yakobo 5:13

inachosema tufanye, kuomba!

Ilitokea tu kwamba tulikuwa tumeshinda safari nyingine ya kwenda Hawaii kupitia kwa biashara yangu wakati huo. Niligundua benki ilikuwa imeghairi mkopo siku chache tu kabla yetu kuondoka. Nilipokuwa nikitembea katika uwanja wa ndege ili kupanda ndege yetu kwenda Maui, lazima nikubali kwamba bado kidogo nilikuwa na mshtuko. Akili yangu ilikuwa imechanganyikiwa kupita kiasi. Lakini nilipokuwa pale katika uwanja wa ndege, nikiwa na hisia za kutaka kujihurumia, nilisikia sauti ya Bwana. Alisema, “Inua Fimbo Yako!” Niliposimama na kutafakari kile Bwana alichokuwa akijaribu kuniambia, ghafla nilielewa.

Hiki ndicho hasa Mungu alichomwambia Musa wakati Waisraeli hawakuwa na mahali pa kwenda jeshi la Farao lilipowafinyilia katika Bahari Nyekundu. Mungu alimwambia Musa ainuie fimbo yake juu ya bahari, na alipofanya hivyo, Bahari iligawanyika, na kuwatengenezea Israeli njia ya kuvuka na kutoroka. Fimbo aliyoiweba Musa iliwakilisha ahadi pamoja na mamlaka aliyopewa na Mungu kufanya kazi hiyo.

Nilipata ufahamu wa kile Mungu alichokuwa akiniambia. Nilikuwa mchungaji wa kanisa hili; na nilikuwa nimepewa mamlaka ya kukabili na hali hii. Ilinibidi nichukue mamlaka na nisimame kidete ili kupata suluhisho. Tulipofika Hawaii, sikuweza kufanya mengi ila kusali tu. Sikuweza kulala usiku. Roho yangu ilikuwa imejaa misukosuko, na nilifahamu kwamba nilikuwa katika mapambano kupitia kwa Roho Mtakatifu kupata jibu nililohitaji. Hatimaye, Drenda alipata wazo ambalo aliamini lilitoka kwa Bwana. Asante Mungu kwa ajili ya mke wangu! Ametumiwa mara nyingi sana kupata mipango na mwelekeo niliohitaji katika hali nyingi. Siwezi kueleza jinsi alivyo wa thamani kwangu na jinsi ninavyompenda. Yeye huwa hakati tamaa!

Mpango wake ulikuwa rahisi lakini wa kina. Hakukuwa ishara yoyote iliyoonyesha kwamba mpango huu ungefua dafu, lakini tulianza kuufanya kazi mara moja. Mpango ulikuwa kwamba tuandae mpango wa kukopa pesa kutoka kwa benki ya mjenzi wetu, sio benki yetu. Mpango wetu ungeonyesha sisi ni akina nani na kwa nini tulihisi mkopo huo ulikuwa bora kwetu sote. Lilikuwa jambo gumu sana, maana kama nilivyosema tayari, benki zote katika mji wetu zilikuwa zimeghairi mikopo yote. Mawazo yetu yalikuwa kwamba ikiwa mjenzi wetu hangalipwa, basi kisheria angelazimika kusema kwamba amefilisika, na hivyo kuweka mikopo yoyote aliyokuwa nayo na benki yake katika hatari ya kutolipwa. Tulikuwa na uhakika huo ungekuwa mradi wa gharama kubwa kwa benki yake, ambao tulijua benki

haingetaka. Na tena, hii haikuwa benki yetu, na haikuwa na uhusiano au historia yoyote na sisi.

Kwa hivyo tuliandaa taarifa iliyoelezea idadi ya watu katika eneo letu na jinsi lilivyokuwa likikua. Tulionyesha benki historia yetu na ukuaji wetu uliotarajiwa. Pia tulishughulikia njia nyingi ambazo jengo letu lingezalisha mapato nje ya huduma za kanisa letu, kama vile jinsi mapato ya huduma yetu ya runinga yalivyokuwa yakiongezeka na mambo mengine mengi tuliyofikiri yangevutia benki. Tilitaka kuhakikishia benki kwamba tulikuwa mradi wenye hatari kubwa ambao ungeifaidi, hata katika nyakati hizo ngumu. Pia tilitaka kusema kwamba ikiwa mjenzi hangelipwa, angeweza kuingia katika hatari ya hasara kubwa ambayo tilitaka “kumsaidia” kuepuka. Tuliomba kukutana na makamu wa rais wa benki ambaye alikuwa msimamizi katika kitengo cha mikopo ya kibiashara. Tuliomba Mungu kisha tukaingia ofisini mwake, tukiwa na ujasiri kwamba huo ulikuwa mpango wa Roho Mtakatifu kwetu, na tukamjulisha ombi letu.

Cha kushangaza ni kwamba, baada ya maelezo yetu, ofisa huyo

**IKIWA UTAWAHI KUPOKEA  
KUPITIA KWA UWEZO  
MKUU WA UFALME WA  
MUNGU, UTAHITAJI  
KUJIFUNZA JINSI  
YA KUMSIKIA ROHO  
MTAKATIFU.**

alimwambia katibu wake papo hapo atayarishie kanisa hundi ya \$500,000 ili tuondoke nayo. Alisema alichokuwa akitufanyia hakikuwa cha kawaida.

Hakufanya utathmini wa mali yetu kwanza, hakutupa fomu za kujaza, bali hundi ya \$500,000 tu. Alisema zile \$500,000 zilizosalia kwamba wangefanya utathmini wa mali yetu kwanza, lakini alituhakikishia kwamba hilo lingefaulu

maana yeye ndiye aliyefanya uamuzi, na kweli hilo lilitendeka. Basi tulimlipa mjenzi wetu dola milioni moja naye akamaliza kujenga jengo letu.

Ni vigumu kukueleza jinsi mimi na Drenda tulivyohisi tulipokuwa garini kwa saa moja tukirudi nyumbani kwetu, huku tukiwa tumebeba hiyo hundi ya \$500,000 mfukoni. Tulijawa na furaha nyingi na kuwa na hisia nzuri ajabu! Hakuna neno linaloweza kueleza vyema jinsi tulivyohisi wakati huo, lakini tulikuwa na hofu kwa yale ambayo Roho Mtakatifu alikuwa amefanya. Mtu wa kwanza tuliyempigia simu alikuwa mjenzi wetu. Ningali ninasikia moyoni mwangu shangwe iliyokuwa katika sauti yake tulipomwambia habari hizo njema. “Ulifanya nini?” aliuliza. “Walikupa hundi papo hapo?” Sote wawili tulijua ilitoka kwa Mungu.

Hilo lilifanyikaje? Roho Mtakatifu! Mungu ana majibu unayohitaji,



rafiki. Ikiwa utawahi kupokea kupitia kwa uwezo mkuu wa Ufalme wa Mungu, utahitaji kujifunza jinsi ya kumsikia Roho Mtakatifu. Na hilo ndilo kitabu hiki kinahusu.

Kutembea na Roho Mtakatifu katika hali zote maishani kunasisimua zaidi kuliko filamu yoyote ya James Bond ambayo umewahi kuona! Na kama ilivyo katika filamu yenyewe, bila shaka tunajua ni nani hatimaye ataibuka mshindi, haijalishi ni nyakati ngapi za wasiwasi zilizopo.



## SURA YA 2

# UFALME

Nina hakika umesikia kuhusu kesi nyingi za kiupuzi ambazo huanzishwa mahakamani kisha zinatupwa nje. Hapa kuna mfano.

Mfungwa katika gereza kule Colorado alianzisha kesi ya madai ya zaidi ya dola bilioni 88 (ndio, *bilioni*) dhidi ya Ligi ya Kitaifa ya Soka. Madai hayo yalitokana na uamuzi uliotolewa na maafisa wakati wa mchezo wa mchujo kati ya Dallas Cowboys na Green Bay Packers. Waliamua kwamba Dez Bryant (wa Cowboys) hakukamata mpira vyema ilivyopaswa. Mfungwa hakukubaliana na hilo. Alidai kwamba maafisa wa NFL walikuwa wazembe na walikiuka wajibu wao wa kuwa waaminifu. Kwa nini mfungwa alikuwa akidai dola bilioni 88? Kwa sababu nambari ya shati ya Bw. Bryant ni 88.

Jambo la kichaa sana sivyo? Nafikiri kila mtu anaweza kuona kwamba kesi hiyo haingeenda popote. Lakini ni kitu gani huamua ikiwa kesi ni halali au la? Kwa mujibu wa mtandao wa law.com, sababu kuu mbili za kesi kukataliwa mahakamani ni kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kushughulikia kesi hiyo au suluhu yake haipatikani katika sheria. Kwa nini ninaleta masuala ya kisheria katika kitabu kinachohusu Roho Mtakatifu? Kwa sababu ukitaka kuona Roho Mtakatifu akishughulikia hali yako, unahitaji kujua wazi kile ambacho sheria inasema. Ufalme wa Mungu ni ufalme tu, na unafanya kazi ndani ya mipaka ya sheria zake. Katika vitabu vyangu viwili vya awali katika mfululizo huu, *Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kuwa Mwaminifu na Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kupumzika*, niliweka misingi ya jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi inapohusu mamlaka na sheria. Lakini ili kuelewa ninachosema kuhusu Roho Mtakatifu, itafaa tujikumbushe kuhusu kanuni hizi. Hebu tuanze na mtihani.

*Yesu akawaambia, Nabii hakosi heshima, isipokuwa katika nchi yake mwenyewe, na kwa jamaa zake, na nyumbani mwake. Wala **hakuweza** kufanya mwujiza wo wote huko, isipokuwa aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponya. Akastaajabu kwa sababu ya kutokuamini kwao.*

—Marko 6:4-6

Je, unaweza kuniambia kwa nini Yesu hakuweza kuponya watu katika kifungu hiki? Jibu la kawaida la kidini ni kwamba lazima ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kutowaponya. Mungu ndiye mjuzi wa yote, na kama angetaka kuwaponya, angefanya hivyo, sivyo? Yeye ni Mungu. Je, kuna uwezekano pia kwamba kulikuwa na watu huko ambao walihitaji kuponywa lakini hawakupokea uponyaji wao? Nafikiri hilo liko dhahiri katika maandiko pia. Ni muhimu kujua ni kwa nini Yesu hakuweza kuponya watu hapa. Tunaposoma mwisho wa hadithi hii, tunapata kwamba Yesu alisema ni kutokuamini kwao kulikowazuia kupokea uponyaji. Ili kuelewa maoni na hitimisho la Yesu kuhusu sababu watu hawakupokea, itatubidi tuelewe vyema imani ni nini na kwa nini inahitajika ili kuipa mbingu uhalali wa kuwa na mamlaka hapa duniani.

Acha niseme kwa muhtasari suala lililokuwa katika tukio hili. Kulingana na mtazamo wa Yesu, haikuwa ukosefu wa nguvu wala nia Yake. Suala lilihusu mamlaka. Kimsingi, mbingu haikuwa na mamlaka kisheria ya kutenda kazi katika hali ya watu wengi huko. Sasa, kabla hujatupa kitabu hiki chumbani huku ukisema kwamba sijui ninachozungumzia, nipe dakika chache nikueleze.

Adamu na Hawa walipowekwa duniani, walikuwa na mamlaka yote na kamili juu ya ulimwengu. Nafikiri kifungu kifuatacho kinathibitisha kauli yangu kwa udhahiri.

*Umefanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, umemtawaza juu ya kazi za mikono Yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake. Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake **hakusaza kitu kisichowekwa chini yake.***

—Waebrania 2:7-8

Tambua kwamba Biblia inasema Adamu alivikwa taji ya utukufu na heshima. Neno kuvikwa taji hapa linarejelea mahali pa mamlaka ambapo Adamu alitawala, sio kwamba alikuwa amevaa taji kwenye bustani. Lakini

tunaweza kukisia kwamba labda alikuwa na mwanga au nuru juu yake, hilo ni wazo tu. Adamu alikuwa na utukufu (upako na ukuu wa Ufalme) na heshima (mahali pa mamlaka) ya Ufalme wa Mungu. Akiwa na mambo hayo mawili, alitawala juu ya dunia, akiwa na mamlaka aliyokabidhiwa, kwa niaba ya Ufalme wa Mungu. Shetani, ambaye tayari alikuwa duniani wakati mwanadamu alipoumbwa, alimdharau mwanadamu na kutamani mamlaka aliyokuwa nayo. Maana alijua kwamba hangeweza kumpokonya taji yake ya mamlaka, kwa vile Adamu alikuwa na mamlaka kamili juu yake, ilimbidi amdanganye kwa njia moja au nyingine ili aweze kuivua (mamlaka) kwa hiari.

Hivyo, Shetani alimdanganya Hawa, naye Adamu akamfuata katika kumwasi Mungu, na hivyo wakapoteza cheo chao katika Ufalme wa Mungu. Kwa kuwa walimfuata Shetani, sasa walikuja chini ya mamlaka ya ufalme wake. Hata hiyo unaweza kuuliza, “Kwa nini Mungu alimruhusu Shetani kuingia katika bustani?” Ilimbidi. Najua unaweza kushtushwa kidogo na jibu hilo, lakini utaona kwamba ni kweli. Hebu haraka tuangalie Mwanzo 2:8-9.

*Bwana Mungu akapanda bustani upande wa mashariki wa Edeni, akamweka ndani yake huyo mtu aliyemfanya. Bwana Mungu akachipusha katika ardhi kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa; na mti wa uzima katikati ya bustani, na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.*

Tunaposoma kifungu hiki, tunaweza kujiuliza kwa nini Mungu aliweka Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya katikati ya Bustani karibu na Mti wa Uzima. Kimsingi, ili kumpa Mungu uhalali wa kuvamia eneo la Shetani, Mungu alipaswa kumpa mwanadamu uhuru wa kuchagua yule ambaye angemtumikia. Mungu hangeweza kisheria kuingilia mamlaka ya Shetani na kumweka mtu hapo. Ili kuhalalisha mambo, mwanamume huyo alipaswa kuchagua yule ambaye angejitiisha kwake. Mradi tu mwanadamu angemchagua Mungu, yaani Mti wa Uzima, angemtawala Shetani. Ndio maana Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya ulipaswa kuwekwa kando ya Mti wa Uzima.

Hapa tunahitaji kuona jambo muhimu. Mwanadamu hangewekwa duniani bila uhuru wa kuchagua. Najua, Wakristo wengi wanasema tuliumbwa na uhuru wa kuchagua ili kumwezesha Mungu kuona ni nani anayempenda. Nafikiri taarifa hiyo ni kweli kidogo lakini, kimsingi, ingekuwa kinyume cha sheria kuwa bila uwezo wa kuchagua. Ikiwa

mwanadamu hangepewa uhuru wa kuchagua hangewekwa hapa. Kuna mengi zaidi ningeweza kuzungumzia katika mjadala huu, lakini yameelezewa katika vitabu vyangu viwili vya awali.

Kwa hiyo Adamu alichagua udanganyifu wa Shetani, akapoteza Ufalme wa Mungu, na Mungu akakabilia naye katika Mwanzo 3:17-19:

*Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.*

Kimsingi, Mungu alikuwa akimwambia Adamu kwamba yeye, Adamu, aliilaani dunia. Kwa sababu ya Adamu kuwa na mamlaka kamili juu ya dunia, yeye ndiye aliyefungulia Shetani mlango wa utawala na kimsingi ndiye aliyemfukuza Mungu. Mikono ya Mungu sasa ilikuwa imefungwa, na Adamu sasa angeishi kwa uchungu wa taabu na jasho lake mwenyewe. Kuna jambo moja dogo sana ambalo Shetani alisahau kumwambia Hawa alipokuwa akimjaribu. Na hiyo ilikuwa kwamba tayari Mungu alikuwa amemhukumu Shetani, alikuwa amemfukuza kutoka mbinguni, na kutangaza makao yake ya milele yangekuwa kuzimu. Ni muhimu kuelewa hili. Watu wengi sana wanaweza kusema, “Mungu mwenye upendo angewezaje kuwatupa watu kuzimu?” Si Mungu bali ni Adamu. Kama ilivyo wazi katika kifungu kifuatacho, kuzimu haikuumbwa kwa ajili ya mwanadamu.

*“Kisha atawaambia na wale walioko mkono Wake wa kushoto, ‘Ondokeni Kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliwekewa tayari Ibilisi na malaika zake.’” (Mathayo 25:41)*

Adamu na Hawa walipokuja chini ya mamlaka ya Shetani, wao pia sasa walikuja chini ya hukumu ya Shetani. Jamii nzima ya wanadamu ilikuja chini ya utawala wa Shetani kupitia kwa Adamu. Tafakari kuhusu kufuga ng’ombe. Ikiwa mmoja wa ng’ombe wako ana ndama, ndama huyo atatiwa alama yako kama mali yako kwa sababu kundi zima ni lako. Kwa hiyo wazao wote wa Adamu walikuja chini ya mamlaka ya Shetani moja kwa moja. Ufahamu wa kawaida wa kidini, au niseme ukosefu wa ufahamu, unaosema kwamba hatima ya mtu, iwe ni mbinguni au kuzimu ni kadri ya

jinsi alivyo mzuri au mbaya, sio sahihi kabisa. Ukweli ni kwamba hukumu ya wanadamu tayari imewekwa. Wote wanaenda kuzimu. Si kwa sababu ya kosa lolote walilofanya bali kwa sababu ya kile Adamu alichofanya. Sasa, kwa sababu ya upendo wa Mungu kwa watu aliowaumba, aliweka mpango wa kuwaokoa kupitia kwa Yesu Kristo ambaye anawawezesha wanadamu kuepuka hukumu hiyo na kurudishwa katika mamlaka ya Ufalme wa Mungu.

*Naye **alituokoa** katika nguvu za giza, akatubamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo Lake (Wakolosai 1:13).*

Ni lazima ifahamike kwamba Mungu ametuandalia kisheria, njia ya kuepuka kutoka kwa mamlaka na hukumu ya Shetani. Lakini ili kufaidika na hilo, ni lazima kila mwanamume, mwanamke, na mtoto achague kujinufaisha kwa kuliitia jina la Yesu. Wakristo, nisikilizeni kwa muda mfupi. Yule mwanamke mrembo mtaani ataishia kuzimu mtu asipomwambia aliitie jina la Yesu kabla hajafa. Kutakuwa na watu wengi wazuri kuzimu. Ni uwongo wa Shetani unaowafanya watu wafikiri kwamba wanaweza kuepuka kuzimu kwa sababu ya kufanya kazi nzuri. Jina la Yesu ndilo jina pekee ambalo limepewa wanaume na wanawake kwa ajili ya wokovu na kuepuka hukumu ya Shetani. Pia nataka kufafanua kwamba Adamu alipoanguka, alikufa kiroho na alitengwa na Mungu; hata hivyo, bado kisheria alidumisha kazi yake duniani. Kwa sababu hii, Shetani hana budi kutumia watu waliovuviwa na pepo, na Mungu anapaswa kutumia watu waliojazwa na Roho ili kufanya mambo katika ufalme wa wanadamu. Kwa hivyo tunapotazama jambo hili tena, tunaelewa kwamba kwenda mbinguni au kuzimu ni suala la kisheria na si kadri ya jinsi tulivyo wema, bali ni kwa sababu ya ushindi wa kisheria ambao Yesu aliupata dhidi ya Shetani pale Msalabani. Ingawa Yesu aliifanya kuwa halali kwa mwanadamu kutoka katika mamlaka ya Shetani, tena, kila mtu lazima aliitie jina la Yesu kwa imani ili kupata ushindi.

Najua tuliacha mjadala huu aya chache zilizopita, lakini sasa hebu turudi kwenye swali tulilouliza awali, “Kwa nini Yesu hakuweza kuponya watu katika Marko 6?” Nilisema ni suala la mamlaka, na ndivyo ilivyo. Kwa kuwa Adamu alikabidhi mamlaka ya kiroho ya ufalme wa wanadamu kwa Shetani, Mungu hawezi kuja ghafula na kuingilia kati wakati wowote anapotaka maana kufanya hivyo ni kinyume na sheria. Sasa, usichanganyikiwe na nilichosema hivi punde kuhusu mmiliki wa ardhi

yenyewe. Biblia iko wazi kwamba Mungu ndiye mmiliki wa dunia na vyote vilivyomo. Lakini Mungu hana mamlaka ya kisheria juu ya ufalme wa wanadamu. Tunaweza kupata hili katika Luka 4:5–7.

*Akampanidisha juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, “Nitakupa Wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Basi, Wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa Yako.”*

Tunaweza kuona hapa kwamba Adamu alimpa Shetani mamlaka ya kisheria juu ya falme za ulimwengu. Kwa sababu hii, Mungu hawezi kufanya chochote anachotaka katika ulimwengu kuhusu wanadamu. Lakini Mungu anapopata mtu anayemwamini, na kusadikishwa kabisa na mamlaka ya mbinguni, basi Mungu anaweza kutumia mamlaka Yake kupitia kwa mtu huyo. Hiyo ndiyo njia ileile ambayo Shetani alitumia kuingia katika makao ya dunia hapo mwanzoni, kupitia yule aliyekuwa na kazi ya kisheria ya dunia, Adamu. Mungu alipompoteza mtu Wake, yaani Adamu, ilimbidi atafute njia nyingine ya kurudi duniani ili kuimarisha mpango Wake wa uokoaji, na jina la mtu huyo lilikuwa Abramamu.

*Bwana akamwambia Abramamu, “Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.”*

—Mwanzo 12:1-3

Abramu, au Ibrahimu, alikuwa mlango ambao Mungu alitumia kupata njia ya kurudi katika ulimwengu na kuleta mpango Wake wa wokovu kwa wanadamu. Mungu alifanya agano na Ibrahimu na uzao wake, na kupitia mapatano haya ya kisheria, Mungu alipata fursa ya kumleta Yesu Kristo ulimwenguni, lakini kupitia ukoo wa Abrahamu tu. Hii ndiyo sababu Yesu alipaswa kuwa mzao wa Ibrahimu na sababu Waisraeli hawakuruhusiwa kuoana na mataifa jirani. Pia ndiyo sababu kitabu cha kwanza cha Agano Jipya ni nasaba tu. Kinathibitisha kwamba Yesu, kwa kweli, ni mzao halali wa Abrahamu, hivyo kumthibitishia Shetani kwamba ilikuwa halali kwa



Yesu kuja na kulipa gharama ya dhambi.

Kwa kuwa wanadamu bado wana mamlaka ya kisheria juu ya dunia, sio mamlaka ya kiroho, ni lazima Mungu na Shetani watumie watu kufanya mambo. Kwa ufupi, wanadamu pekee ndio viumbe halali duniani. Lakini kama vile Shetani alipopata kiingilio kupitia kwa Adamu na Hawa kuamini kile alichosema, vivyo hivyo Mungu lazima atafute watu watakaoamini kile anachosema ili kujidhihirisha duniani pia. Mtu anaposhawishika kabisa moyoni mwake kuhusu yale mbingu inasema badala ya yale ambayo ufalme wa Shetani unasema, hiyo ni imani, na inaipa mbingu mamlaka ya kisheria kuleta mapenzi ya Mungu kupitia kwa mtu huyo hadi duniani dhidi ya ufalme wa Shetani. Kuna mengi zaidi ya kusema, lakini nimeangazia haya kwa undani katika vitabu vyangu viwili vya awali.

Jambo muhimu ni hili. Kwa kuwa Shetani yuko hapa duniani, daima yeye hutetea ufalme wake na kujaribu kushinda mipango ya Mungu. Kwa sababu hii, Mungu hufanya kazi kwa siri ili kutekeleza mipango na mikakati Yake ulimwenguni. Na ni katika kuwa na ufahamu wa jinsi Mungu anavyofanya kazi kwa siri ndipo utakapopata ufunguo mkubwa wa mafanikio na ushindi wako maishani. Ninauita Nguvu ya Kuwa na Mkakati!



## SURA YA 3

# MSHANGAO

Nilipigiwa simu na kijana ambaye sikuwa nimewahi kukutana naye. Alijitambulisha na kusema kwamba yeye na wavulana fulani walikuwa wamefurahia sana kitabu changu cha *Faith Hunt* na mafundisho yangu juu ya Ufalme wa Mungu. Kisha aliniomba ikiwa ningependa kwenda Montana kufundisha kikundi cha wanaume takriban 70 Ijumaa jioni na Jumamosi asubuhi. Kabla ya kumjibu, alisema, “Jumamosi asubuhi baada ya kufundisha, tungependa kukupeleka kuwinda swala maana huu ndio msimu wao.” Haikuchukua muda mrefu sana kujibu swali hilo. Alisema vijana wangu walikaribishwa kusafiri pamoja nami ikiwa walipenda. Wakati wa miezi ya joto iliyofuata, walinisaidia kupata leseni sahihi ya kuwinda. Mwanangu Tim alikuwa ameamua kusafiri pamoja nami, naye alinunua leseni yake.

Nilipata taarifa kwamba, hiki kilikuwa kikundi cha wanaume kilichoitwa *Promise Keepers*, ambacho kilivutiwa na hadithi za uwindaji nilizosimulia katika mafundisho yangu na jinsi nilivyompokea kulungu wangu kwa imani. Walitaka kusikia zaidi kuhusu jinsi nilivyopata kulungu wangu kila mara kwa dakika 30 au 40 na jinsi Mungu alivyonifunza kuwa mahususi kuhusu jinsia na ukubwa wa pembe za mnyama niliyetaka kupokea. Lazima nikubali kwamba haikuwa rahisi kuamini yale niliyoyaona yakitukia, na kama singeyaona moja kwa moja, labda ningetamani pia kujionea mwenyewe.

Hatimaye, juma la kusafiri kwenda Montana lilifika. Mimi na Tim tulisafiri na tukakutana na viongozi wachache wa kikundi cha wanaume, kikundi cha watu wazuri ajabu waliompenda Bwana kweli. Walitupeleka

kuvua samaki aina ya *trout* pamoja na kutupeleka hadi sehemu ya kufyatulia risasi ili tuone uwezo wa bunduki za kuwinda walizotuandalia. Nilipokuwa nikikulia Ohio, sikuwa na uzoefu wa kufyatua bunduki kwa umbali mrefu. Sheria zetu zilituruhusu kuwa na bunduki za kuwinda kulungu tu, na kufyatua risasi kwa umbali wa chini ya yadi 100, mara nyingi hata chini ya yadi 50. Kwa hivyo walipotuwekea umbali wa yadi 200, nilihitaji kufanya mazoezi kidogo na baada ya muda mfupi niliweza kulenga vyema na hivyo kuwa tayari kwenda kuwinda.

Jioni hiyo na asubuhi iliyofuata, nilifundisha wanaume katika jumba moja la shule ya mtaani. Wote walikuwa na hamu ya kusikia na kujifunza kuhusu Ufalme wa Mungu, hasa jinsi Mungu alikuwa amenifundisha sheria za Ufalme kupitia kwa uwindaji. Baada ya chakula cha mchana, walisema, “Sawa basi, tumwendee swala.” Sikuwa nimewahi kuwinda swala wala sikuelewa utaratibu wa kumwinda ungekuwaje. Katika uzoefu wangu wa uwindaji, mtu huwa anaenda na angalau wanaume wawili au watatu. Lakini walikuwa wamejaza magari matatu au manne ya wanaume. Nakumbuka usiku Tim alikuwa ameniuliza, “Baba, huna woga kuhusu kumpata swala? Utakuwa unawafundisha juu ya Ufalme na kutangaza kwa uhakika kwamba Ufalme unafanya kazi kila wakati, lakini vipi ikiwa hutapata swala na wote wanakutazama?” Nilimwambia kwamba sikuwa na wasiwasi kuhusu kupata swala. Mimi na Drenda tulikuwa tayari tumetoa fedha kama mbegu na tukakubaliana kuhusu swala huyo; bila shaka angekuwepo.

Tulipokuwa tukielekea kwenye eneo ambalo waliruhusiwa kuwinda, walikuwa wakieleza kwamba swala ndiye mnyama mwenye kasi zaidi katika Amerika Kaskazini na mnyama wa pili kwa kasi duniani baada ya duma. Walieleza kuwa swala ana macho makubwa na ulinzi wake mkuu ni kukimbia, hivyo anapokuona yeye huondoka mara moja. Leseni yangu iliniruhusu kuwinda swala dume, na ya Tim ilimruhusu kuwinda swala wa kike.

Mpango wetu ulikuwa ni kuendesha gari hadi sehemu iliyo juu kwenye shamba la mifugo, kisha kutembea kwa miguu huku tukitazama chini katika mabonde yasiyo na kina kirefu kuona kama tungeweza kuona wanyama. Tulipokuwa tukitembea pale juu, tuliona kundi la swala kwa mbali. Kwa sababu ya mandhari nzuri ya shamba hilo, tulihisi tungeweza kukaribia vya kutosha ili kuweza kufyatua risasi huku tukiendelea kukaa kwenye mikorongo ya chini na kukaribia. Ingetubidi kunyemelea kwenda kwa kilima cha mwisho kwa uangalifu mwingi, na kujikokota polepole

hadi kwenye kilele ili kufyatua risasi ikiwa swala bado walikuwa pale tulipofika. Walitutaka tufyatue risasi kwa umbali wa yadi 200 hadi 250 tulipofika mahali palipostahili.

Mimi na Tim tulitambaa polepole kwa matumbo yetu kwa muda ili kukaribia ukingo wa kilima kilichotazama bonde ambalo tulikuwa tumeona wanyama. Mpango ulikuwa kwamba baada ya kumuua dume wangu, naye Tim angemuua swala wake wa kike. Nilitambaa polepole hadi ukingoni na kutazama. Hakika, mpango wetu ulikuwa umefanya kazi; kundi lile dogo halikuwa limetuona. Nilinyanyua bunduki yangu na nikaona ni vigumu kuishika mikononi kwa uthabiti kwa sababu ya umbali na kupumua kwa shida kutokana na kutambaa. Lakini hatimaye, nilipoona swala kwa udhahiri, nilifyatua risasi lakini haikumpiga. Kundi la wanyama lilionekana kuchanganyikiwa nilipofyatua risasi ya pili. Sikumpiga tena. Sasa kundi lilianza kusonga huku nikifyatua risasi ya tatu kisha ya nne, wala sikumpiga. Nilipofyatua risasi ya tano, nilichosikia ni sauti ya kubofya tu. Risasi zilikuwa zimeisha.

Katika mtafaruku huo, sikuwa nimeona kwamba kundi lote lilikuwa limeondoka na lilikuwa limeenda mbali. Wanyama wote isipokuwa yule niliyemfyatulia risasi. Alisimama tuli kabisa yadi chache tu kutoka mahali aliposimama nilipofyatua mara ya kwanza. Nilimwomba Tim bunduki yake nikiwa na wasiwasi nyingi. Nilikuwa nimesimama sasa, na nikapiga risasi kwa utulivu, kisha swala dume akaanguka. Nilisisimka na kufarijika kwa wakati mmoja. Swala dume alikuwa wangu. Nilipotazama nyuma juu ya bega langu, nilishangaa kuona kikundi chote cha wanaume wakipiga kelele na kusherehekea. Baadhi yao walikuwa wakizungumza kwa simu zao za rununu, na nikasikia mmoja akisema, “Ndio, ilikuwa dakika 40 tu na swala dume alisimama tuli, kama alivyosema katika kitabu chake *Faith Hunt*.” Wote walikuwa wamekuja kuona Ufalme ukitenda kazi. Na nilikuwa nimewafundisha kwa masaa mengi, kwa hivyo walitaka kuuona ukifanya kazi. Naam, licha ya upigaji risasi wangu mbaya, bado Ufalme ulifanya kazi na kuthibitisha yale niliyoyafundisha. Tim alipata swala wake wa kike alasiri hiyo kwa kumfyatulia risasi vizuri sana swala aliyekuwa akikimbia mbio. Sote wawili tulifurahi sana! Montana ni mahali pazuri sana, na mimi na Tim tuliona Ufalme ukitenda kazi vyema sana. Kichwa cha swala huyo kimening’inizwa juu ya dawati ofisini mwangu ili kunikumbusha kuhusu Ufalme na uaminifu wa Mungu.

Kwa nini nikuambie hadithi ya uwindaji katika kitabu hiki? Kwa sababu Mungu anataka kukutumia wewe kuonyesha Ufalme Wake kwa

## **ULIMWENGU UNA NJAA YA KUONA KITU HALISI, NA MUNGU ANAPENDA KUUSHANGAZA PIA.**

marafiki, majirani, na familia yako yote. Wote wanataka kuona ukifanya kazi. Ulimwengu una njaa ya kuona kitu halisi, na Mungu anapenda kuushangaza pia. Ili kuushangaza, itabidi ujifunze jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi na jinsi Roho Mtakatifu anavyoleta majibu na fursa unazohitaji ili kushangaza kila mtu, hata wewe. Niliarifiwa baadaye kwamba wale viongozi wachache waliosimamia kikundi cha wanaume walinileta kwa kusudi hasa la kuwaonyesha Ufalme watu wengi waliokuwa wamekwama katika dini. Pia niligundua baadaye kwamba wengi walikuwa wametoa mioyo yao kwa Bwana kutokana na mafundisho yangu siku hiyo. Roho Mtakatifu ndiye aliyepanga hivyo, naye atakusaidia katika mipango yako ya mafanikio pia.

Hebu nikupe hadithi moja nyingine, lakini hii ni moja kwa moja kutoka kwa Biblia na itaonyesha tena jinsi Mungu anavyotaka kukushangaza kupitia kwa mipango na mikakati isiyo ya kawaida ambayo italeta ushahidi wa ukweli Wake na upendo kwa wale walio karibu nawe.

Ikawa makutano walipomsonga wakilisikiliza neno la Mungu, yeye alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesareti, akaona vyombo viwili vimekaa kando ya ziwa, lakini wavuvi wametoka, wanaosha nyavu zao. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akamtaka akipeleke mbali kidogo na pwani. Akaketi, akawafundisha makutano ali chomboni.

*Hata alipokwisha kunena, alimwambia Simoni, “Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki.”*

*Simoni akajibu akamwambia, “Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu.”*

*Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa katika chombo cha pili, waje kuwasaidia; wakaja, wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama.*

*Simoni Petro alipoona hayo, alianguka magotini pa Yesu,*

*akisema, “Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana!” Maana alishikwa na ushangao, yeye na wote waliokuwa pamoja naye, kwa sababu ya wingi wa samaki walioupata; na kadhalika Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, waliokuwa washirika wa Simoni. Yesu akamwambia Simoni, Usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu.*

—Luka 5:1-10

Petro, Yakobo, na Yohana walikuwa wavuvi wataalam na walikuwa katika ziwa walilolijua vyema, lakini hawakuwa wamepata chochote baada ya kuvua samaki usiku kucha. Lakini, bila shaka, hadithi haikuishia hapo. Yesu aliazima mashua ya Petro ili kuhubiri kutoka humo kisha akamwambia atupe wavu wake kwenye kilindi cha maji ili kuvua samaki. Petro, akiwa ameshtuka kidogo, alisema kwamba walikuwa wamevua samaki usiku kucha bila chochote, lakini kwa sababu Yesu alisema afanye hivyo, angetupa wavu. Petro alipofanya hivyo, Biblia inasema alipata samaki wengi sana hata wavu wake ulikuwa karibu kukatika, kwa hivyo akawaita wenzake wamsaidie. Maandiko yanaendelea kusema nyavu za wenzake zilikuwa karibu kuraruka pia na kwamba mashua zote mbili zilijaa samaki kiasi cha kuwa karibu kuzama. Biblia inasema kwamba wavuvi hao wataalam walishangazwa sana na matokeo yao siku hiyo wakaacha kuvua na kumfuata Yesu.

Hii ni moja ya hadithi ninazozipenda sana katika Biblia kwa kuwa inaonyesha wazi picha ya tofauti kati ya falme mbili, ufalme wa giza na Ufalme wa Mungu. Ufalme wa giza, ambao ni utawala wa Shetani, ni ufalme uliovunjika, ni wa umaskini, ni ufalme wa kuvua usiku kucha na kutopata chochote, na umejaa taabu chungu na jasho ili tu kupata riziki. Ninauita mfumo wa laana ya dunia ulioletwa na uasi wa Adamu, unapolinganishwa na picha tukufu ya Ufalme wa Mungu na kile unachozalisha. Chunguza kwa muda mrefu mambo haya mawili ambayo yana tofauti kubwa kabisa, na utambue kwamba Mungu amekupa mlango wa pili, yaani Ufalme.

Sasa, kila Mkristo atapaza sauti na kupiga makofi na kusema, “Naam, Ufalme wa Mungu ni mkuu; tazama samaki hao waliovuliwa!” Lakini ni wachache sana watakaouliza jinsi Yesu alivyoweza kufanya hivyo, na wengi hawajui kwamba wamepewa mamlaka na uwezo ulleule wa kufurahia kiwango kile kile cha riziki kama Petro, Yakobo, na Yohana. Jibu la kawaida kwa yale Yesu aliyoyafanya siku hiyo ni kwamba Yesu

aliweza kufanya hivyo kwa sababu Yeye ni Yesu. Lakini subiri; tayari tumeona kwamba Yesu hakuweza kuponya kila mtu katika Marko 6 kwa sababu mbingu haikuwa na mamlaka. La, kulikuwa na sheria za kiroho za Ufalme ambazo zilitenda kazi siku hiyo kwa kuleta uwezo na uzalishaji wa samaki wale.

Lakini hapa kuna suala. Wakristo wengi ninaokutana nao hawafikirii kwamba kuna uwezekano wa kufanya mambo yale yale Yesu aliyoyafanya, na kama inawezekana, hawajui jinsi alivyoyafanya. Nina msemu ninaoutumia katika mikutano yangu kwamba ikiwa huwezi kufundisha kitu, huwezi kukitumia maishani mwako. Ninamaanisha kwamba ikiwa huwezi kufafanua jinsi samaki hao walivyokamatwa, huwezi kamwe kufanya kitendo hicho tena na tena. Kwa hivyo samaki hao wengi walijitokezaje? Je, unaweza kufafanua hilo? Ikiwa unataka kupata mafanikio kama hayo, utahitaji kutafakari jinsi samaki hao walivyojitokeza. Walakini watu wengi hushtuka ninapoanza kuzungumza hivi. Lakini Yesu alisema nini?

*Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba.*

—Yohana 14:12

Yesu aliposema tunaweza kufanya kazi zile zile alizofanya kwa sababu alikuwa anaenda kwa Baba, alikuwa akimaanisha Roho Mtakatifu kuja juu yetu baada ya kufa na kufufuka Kwake. Huyu ndiye Roho Mtakatifu yule yule aliyekuja juu Yake katika Mto Yordani, aliyemwezesha kufanya matendo makuu ya Mungu tunayoyaona tunapofuata huduma Yake. Maana tunajua kwamba nguvu hii ilizuiliwa katika Marko 6 kwa sababu ya kutokuamini kwa watu, lakini haikuzuiliwa katika tukio la kuvua samaki la Luka 5, tunahitaji kujifunza sheria za Ufalme ili tuweze kuamua ni nini kinachozuia au ni nini kinachoruhusu mtiririko huru wa Roho Mtakatifu katika hali yoyote ile. Kwa hiyo, hebu tuangalie hadithi hiyo na tuone ikiwa tunaweza kugundua sheria na kanuni za Ufalme ambazo tunaweza kutambua na kujifunza kutokana nazo.

Sasa, ikiwa umesoma kitabu changu cha kwanza, unajua kilichotokea hapa kiroho wakati Petro alipompa Yesu mashua atumie. Mashua ya Petro, na hakika biashara yote yao ya uvuvi, ilibadili falme au mamlaka! Ndio, Yesu alipochukua mashua chini ya huduma Yake, mashua ya Petro



sasa ilikuwa chini ya mamlaka ya Ufalme wa Mungu. Mara tu mashua ilipokuja chini ya Ufalme wa mamlaka ya Mungu, Roho Mtakatifu alikuwa na mamlaka ya kisheria ya kumpa Yesu Neno la Maarifa kuhusu eneo lenye samaki kwenye kilindi cha maji. Uvuvi mkubwa wa samaki ulikuwa ni matokeo ya mpango na mkakati usio wa kawaida uliotolewa na Roho Mtakatifu kwa Petro kupitia kwa Yesu. Ninaita ujuzi wa siri, na kwa sababu hiyo, Petro, Yakobo, na Yohana walivua samaki wengi zaidi kuliko walivyowahi kuvua. Kwa kweli, Biblia inasema kwamba wavuvi hao wataalam walishangaa.

Ninaamini Yesu anataka uishi maisha ya kustaajibisha pia, maisha ambayo yanadhihirisha Ufalme ili watu walio karibu nawe washangazwe na wanachokiona na kumjua Yesu pia. Ninaamini kwamba mashua tupu za kidini hazitawahi kuwavuta watu kwa Mungu. Mungu anataka watu waone wema wa Ufalme Wake ili wote wapate kuona na kuamini kwamba Yeye ni mwema na yuko tayari kuwapokea wote wanaomjia. Isaya alisema haya alipotangaza unabii ufuatao, ambao ulikuwa ukirejelea kanisa.

*“Wapate [yaani sisi] kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na Bwana, ili atukuzwe” (Isaya 61:3b).*

Kwa hivyo, ni ujumbe gani ambao ninataka upate kutoka kwa hadithi ya samaki katika Luka sura ya 5? Kweli, kuna sheria nyingi za kiroho unaweza kuchagua kutoka kwa hadithi hiyo, lakini ikiwa unaweza kuondoka tu na wazo hili, litabadilisha maisha yako.

**Mtu yeyote anaweza kuvua samaki ikiwa Yesu atamwambia mahali hasa pa kutupa wavu wake!! Au acha niseme hivi: Yeyote anaweza kuvua samaki ikiwa Yesu atamwambia mahali samaki walipo na jinsi ya kuwavua!**

Watu huniambia, “Naam, hivyo ni vizuri, Gary, lakini Yesu hayupo hapa tena.” Hapana, lakini Roho Mtakatifu yule yule aliyemwambia siku ile mahali walipokuwa samaki yuko hapa leo na anaishi ndani yako ikiwa wewe ni muumini. Sikiliza kile Yesu alichowaambia wanafunzi Wake alipokuwa akijiandaa kuwaacha.

*Hayo ndiyo niliyowaambia wakati nilipokuwa nikikaa kwenu. Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atamleta kwa jina Langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia. Amani nawaachieni; amani Yangu nawapa;*

*niwapavyo Mimi siyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga.*

—Yohana 14:25-27

Amani ya Yesu ilikuwa nini? Ni Roho Mtakatifu ambaye alimwambia jinsi ya kushughulikia kila hali aliyokutana nayo. Yesu alimwita Roho Mtakatifu Mshauri. Rafiki, huyu Mshauri anaishi ndani yako na hatakuacha kamwe. Je, unamsikiliza Yeye? Itabidi ukubaliane kwamba Mungu ana jibu kwa hali yoyote unayoweza kujipata. Yesu anasema kwamba Mshauri huyu anaweza kukufundisha au kukupa ushauri kuhusu mambo yote. Kulingana na kamusi fafanuzi ya Biblia inayoitwa *Strong's*

**YESU ALIMWITA ROHO  
MTAKATIFU MSHAURI.  
RAFIKI, HUYU MSHAURI  
ANAISHI NDANI YAKO NA  
HATAKUACHA KAMWE.**

*Exhaustive Concordance* (nambari 3875), neno Mshauri katika lugha ya Kiyunani linamaanisha: mtu aliyemitwa, au kuitwa kuwa upande wa mtu mwingine, hasa yule anayemitwa ili kusaidia mwingine. Pia linamaanisha mtu anayetetea kesi ya mwingine mbele ya hakimu, mtetezi, msaidizi wa kisheria, au wakili. Katika

maana yake pana, neno hili linamaanisha msaidizi au yule anayeleta msaada, au makamu.

Sijui kukuhusu, lakini ninahitaji msaidizi kama huyo; je, nawe? Roho Mtakatifu alikuwa jibu la akina Petro wakati walikuwa wamevua usiku kucha na kutopata chochote. Na Roho Mtakatifu ndiye aliyekuwa jibu langu wakati sikujua ningepata pesa nilizohitaji ili kutoka kwa madeni. Baada ya kuiingiza familia yangu katika hali mbaya ya kifedha kwa miaka yote hiyo, nilipomgeukia Mungu kutafuta msaada, ni Roho Mtakatifu aliyenipa ndoto usiku mmoja kunionyesha niache kampuni niliyoifanyia kazi na kuanzisha kampuni yangu kuanzia chini kabisa.

Ni Roho Mtakatifu aliyeniambia kwamba kazi ya kampuni yangu mpya ilikuwa kutangaza wema wa Mungu na kuwasaidia watu kutoka kwa madeni, jambo ambalo wakati huo lilionekana kuwa la kichaa sana kwangu. Eti mimi, nisaidie watu kuondoka kwa madeni? Nilikuwa mfano halisi wa kile usichopaswa kufanya na pesa zako. Maisha yangu yalikuwa janga la kifedha. Lakini hivyo ndivyo alivyosema tufanye, kwa hiyo, kwa imani, mimi na Drenda tulianza mwendo huku tukisema kama Petro alivyosema. “Bwana, hatuelewi jambo hili, lakini kwa sababu umesema, tatalifanya.” Kwa kufuata ushauri wa Roho Mtakatifu, kampuni hiyo

mpya ilikua na kukua na kuzalisha pesa ambazo zilituwezesha mimi na Drenda kuondoka kabisa kwa madeni. Kampuni yangu bado inafanya biashara leo, na baada ya miaka 30 ingali inazalisha mamia ya maelfu ya dola kwa mwaka kama faida.

Naam, mimi na wewe si werevu kiasi hicho, bali Mungu ametupa Roho Mtakatifu ili atusaidie katika majibu tunayohitaji maishani. Lakini kama tutakavyojifunza katika kitabu hiki, tuna sehemu yetu ya kutekeleza, huku tukifanya kazi na Roho Mtakatifu ili kutimiza mapenzi ya Mungu.

Kutokana na uzoefu wangu na watu, cha kusikitisha ni kwamba, inaonekana Wakristo wengi hawana jibu kwa matatizo wanayokabiliana nayo maishani. Wao huendelea kuvua kwa uwezo wao wenyewe na, baada ya kuvua usiku kucha, daima hurudi mikono mitupu au kukaribia kupata walichokuwa wakitafuta. Hawajawahi kusikia kwamba Roho Mtakatifu yupo ili kuwasaidia katika kila hali. Ingawa Wakristo wengi husema, “Mungu atawasaidia kufanya hili au lile,” hawaelewi jinsi Yeye huwasaidia, au jinsi ya kusikia majibu wanayohitaji. Kwa hiyo wengi hawatambui kwamba ni lazima washirikiane na Mungu ili kutimiza majibu wanayohitaji na bado huendelea kusubiri Mungu afanye jambo kuhusu tatizo lao wakati jibu tayari lipo ndani yao.

Kwa mfano kuhusu pesa, watu husema kwamba Mungu atawafanikisha. Nami nasema “Vema! Mungu atawapaje hizo pesa?” Mwanzoni, wao huudhika ninapouliza swali hili kana kwamba ninapinga imani yao. Lakini mimi huendelea. “Pesa zitatokea wapi? Mungu atakuleteaje?” Ninaposhinikiza watu wanipe jibu, kwa kawaida hawajui. Ni sawa kutojua kwa muda fulani, lakini hatimaye, unahitaji kuwa na jibu. Huwezi kuvuna usichokiona. Kumbuka, Yesu alizungumza hususa alipomwambia Petro mahali samaki walikuwa, na pia jinsi ya kuwavua: “Rusha wavu wako.” Hatimaye, utahitaji kujua mahali pa kurusha wavu wako ikiwa utavua samaki.

Kwa sababu watu kwa kawaida huwa na kile ninachoita mawazo ya kisanduku cha barua, wakifikiri tu kwamba Mungu atafanya kila kitu, maisha yao ya kifedha hukaa katika hali ile ile mbaya kwa miaka 10 au 20 bila mabadiliko yoyote. Inasikitisha. Je, wataka kujua kwa nini fedha zao hukaa katika hali ileile? Ni kwa sababu hawajawahi kufundishwa jinsi ya kuvua kuptia kwa njia ya Roho Mtakatifu, yaani njia ya Ufalme. Hawajui jinsi Roho Mtakatifu anavyofanya kazi katika ulimwengu ili kuwasaidia kufanikiwa. Hawajui ni sehemu gani wanapaswa kutekeleza na Roho Mtakatifu ana sehemu gani katika kufikia mafanikio wanayohitaji sana.

Ni kama mtu ambaye niliona nilipokuwa nikila chakula cha mchana leo. Alikuwa mnene sana, na mwenye uzito wa labda pauni 375. Alikuwa amevaa kibano kwa mguu mmoja na kuegemea fimbo mbili alipotembea. Hakuwa na uwezo wa kusogea. Baada ya kula mkate ulio na jibini, aliomba kipande cha keki ya siagi ya karanga. Niliketi pale na mshtuko kumsikia akiomba keki hiyo. Sijui alikuwa akifikiria nini, lakini alikuwa amekula keki za kutosha. Hilo lilikuwa dhahiri, na lilikuwa linamuua polepole. Alijitahidi kuinuka kutoka pale mezani na taratibu na kwa uchungu akaondoka mkahawani. Hivi ndivyo ninavyowaona Wakristo wakiishi leo—wanasikia ahadi za Mungu lakini wanaendelea kula sumu kisha wanashangaa kwa nini mambo hayaendelei vyema.

## **ROHO MTAKATIFU, MUNGU MWENYEWU, ANAISHI NDANI YAKO ILI KUKUPA JIBU LOLOTE UNALOHITAJI.**

Rafiki, una jibu! Roho Mtakatifu, Mungu mwenyewe, anaishi ndani yako ili kukupa jibu lolote unalohitaji. Watu huniuliza ikiwa wanapaswa kuoa fulani au fulani, kuchukua kazi hii au ile, kuhama au kukaa mahali walipo, kuuza hisa zao au kununua hisa, nk. Roho Mtakatifu aliye ndani yako ana majibu. Tena, hili ndilo kusudi la kitabu hiki, kujifunza jinsi Roho Mtakatifu anavyotusaidia na jinsi Ufalme unavyotenda kazi inapohusu kusikia sauti ya Roho Mtakatifu.

Kwa hivyo hebu tuyapitie yale ambayo tumejifunza.

**Mtu yeyote anaweza kuvua samaki ikiwa Yesu atamwambia mahali walipo na jinsi ya kuwavua, hata wewe!**

*Karol anaeleza katika barua pepe hii jinsi maisha yake yalivyobadilishwa.*

*Mwaka jana, tarehe kama ya leo, nilikuwa nikinunua zawadi za Krismasi nikitumia kadi za mkopo, na nikapitisha kiwango kilichostahili kwa sababu sikuwa na pesa za kumnunulia binti yangu zawadi, ambaye bado aliamini kumbusu Santa Claus. Maisha yangu yalijawa wasiwasi na huzuni mara kwa mara, kwa hivyo nilimwandikia ujumbe Mchungaji Gary kwamba jambo hili la kutoa matoleo kama mbegu halifanyi kazi, kwamba hakukuwa na matokeo yoyote; naye akanijibu kwa subira sana ningoje, kwamba mavuno huchukua muda na si kawaida kuyaona haraka.*

*Sasa leo, baada ya mwaka mmoja, ninanunulia familia yangu yote zawadi kwa pesa taslimu. Ninanunua zawadi zinazogharimu dola 300 au 400, na ninawastahi watu kadhaa walionisaidia katika nyakati hizo ngumu. Mwaka jana, niliishi katika chumba cha chini katika orofa ambapo marafiki fulani waliniruhusu nikae humo kwa miezi michache. Sikuwa na pesa za chakula wala petroli. Lakini sasa ninaishi katika nyumba nzuri na ya kifahari, na jokofu langu limejaa chakula.*

*Binti yangu alizaliwa tarehe 3 Desemba, na ili kusherehekea siku ya kuzaliwa kwake tulimpeleka kwenye uwanja wa burudani unaoitwa Hershey kule Pennsylvania. Tulimwalika rafiki yake mkubwa na tukakaa sote kwenye hoteli moja pale, na tulilipia kila kitu kwa pesa taslimu. Na niliweza kumnunulia zawadi kubwa iliyogharimu zaidi ya \$400 wakati mwaka jana mtu alinidharau kwa kunipa \$30 kusherehekea siku yake ya kuzaliwa.*

*Siwezi kuandika ujumbe huu bila kulia. Ninamsbukuru sana Mchungaji Gary na mke wake, Drenda. Mwaka huu umekuwa mwaka bora zaidi maishani mwangu. Mambo ambayo Mungu amefanya katika maisha yangu ni ya ajabu. Ninaweza kujaza kitabu na hadithi zangu zote. Asante kwa kunifundisha kwamba ninaweza kuishi maisha ya mbinguni duniani.*

Barua pepe ifuatayo ni mojawapo ya hadithi za ajabu sana ambazo nimewahi kusikia kuhusu Ufalme; inatoka kwa Sharon huko Michigan.

*Mchungaji Gary, ninaandika haya kwa niaba ya mume wangu na mimi mwenyewe. Nataka kusema asante kwa sababu wewe na mke wako mmekuwa kihamasisho kikubwa kwetu. Tulisikia kukuhusu katika kipindi cha runinga cha Sid Roth yapata miaka mitatu au minne iliyopita. Tulikuwa tunapitia wakati mgumu sana. Mume wangu alifukuzwa kazi baada ya miaka 18, na tulikuwa tumetumia \$280,000 kujenga nyumba jambo hili lilipotokea. Tulikuwa tumezidiwa na madeni na mafadhaiko.*

*Tuliagiza CD zenu, na zilitupitisha wakati huo mgumu. Tulijifunza jinsi madeni yanavyoweza kulemaza na kuathiri afya*

*na maisha kwa kiasi kikubwa. Hatukuona njia nyingine. Ingawa hatukuweza kumaliza kulipia nyumba yetu mpya, tuliishi humo kwa miaka miwili kabla ya kuondoka. Hiyo ilikuwa baraka kivyake.*

*Lakini ili kufupisha hadithi ndefu, mume wangu aliweza kupata kazi yake tena ya zamani baada ya miaka minne kwa sababu alikaa katika imani na kuamini ahadi za Mungu, na wewe na mkeo mkitusaidia kupitia kwa kusikiliza CD zenu. Hakurudishiwa kazi yake ya zamani tu bali alilipwa malipo yote ya miaka hiyo minne! Hakukuwa na wakili wala chochote cha kisheria kilichohusishwa. Pia alirudishiwa muda wake wote wa likizo ya miaka hiyo minne. Walipomwajiri tena, jambo la kwanza walilotaka afanye ni kwenda likizo! Naam, tuliweza kulipia nyumba nyingine bora kuliko ile tuliyopoteza pesa taslimu kutokana na malipo ya miaka hiyo minne aliyopokea. Asante kwa yote mnayofanya.*

Kutoka kwa Andrew huko Missouri:

*Miaka miwili iliyopita mnamo Mei, nilikuwa katika hali ngumu sana. Sikufurahia kazi niliyokuwa nikifanya kwa hivyo nilikubali kazi mpya katika uuzaji wa bidhaa. Wadai wa malipo ya bili walikuwa wakipiga simu, sikuwa na pesa za kutosha kununua petroli au chakula, mwisho wa mwezi na malipo ya kodi yalikuwa yakikaribia. NILICHOKUWA NACHO, hata hivyo ni mkusanyiko wa mfululizo wa CD za Gary kuhusu Mapinduzi 2.0. Katika ibada siku moja nilihisi kutoa matoleo kama mbegu, lakini sikuwa na zaidi ya \$23 na petroli kidogo sana ya kunisaidia kumaliza wiki. Kazi haikuwa ikiendelea vyema, na nilimwambia Mungu kwamba nilitaka kutoa matoleo kama mbegu, lakini sikuwa na pesa. Nilisikia sauti kutoka ndani yangu ikisema kwamba, “Mimi (Mungu) naweza kufanya mengi zaidi na hizo \$23 kuliko wewe unavyoweza.” Mungu alinishawishi kutoa matoleo ya dola 20 na kumwamini kupata matokeo mazuri.*

*Alhamisi hiyo, nilikuwa nikisaidia mtu kushughulikia akaunti yake. Nilikuwa tayari kusaidia ingawa singepokea chochote hata kama tungemuuzia bidhaa yoyote. Mwisho wa siku, msimamizi wangu alisema alithamini usaidizi huo na akanipa*

*mauzo yote ya siku hiyo (ikiwa unashangaa, hilo kamwe halifanyiki katika mauzo ya kamisheni). Wajua nini? Jumla ya faida ambayo ningepokea ilikuwa... \$2,000!!! UREJESHO MARA 100 kabla ya wiki moja kuisha!*

*Mungu ni mwaminifu kweli, na mambo madogo huwa makubwa sana Mungu anapokuwemo. Tangu wakati huo, nimekuwa na bidii katika kutoa zaka na matoleo yangu nikiwa na mtazamo wa furaha huku nikitarajia kukua.*

*Miezi michache baada ya hili kutokea, nilibarikiwa na cheo kipya ambacho nilikuwa HASA nimetolea toleo. Nilitoka kwa kuchakachua na kuona mapato yangu yakiongezeka mara nne chini ya miaka miwili tu. Mungu asifiwe, na apewe Utukufu wote. Sifa ya Ziada: Benki haimiliki gari langu tena, na ninaendesha gari jipya kabisa LILILOLIPIWA!!!*

Huu hapa ni ushuhuda wa sifa kutoka Korea:

*Mchungaji Mpendwa Gary,*

*Nilikuwa nikiishi maisha yasiyo na kusudi, na sikuwa na uwezo wa kumudu chochote peke yangu. Nilikuwa nikitegemea msaada wa watu, na walipochoka kunisaidia, tumaini langu lilikuwa kupata pakiti ya biskuti na chupa ya soda. Hivyo tu ndivyo nilivyokuwa na uwezo wa kujinunulia na kula na watoto wangu wawili. Sikuwa na uwezo wa kulipa kodi au bili zetu. Bado ninakumbuka mara ya kwanza nilipotazama moja kwa moja ibada ya Kanisa la Faith Life kwenye mtandao. Nilimweleza mchungaji wenu wa mtandao jinsi hali yangu ilivyokuwa mbaya, naye akasema kile tu nilichobitaji ni kumwomba Mungu anionyeshe jinsi ya kuvua samaki na mahali pa kuvua kama alivyomwonyesha Petro alipohitaji kulipa kodi. Ili kufupisha hadithi ndefu, sasa ninamiliki mkahawa wa Kiafrika na kinyozi, yote hayo kwa sababu ya kusikiliza mafundisho ya Mchungaji Gary. Sifa zangu ni kwa Mungu!*

Hizi zimekuwa hadithi nzuri! Lakini labda unasema, “Vema, Gary. Hakika, mambo yalikwenda vyema kwa watu wengine lakini sio kwangu.”

Kweli, hadithi yako haijakamilika! Hebu nikuulize. Unapoketi ukisoma sura hii, je, unashikilia sana kiti chako kwa hofu kubwa kwamba unaweza kuelea? La, hufanyi hivyo. Kwa nini? Kwa sababu unaelewa sheria ya mvuto wa ardhi, na unajua kwamba inafanya kazi sawa kwa kila mtu. Naam, Ufalme wa Mungu hufanya kazi vivyo hivyo. Unaweza kujifunza sheria hizo. Unaweza kujifunza jinsi ya kusikia kuhusu mikakati ya kipekee itakayogeza maisha yako na kuyafanya yawe hadithi ya nguvu kuu za Mungu. Tayari tumethibitisha ukweli kwamba ni utambuzi na usaidizi wa Roho Mtakatifu uliofanikisha hadithi hizi. Kwa hivyo, hebu tuanze safari yetu kwa kuangalia tena baadhi ya misingi ya Roho Mtakatifu, kisha tutazungumzia kwa kina zaidi juu ya kusikia kuhusu mikakati tunayoihitaji.



## SURA YA 4

# MAMBO YA KIMSINGI: USITOKE NYUMBANI BILA HILI

Ikiwa utaishi maisha yaliyojaa mikakati na ushindi unaoongozwa na Roho Mtakatifu, kwanza, lazima uzaliwe mara ya pili, kisha ubatizwe na Roho Mtakatifu. Ndio, ni kazi mbili tofauti kabisa za Roho yule yule. Ikiwa hili ni jambo geni kwako, hamna shida. Nitakueleza mambo yote. Lakini wacha niende moja kwa moja kwenye hoja muhimu, Yesu alisema ni bora sana kuwa na Ubatizo wa Roho Mtakatifu kiasi cha kusema kwamba mtu hapaswi kuondoka nyumbani bila hilo! Tena, sikusema hivyo; Yesu ndiye aliyesema hivyo katika Matendo 1:4-5.

*Msitoke Yerusalemu, bali ngojeni ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari Zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache.*

—Matendo 1:4b-5

*Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu.*

—Matendo 1:8

Tazama Yesu alisema, “Usitoke nyumbani bila hili—ni jambo muhimu!” Kimsingi, alikuwa akisema, “Unahitaji nguvu hizi ili kufanya kazi za Mungu, kuwa shahidi wa Ufalme. Hata hivyo leo, kuna Wakristo wengi ambao bado hawajasikia au kupata Ubatizo wa Roho Mtakatifu, wengi ambao wamelelewa kanisani lakini bado hawajasikia kuhusu haja ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Au walilelewa kanisani lakini wakaambiwa kwamba ubatizo si wa nyakati hizi, na kwamba miujiza haitokei tena.

Nililelewa katika kanisa kama hilo na sikuwa nimewahi kusikia juu ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Pia huwa ninapokea barua pepe nyingi kutoka kwa watu ulimwenguni kote ambao bado hawajasikia ukweli huu wenye nguvu. Barua pepe nyingi ninazopokea zinahoji uhalali wa kipawa hiki katika nyakati za leo, ndiyo maana nimechukua muda kuandika ukweli kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Ninaamini kuwa Biblia iko wazi sana kuhusu jambo hili, na ninataka Biblia ijizungumzie yenyewe. Itajibu maswali yako yote. Lakini, kwanza, nataka kukupa usuli fulani juu ya jinsi nilivyogundua ukweli kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Nilipokuwa mdogo, nilikuwa na njaa ya Mungu (bado nina njaa, ingawa mimi ni mtu mzima), na nilikuwa mshirika katika kanisa la kimadhehebu. Tulikuwa na taratibu za kawaida za kidini kila Jumapili asubuhi. Labda ulifanya hivyo pia. Nakumbuka nyimbo kadhaa tulizoimba wakati wa kimya wa kutafakari. Kila mara tulinukuu Sala ya Bwana, kisha kasisi angetoa mahubiri, wimbo wa kumalizia, na baraka. Kila ibada ilifanywa kwa njia hiyo hiyo.

Watu pale walikuwa wa ajabu na, ndio, walimpenda Mungu hakika. Lakini sikuwa nimewahi kuona ukweli wa Injili. Sikuona maisha ya watu yakibadilika sana au watu wakiponywa kwa uwezo wa Mungu. Nafikiri ninaweza kusema kwamba sikuona onyesho kubwa la Ufalme wa Mungu.

Kwa hivyo nilikuwa kijana wa umri wa miaka 18 mwenye njaa ya Mungu, huku nikifanya biashara kwa duka la pizza la babangu. Jioni moja, kijana fulani alikuja dukani na akanialika kuhudhuria mkutano wa uamsho. Ulikuwa katika kanisa dogo la Kimethodisti katika mji wangu, na mnenaji mgeni alikuwa mwinjilisti aliyehubiri kwamba Yesu anafanya mambo yale yale aliyoyafanya katika Biblia.

Sasa, hilo lilivutia umakini wangu kwa sababu nilitaka kuona mambo kama hayo. Marafiki zangu kadhaa walikuwa washirika katika kanisa hilo, kwa hivyo niliamua kuhudhuria mkutano huo. Ingawa sikusikia kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu usiku huo, niliguswa sana na uwepo wa

Mungu katika ibada hiyo. Marafiki zangu walinitia moyo nirudi Jumapili, jambo ambalo nilifanya. Nilipenda sana kanisa hilo na nilijiunga nalo kama kanisa langu jipya.

Wiki chache baada ya mkutano huo wa uamsho, nilikutana na kikundi cha wanawake waliokuwa washirika pale na kuhudhuria mafunzo ya Biblia ya kila juma pia. Walikuwa wakizungumza juu ya kitu kinachoitwa Ubatizo wa Roho Mtakatifu, karama za Roho, na mambo mengine mbalimbali ambayo sikuwa nimewahi kuyasikia hapo awali. Nilitamani sana kusikia juu ya uwezo huo waliozungumzia kiasi kwamba nikawauliza ikiwa ningeweza kuhudhuria mafunzo yao ya Biblia ya wanawake. Mafunzo yao ya Biblia yalikuwa asubuhi, na kwa kuwa nilifanya kazi usiku katika duka la babangu, niliamua kuhudhuria.

Nilipofika huko, niligundua kwamba kwa kweli mimi tu ndiye niliyekuwa kijana pekee pale na wa miaka 18, lakini sikujali kuhusu hilo. Nilihudhuria mafundisho ya Biblia kwa sababu nilikuwa na njaa ya Mungu. Niliuliza maswali mengi *sana*.

Mabibi hao walinivumilia sana na kunipitisha katika Maandiko na kunionyesha katika Biblia yangu *mwenyewe* kwamba Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa wa nyakati za leo na kwamba nguvu za Mungu zipo leo kama ilivyokuwa wakati Yesu alipokuwa duniani. Sehemu nzuri zaidi ilikuwa wakati walisema zipo kwa waumini *wote*—ni kwa yeyote anayeomba.

Baada ya kuhudhuria mafundisho kwa majuma kadhaa, waliniambia kwamba huduma ya kitaifa iitwayo *Women's Aglow* ilikuwa ikifanya mkutano katika jiji zima. *Women's Aglow* lilikuwa wakati huo na bado ni shirika linalofundisha mengi kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wanawake hao walikuwa wakipanga kuhudhuria mkutano huo, na wakanialika niende nao. Katika nyakati hizo, watu kutoka madhehebu yote walikusanyika ili kusikia na kufurahia ubatizo huu ambao, hadi kufikia wakati huo, ulikuwa unazungumziwa hasa katika makanisa ya Kipentekoste pekee. Hizo ndizo siku ambazo watu wengi huziita Ufufuo wa Kikarismatiki, ambapo mafundisho haya ya Roho Mtakatifu yalivuka mipaka yote ya madhehebu.

Nilipohudhuria mkutano wa *Women's Aglow*, niliona kwamba mamia ya wanawake walikuwa wamekusanyika. Tena, nilikuwa kati ya wanaume wachache waliohudhuria, lakini uwepo wa Mungu katika chumba hicho ulikuwa mkuu kiasi cha kushikika.

Nilistaajabu watu walipokuwa wakizungumza kuhusu kuponywa, na nilitazama kwa mshangao wengine waliokuwa wakiombewa wakianguka chini. Hili lilikuwa jambo ambalo sikuwa nimewahi kuona hapo awali,

na nilikuwa na hamu ya kujua lakini nilichanganyikiwa kidogo nalo. Niligundua ya kwamba watu pale waliita jambo hilo kuuawa katika Roho. Ingawa katika hali ya asili lilionekana kuwa jambo la ajabu kidogo kwangu, ilionekana kwamba watu waliofanyikiwa na jambo hilo walianka wakiwa na furaha na bila shaka kuguswa na Mungu. Baadaye, niligundua kutoka kwa wanawake hao kwamba mwili wetu hauwezi kuhimili nguvu za Mungu na wakati mwingine unaweza kulemewa na kile walichokiita “upako.”

Walinionyesha mahali jambo hili lilifanyika katika huduma ya Yesu mwenyewe. Katika Yohana 18:4b-6 askari walipomjia Yesu ili wamkamate, Yesu aliuliza,

*Ni nani mnayemtafuta? Wao wakamjibu, “Ni Yesu Mnazareti.” Yesu akawaambia, “Ni mimi.” Yuda naye aliyemsaliti alikuwa amesimama pamoja nao. Basi alipowaambia, “Ni mimi,” walirudi nyuma, wakaanguka chini.*

Wakati wa ibada, wanawake waliokuwa karibu nami wote walikuwa na furaha nyingi, na nilisikia watu wengi wakinena na kumsifu Mungu kwa lugha. Haya yote yalikuwa mapya kwangu sehemu kubwa ya mkutano nilisimama tu kwa mshangao. Ingawa kulikuwa na vipengele vingi vya mkutano ambavyo vilikuwa vya ajabu kidogo kwangu, sikuweza kupinga kwamba uwepo wa ajabu na wa kushikika wa Mungu ulikuwepo. Nilifurahi sana kupata ukweli wa Injili, na nguvu ya Mungu kweli ilikuwa ingali inatenda kazi duniani, kama katika Biblia.

Siku hiyo, mnenaji alimwomba yeyote aliyetaka kupokea kipawa hiki cha Roho Mtakatifu aje mbele kwa maombi mwishoni mwa mkutano. Kwa hiyo nilikwenda mbele ili wanawake wasali pamoja nami. Walipokuwa wakiomba, nilijikuta nikifadhaika huku uwepo wa Mungu ukizidi kuongezeka. Nilipojalisimisha kwa uwepo Wake, nilishangaa kujisikia nikianza kuomba katika Roho Mtakatifu, na kusema maneno ambayo sikuelewa. Niliomba kwa lugha kwa muda mrefu sana usiku huo. Nilivutiwa sana na tukio hilo, nilitaka kumwambia kila mtu niliyekutana naye kuhusu kile kilichonipata! Lakini niliposhiriki na marafiki zangu kanisani yale niliojionea, hawakusisimka sana. Walisema kwamba ndimi ni za shetani, au kwamba ni kitu kisicho cha leo. Walinionya nijiepushe na Wakristo hao wainjilisti wanaoonyesha ari ya kidini kwa msisimko mkali!

Katika nyakati hizo, makanisa hayakuwa wazi kwa karama za Roho, na mafundisho yaliyoenea yalikuwa kwamba miujiza ilikuwa imepita pamoja

na mitume. Lakini sasa nilielewa kwamba nguvu za Mungu hazikuwa zimepita hata kidogo!

Kabla ya mkutano huo wa *Women's Aglow* kufanyika, nilikuwa nimewekwa kusimamia vijana katika kanisa hilo dogo la Kimethodisti. Kwa kweli sikuhitajika kufanya mengi isipokuwa tu kuwa na mkutano wa vijana kila Jumapili usiku katika chumba kilichokuwa chini ya kanisa. Kwa kawaida tulicheza michezo, tulipata viburudisho, kisha kuwa na mafundisho mafupi ya Biblia. Nilikuwa kijana tu, lakini niliona kwamba nilikuwa na bidii kwa ajili ya mambo ya Mungu na nilikuwa tayari kusaaidia katika hilo.

Kwa kawaida kulikuwa na vijana wapatao 15 katika kikundi, na baada ya yale niliyoyaona katika mkutano wa *Women's Aglow*, nilitaka kuwaambia kuhusu Ubatizo huu wa Roho Mtakatifu niliokuwa nimepokea. Niligundua kwamba, kama mimi, wengi wao hawakuwa wamesikia kuhusu jambo hili, na nilijua kwamba hawangesikia kulihusu wakati wa ibada ya Jumapili asubuhi katika kanisa hilo.

Kabla sijakuambia kilichofuata, nafikiri ninafaa kukupa sasisho la haraka kuhusu mtazamo wangu wa wakati huo. Sikupata kibali cha mchungaji kuzungumza na vijana kuhusu hili. (Sasa ninaona kwamba ningefanya hivyo.) Pia sikuwa nimemwambia kuhusu kile nilichokuwa nimepokea.

Sikuwa ninajaribu kuasi kanisa langu na mchungaji wangu, wala kujaribu kufanya mambo kichinichini. Nilikuwa na msisimko mwingi tu. Wakati huo, kwa kweli sikuelewa utata juu ya mada hii, na hakika sikufikiri mchungaji hangetaka hilo.

Jumapili usiku baada ya kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu, nilipanga kuwaeleza vijana juu ya kile nilichopokea, na kuwaonyesha baadhi ya Maandiko yaliyozungumzia jambo hilo katika kitabu cha Matendo. Tulikuwa tumeketi sakafuni kwa mviringo katika kile chumba chetu chini ya kanisa niliposhiriki nao na kuwaonyesha baadhi ya Maandiko kuthibitisha tukio hilo.

Jioni hii hasa, kasisi alikuja kwa mkutano wetu na alikuwa ameketi upande wangu wa kushoto nilipokuwa nikishiriki. Sikufikiria chochote kuhusu kuwepo kwake pale. Hata hivyo, nilifikiri yeye kama mchungaji wangu, tayari alijua kila kitu ambacho ningeshiriki.

Kwa hiyo, nilishiriki nao kuhusu mkutano niliokuwa nimehudhuria na mambo niliyoyaona. Sikuzungumzia kwa kina kuhusu kunena kwa lugha. Badala yake, nilielekeza mawazo yangu kwenye Matendo 1:9 ambapo inasema kwamba tutapokea *nguvu* wakati Roho Mtakatifu atakapokuja juu yetu kuwa shahidi wa Mungu. Mwishoni mwa mkutano, sikujua jinsi ya

kumalizia somo langu, kwa hiyo niliwaomba vijana wainue mikono yao ikiwa walitaka kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Sikujua la kufanya wakati huo. Namaanisha, sikuwa nimewahi kuona mtu yeyote akimhudumia mtu kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu isipokuwa kile nilichokuwa nimeona katika mkutano wa *Women's Aglow*. Nafikiri huenda nilijua Maandiko mawili au matatu tu yaliyorejelea jambo hilo wakati huo.

Kwa hiyo, nilisema, “Kama ungependa kupokea karama hii ya bure ya Roho Mtakatifu, inua mkono wako, na tuinamishe vichwa vyetu tuombe.” Hayo ndiyo tu niliyoyasema. Sikuwagusa wala kuwafundisha jinsi ya kupokea Roho Mtakatifu. Tuliinamisha vichwa vyetu na tukaomba. Bila shaka, tulifunga macho yetu kuomba kama Wakristo wote “wema” wa madhehebu walivyofundishwa.

Nilipokuwa nimeketi pale baada ya kusema “Amina,” nilianza kusikia mtafaruku fulani miongoni mwa vijana. Nilifungua macho yangu na kuona kwamba baadhi yao walikuwa wakilia, wengine walikuwa wakitetemeka, na vijana saba walikuwa wameanza kunena kwa lugha. Walipoanza kunena kwa lugha, niliona mwanga usio wa kawaida kwenye nyuso zao. Walikuwa wameng’aa kama taa! Nilishtuka!

Mchungaji wangu, ambaye alikuwa hajasema lolote hadi wakati huo, alinigusa begani haraka na kuniuliza ikiwa angeweza kuzungumza nami mara moja. Tuliingia kwenye chumba kilichofuata, kisha akanitazama machoni na kusema, “Haya ni mambo ya kishetani. Huwezi kuendelea kuwa kiongozi wa vijana hapa. Hatutakuwa na mambo haya hapa.”

Nikawaza, *Unawezaje kusema ni ya kishetani? Waangalie vijana hawa! Wanang’aa!* Upako juu yao ulikuwa dhahiri kabisa. Kwa kweli, sikujua neno *upako* lilikuwa na maana gani wakati huo. Nilijua tu kwamba walikuwa wanang’aa, na sikuwa nimewagusa au kuwaambia cha kufanya. Nilikatishwa tamaa na kuchanganyikiwa sana mchungaji wangu aliponikaripia hivyo, wala sikujua la kufanya.

Kabla ya mkutano huo wa Women’s Aglow kufanyika, nilikuwa nimewekwa kusimamia vijana katika kanisa hilo dogo la Kimethodisti. Kwa kweli sikuhitajika kufanya mengi isipokuwa tu kuwa na mkutano wa vijana kila Jumapili usiku katika chumba kilichokuwa chini ya kanisa. Kwa kawaida tulicheza michezo, tulipata viburudisho, kisha kuwa na mafundisho mafupi ya Biblia. Nilikuwa kijana tu, lakini niliona kwamba nilikuwa na bidii kwa ajili ya mambo ya Mungu na nilikuwa tayari kusaidia katika hilo.

Kwa kawaida kulikuwa na vijana wapatao 15 katika kikundi, na baada

ya yale niliyoyaona katika mkutano wa Women's Aglow, nilitaka kuwaambia kuhusu Ubatizo huu wa Roho Mtakatifu niliokuwa nimepokea. Niligundua kwamba, kama mimi, wengi wao hawakuwa wamesikia kuhusu jambo hili, na nilijua kwamba hawangesikia kulihusu wakati wa ibada ya Jumapili asubuhi katika kanisa hilo.

Kabla sijakuambia kilichofuata, nafikiri ninafaa kukupa sasisho la haraka kuhusu mtazamo wangu wa wakati huo. Sikupata kibali cha mchungaji kuzungumza na vijana kuhusu hili. (Sasa ninaona kwamba ningefanya hivyo.) Pia sikuwa nimemwambia kuhusu kile nilichokuwa nimepokea.

Sikuwa ninajaribu kuasi kanisa langu na mchungaji wangu, wala kujaribu kufanya mambo kichinichini. Nilikuwa na msisimko mwingi tu. Wakati huo, kwa kweli sikuelewa utata juu ya mada hii, na hakika sikufikiri mchungaji hangetaka hilo.

Jumapili usiku baada ya kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu, nilipanga kuwaeleza vijana juu ya kile nilichopokea, na kuwaonyesha baadhi ya Maandiko yaliyozungumzia jambo hilo katika kitabu cha Matendo. Tulikuwa tumeketi sakafuni kwa mviringo katika kile chumba chetu chini ya kanisa niliposhiriki nao na kuwaonyesha baadhi ya Maandiko kuthibitisha tukio hilo.

Jioni hii hasa, kasisi alikuja kwa mkutano wetu na alikuwa ameketi upande wangu wa kushoto nilipokuwa nikishiriki. Sikufikiria chochote kuhusu kuwepo kwake pale. Hata hivyo, nilifikiri yeye kama mchungaji wangu, tayari alijua kila kitu ambacho ningeshiriki.

Kwa hiyo, nilishiriki nao kuhusu mkutano niliokuwa nimehudhuria na mambo niliyoyaona. Sikuzungumzia kwa kina kuhusu kunena kwa lugha. Badala yake, nilielekeza mawazo yangu kwenye Matendo 1:9 ambapo inasema kwamba tutapokea nguvu wakati Roho Mtakatifu atakapokuja juu yetu kuwa shahidi wa Mungu. Mwishoni mwa mkutano, sikujua jinsi ya kumalizia somo langu, kwa hiyo niliwaomba vijana wainue mikono yao ikiwa walitaka kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Sikujua la kufanya wakati huo. Namaanisha, sikuwa nimewahi kuona mtu yeyote akimhudumia mtu kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu isipokuwa kile nilichokuwa nimeona katika mkutano wa Women's Aglow. Nafikiri huenda nilijua Maandiko mawili au matatu tu yaliyorejelea jambo hilo wakati huo.

Kwa hiyo, nilisema, "Kama ungependa kupokea karama hii ya bure ya Roho Mtakatifu, inua mkono wako, na tuinamisha vichwa vyetu tuombe."

Hayo ndiyo tu niliyoyasema. Sikuwagusa wala kuwafundisha jinsi ya kupokea Roho Mtakatifu. Tuliinamisha vichwa vyetu na tukaomba. Bila shaka, tulifunga macho yetu kuomba kama Wakristo wote “wema” wa madhehebu walivyofundishwa.

Nilipokuwa nimeketi pale baada ya kusema “Amina,” nilianza kusikia mtafaruku fulani miongoni mwa vijana. Nilifungua macho yangu na kuona kwamba baadhi yao walikuwa wakilia, wengine walikuwa wakitetemeka, na vijana saba walikuwa wameanza kunena kwa lugha. Walipoanza kunena kwa lugha, niliona mwanga usio wa kawaida kwenye nyuso zao. Walikuwa wameng’aa kama taa! Nilishtuka!

Mchungaji wangu, ambaye alikuwa hajasema lolote hadi wakati huo, alinigusa begani haraka na kuniuliza ikiwa angeweza kuzungumza nami mara moja. Tuliingia kwenye chumba kilichofuata, kisha akanitazama machoni na kusema, “Haya ni mambo ya kishetani. Huwezi kuendelea kuwa kiongozi wa vijana hapa. Hatutakuwa na mambo haya hapa.”

Nikawaza, Unawezaje kusema ni ya kishetani? Waangalie vijana hawa! Wanang’aa! Upako juu yao ulikuwa dhahiri kabisa. Kwa kweli, sikujua neno upako lilikuwa na maana gani wakati huo. Nilijua tu kwamba walikuwa wanang’aa, na sikuwa nimewagusa au kuwaambia cha kufanya. Nilikatishwa tamaa na kuchanganyikiwa sana mchungaji wangu aliponikaripia hivyo, wala sikujua la kufanya.

Jumapili iliyofuata, nilirudi kanisani, lakini badala ya kuketi karibu na madhabahu kama kawaida, niliketiki nyuma. Nilijua nilikuwa mahali pabaya machoni pa mchungaji wangu kwa sababu ya ule mkutano wa vijana, na niliwaza ni bora nitulie kwa muda mfupi huku nikiwaza cha kufanya.

Wakati wa ibada, kulikuwa na ule muda wa kawaida wa kukaa kimya ili kutafakari. Huu ulikuwa wakati wa heshima na utulivu sana wa maombi katika kanisa langu. Kichwa cha kila mtu kiliinamishwa, na hapakuwa na sauti yoyote kanisani. Ungesikia hata pini ilipoanguka. Ulikuwa wakati huu ambapo nilihisi mtu akigonga bega langu. Nilikuwa nimeketi mwishoni mwa kiti, na kumbe kulikuwa na mtu ambaye alikuwa amesimama kwenye njia na kunigonga begani mwangu.

Mwanzoni, nilishtuka na kufikiria kwamba ni nani alikuwa amesimama na kutembea wakati wa utulivu sana wa maombi. Nilipotazama juu, nilishangaa kuona mmoja wa wale vijana waliokuwa katika mkutano wetu wa vijana wiki moja awali. Nilifahamu pia kwamba alikuwa mmoja wa wale saba waliokuwa wamepokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu usiku ule. Alinitazama na kusema, “Twende!” Nikawaza, *Twende? Twende wapi?*



Ajabu ni kwamba, alikuwa na mng'ao ule ule aliokuwa nao usiku ule alipopokea Roho Mtakatifu, na nilijua Mungu alikuwa akifanya jambo fulani. Lakini sikuwa na uhakika huu ulikuwa wakati au mahali pa kufanya chochote kwa kuwa tayari nilikuwa shidani na mchungaji. Pia nilijua kwamba hatungeweza kufanya chochote tulichotaka katika ibada ya Jumapili asubuhi. Hapo ndipo alisema, “Ninaenda kumwomba mamangu.”

Sasa, nilianza kuelewa alichokuwa akimaanisha. Nilimfahamu mamake. Alikuwa mwanamke mdogo, mwembamba na alikuwa mgonjwa kwa muda mrefu sana. Mifupa mitano ya uti wa mgongo wake ilikuwa na shida na tumaini pekee la daktari lilikuwa kuiunganisha mifupa hiyo pamoja. Upasuaji huu ulikuwa mgumu sana, na rafiki yangu alikuwa mtoto wake wa pekee. Bila shaka alikuwa na wasiwasi nyingi kuhusu mamake.

Baada ya kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu, alihisi hakika kwamba Yesu angemponya mamake. Kwa hiyo aliposema, “Twende,” nilifikiri angeenda kwa mamake na kumwekelea mikono na kumwomba kwa utulivu. Lakini hakufanya hivyo. Alimwendea mamake, akamnyanyua pale pale kwenye kiti na kumpeleka mbele ya kanisa.

Alimketisha chini na kuanza kumuomba kwa sauti ya juu kama awezavyo kwa ndimi. Sasa kumbuka, haya yote yalifanyika wakati wa kukaa “kimya” na kutafakari, ambao sasa haukuwa kimya tena. Nilishtuka! Kisha akanigeukia na kusema, “Sasa wewe toa maelezo ya kile kinachoendelea hapa.”

Sasa nilipata ufahamu wa sababu alitaka niende pamoja naye. Aliwaza kwamba kwa sababu mimi ndiye niliyemwambia kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu, basi ingefaa niwaambie washirika maana yake baada yao kumsikia akiomwomba mamake kwa ndimi.

Kwa hiyo nilisimama mbele ya mkusanyiko wa washirika nikiwa mnenaji wake, naye alikuwa akimwomba mamake kwa ndimi. Kwa kweli sikujua la kusema, hasa kwa vile mchungaji wetu alikuwa ameketi pale akinikazia macho. Niliwaambia washirika kwamba mamake alikuwa mgonjwa na kwamba alikuwa akimwomba kwa ndimi, kama Biblia inavyosema. Lakini wajua nini? Aliponywa papo hapo kanisani asubuhi hiyo!

Hiyo ilikuwa imani ya mwana ambaye kwa kweli hakujali kile mtu mwingine alichofikiria kuhusu maombi yake. Alikuwa na hakika kwamba Roho Mtakatifu alikuwa hai na angeweza kumponya mamake.

Ingawa aliponywa papo hapo, kanisa halikupokea hilo. Wengi wao walinjia baadaye na kusema, “Naam, hatukujali kwamba alimwomba mamake, lakini ndimi hizo, hatuwezani na mambo hayo ya ndimi.”

Ninaweza kukuhakikishia kwamba shetani anachukia jambo la kunena katika ndimi, lakini ninatumai nitakusaidia kuelewa kwa nini anachukia ndimi kabla ya mwisho wa kitabu hiki.

Labda ulilelewa katika kanisa ambapo ndimi na karama za Roho hazikutumiwa. Au labda ulipokuwa ukikua ulifundishwa kwamba ndimi sio za leo au zilikwisha zamani. Maswali haya si magumu kujibu. Biblia iko wazi sana kuhusu jambo hili. Kwa hiyo hebu tuliangalie Neno vyema ili tupate ukweli juu ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hebu turejee kwenye mistari tuliyosoma mwanzoni mwa sura hii.

*Msitoke Yerusalemu, bali ngojeni ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari Zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache.*

—Matendo 1:4b-5

Kuna mambo kadhaa muhimu tunayoweza kuona katika aya hii:

**HAYO MANENO  
NIWAAMBIAYO MIMI  
SIYASEMI KWA SHAURI  
LANGU; LAKINI BABA  
AKAAYE NDANI YANGU  
HUZIFANYA KAZI ZAKE.  
—YOHANA 14:10B**

1. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tofauti na kubatizwa kwa maji.

2. Yesu alisema ni muhimu sana. Aliweka wazi kwamba hakika huwezi kufanya chochote bila hilo.

Kumbuka, Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi waende kuhubiri Injili kwa kila taifa, lakini hawangeweza kuonyesha au kuthibitisha Ufalme wa mbinguni bila ubatizo huu. Kwa hiyo akasema, “Subirini mpaka mpate uweza huu.”

*Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*

—Matendo 1:8

Nguvu! Neno hili nguvu katika lugha ya Kiyunani ni dunamis na ndipo neno baruti linapotoka. Kwa hiyo tunaona kwamba nguvu ya Mungu

huja juu yetu ili kutuwezesho kufanya kazi Zake. Mwanzoni katika huduma Yake, Yesu alikuwa ametaja kwamba nguvu, au ule upako aliokuwa nao, ulitoka kwa Baba Yake.

*“Hayo maneno niwaambiayo Mimi siyasemi kwa shauri Langu; lakini Baba akaaye ndani Yangu huzifanya kazi Zake (Yohana 14:10b).”*

*“Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe... (Yohana 5:19).”*

Wajua, Yesu Mwenyewe alihitaji kutiwa nguvu na Roho wa Mungu. Neno upako linamaanisha “kutumika kwa.” Yesu alipokea upako huo kwenye Mto Yordani kutoka kwa Baba Yake wakati Roho Mtakatifu alipokuja juu Yake katika umbo la njiwa.

Ni baada tu ya Yesu kupokea upako huo ndipo alipoweza kufanya kazi za Ufalme. Ikiwa Yesu aliuhitaji, sisi pia tunauhitaji! Nguvu hiyo itashuhudia (au kuwa shahidi) kwa kuonyesha kwamba Mungu yuko halisi kwa wale wasiomjua.

Biblia pia inasema kwamba mtapokea nguvu wakati Roho Mtakatifu **ATAKAPOKUJA JUU YENU**, sio atakapokuja ndani yenu kama wakati mlipozaliwa mara ya pili.

Wengi huchanganyikiwa tunapozungumza kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu, wakifikiri kwamba tayari wamempokea Roho Mtakatifu walipomkubali Kristo. Na ukweli ni kwamba walimpokea Roho Mtakatifu walipompokea Kristo. Roho Mtakatifu alihuisha roho zao kwa Mungu na kuzifanya ziwe kitu kimoja na Mungu.

Tunahuishwa kwa Mungu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu ndani yetu tunapozaliwa mara ya pili. Lakini tazama kwamba Maandiko haya yanasema wakati Roho Mtakatifu anapokuja juu yako. Hili ni jambo muhimu ambalo tutalishughulikia baadaye katika kitabu hiki: kuzaliwa mara ya pili na kutiwa mafuta au kubatizwa na Roho Mtakatifu ni matukio mawili tofauti. Tunaweza kupata ufahamu mzuri zaidi kuhusu hili katika Yohana 20:21-22.

*Basi Yesu akawaambia tena, “Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma Mimi, Mimi nami nawapeleka ninyi.” Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia, akawaambia, “Pokeeni Roho Mtakatifu.”*

Hapa tunamwona Yesu baada ya kufufuka akiwasalimia wanafunzi Wake na kuwapulizia na kusema wampokee Roho Mtakatifu. Huu ndio wakati walipozaliwa mara ya pili na roho zao kuhuishwa kwa Mungu. Hata hivyo Yesu aliwaambia wangojee Ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambao ungekuja juu yao siku nyingine baadaye.

Ikiwa walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu kikamilifu Yesu alipowapulizia, kwa nini aliwaambia wangoje Yerusalemu hadi wampokee Roho Mtakatifu ambaye aliahidiwa kuja juu yao? Tena, haya ni matukio mawili tofauti na kazi mbili tofauti, bali Roho yule yule. Pia, kama nilivyosema, nataka kutaja kwamba Yesu alipaswa kubatizwa na Roho Mtakatifu ili aingie na kuwa na ufanisi katika huduma Yake. Kabla ya Yesu kubatizwa na Roho Mtakatifu, hakuna mahali tunaona akifanya muujiza hata mmoja. Je, Yesu alizidisha mkate mezani alipokuwa akikua? Je! Alifanya miujiza alipokuwa mtoto mchanga? Je, alizidisha chakula Chake alipokuwa mtoto kilipoisha kwa sababu bado alikuwa na njaa? La! Hakufanya hivyo. Kwa nini hakufanya hivyo? Jibu rahisi na la ukweli ni: Hangeweza.

Haikuwa mpaka *baada* ya kupokea Roho Mtakatifu katika Mto Yordani ambapo alianza kufanya miujiza. Wajua, Yesu alikuja kama mwanadamu. Hakuja kama Mwana wa Mungu katika nguvu na utukufu Wake. Alikuwa na viziwi kama mwanadamu yeyote yule. Hakuwa na uwezo wa kuponya au kufanya miujiza yoyote, kama ilivyo kwako na mimi.

Lakini, tofauti na sisi, roho ya Yesu ilikuwa hai kwa Mungu alipozaliwa kama mtoto. Roho Yake ilikuwa hai daima kwa Mungu; Yeye hakuhitaji kuzaliwa mara ya pili kama sisi. Hata hivyo, ingawa roho Yake ilikuwa hai kwa Mungu kama Mwana, bado alihitaji kubatizwa na Roho Mtakatifu kabla ya kuanza huduma Yake, kama ilivyo kwetu sisi.

*Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu Yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa naye.*

—Mathayo 3:16-17

Kumbuka, tunamuona Yesu kama Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana, lakini hakuhudumu na cheo hicho. Miujiza ilianza baada ya Roho Mtakatifu kuja juu Yake katika Mto Yordani.

Huduma yako (kwa sababu kila mwamini ameitwa kufanya kazi za

Yesu) haiwezi kuanza hadi utakapobatikwa na Roho Mtakatifu—unahitaji nguvu za Roho Mtakatifu ili kutekeleza mambo. Na unahitaji uwezo wa kuomba katika Roho ili kufahamu jinsi ya kuyafanya, kama tutakavyojadili baadaye.

Bila shaka, unaweza kuwaambia wengine jinsi ulivyojaliwa mara ya pili kama Biblia inavyosema. Wakristo wengi ambao hawajabatizwa na Roho Mtakatifu wana ujuzi wa kushiriki Habari Njema ya Injili, lakini hawana uwezo wa kudhihirisha Ufalme jinsi Yesu alivyofanya. Hii inasababisha udhaifu mwingi katika mahubiri.

Yesu alipowakabili Mafarisayo kuhusu kutokuamini kwao, alirejelea miujiza aliyokuwa akifanya. Alisema,

*“Mnisadiki ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani Yangu; la! Hamsadiki hivyo, sadikini kwa sababu ya kazi zenyewe.”* (Yohana 14:11)

Kimsingi Yesu alikuwa akisema kwamba udhihirisho huu wa Ufalme ulikomesha mabishano yote; tosha. Sasa, bila shaka, kila muumini ana haki kamili za kisheria kudai kila kitu ambacho Yesu alilipia, ikiwa ni pamoja na uponyaji. Kila muumini anaweza kupokea kila ahadi ya Mungu kwa imani (kukubaliana na mbingu), na hahitaji Ubatizo wa Roho Mtakatifu ili kupokea kutoka kwa Mungu.

Lakini ili nguvu hiyo itiririke kutoka kwako kwenda kwa wengine, na ili wewe uweze kutumia karama za Roho na kufurahia faida ya kufahamu siri za mbinguni kwa njia ya kuomba kwa ndimi, lazima uwe na nguvu ya upako huo! Ninatambua kwamba huenda usielewe ninachomaanisha ninaposema kuomba kwa ndimi. Hilo lisikuogopeshe; nitaeleza kulihusu kikamilifu baadaye.

Binti yangu Amy ndiye kiongozi wa ibada ya sifa katika kanisa letu, Faith Life Church, hapa New Albany, Ohio. Kwa miaka michache, alikuwa na hali ambayo ilitushangaza sisi sote—tumbo lake lilikuwa likikua polepole na ukubwa wake ulikuwa umeanza kujitokeza wazi. Ingawa tulikuwa tumeenda kwa madaktari wengi, hakuna hata mmoja aliyejua kwa nini hilo lilikuwa likitendeka. Wote walisema ni jinsi mwili wake ulivyoubwa.

Jambo hili liliendelea hadi ikaonekana kana kwamba alikuwa mjamzito miezi sita. Wakati huo, Amy alipigwa X-ray, kisha tukaona waziwazi katika X-ray uvimbe mkubwa uliokuwa tumboni mwake. Amy alijua hatua iliyohitajika ingekuwa ya kimatibabu, na hiyo ingekuwa upasuaji. Maana

hakuwa ameolewa kwa muda mrefu, Amy alifahamu kwamba upasuaji wa aina yoyote ungemzuia au kumfanya asiweze kupata watoto. Kwa hivyo hakutaka hilo. Maisha yake yote alikuwa na ndoto ya kuwa mama. Tuliona katika X-ray kwamba ukubwa wa uvimbe huo ulikuwa umefinya viungo vyake, na hilo lilisababisha matatizo tumboni mwake alipokula chakula na pia matatizo makubwa ya figo. Aliamua kuchukua kwa uzito Neno la Mungu na kutenga wakati kukaza fikra zake kwa yale ambayo Biblia inafundisha kuhusu uponyaji. Katika majuma hayo hayo, nilikuwa nikifundisha juu ya uponyaji katika kanisa letu. Mwishoni mwa mfululizo wa mafundisho hayo, Amy aliwomba wazee wa kanisa wamwekee mikono na kumwomba kuhusu uponyaji wake kulingana na Yakobo 5:14–15, jambo ambalo tulifanya.

*Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwoko a mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa.*

—Yakobo 5:14-15

Kwa kusadiki Neno la Mungu, Amy *alidai* uponyaji wake tulipomwekelea mikono. Ingawa hakukuwa na udhihirisho wa kimwili wa uponyaji wake wakati tulipomwomba, alikuwa na hakika kwamba ameponywa.

Baada ya majuma mawili, alikwenda kulala bila ushahidi wa kimwili kwamba alikuwa amepona, lakini alipoamka asubuhi alipigwa na mshangao. Alikuwa amepungua pauni 13 na inchi 9 kutoka kiunoni mwake usiku kucha alipokuwa amelala. Uti wa mgongo uliopotoka na wenye mafundo sasa ulikuwa wa kawaida kabisa. Alipona papo hapo!



AWALI

BAADA YA UPONYAJI

Picha hizi zinaonyesha uponyaji wa ajabu. Picha ya kushoto ni jinsi Amy alivyokuwa wakati alipokuwa akienda kulala. Picha ya kulia ni jinsi alivyokuwa wakati alipoamka.



Unaweza kuona X-ray ya mgongo wake upande wa kushoto kabla ya uponyaji na X-ray iliyopigwa wiki moja baada ya uponyaji upande wa kulia. Angalia mabadiliko makubwa yaliyo katika uti wa mgongo!

Wakati huo Amy alikuwa na yungali kiongozi wetu wa ibada ya sifa katika Kanisa la Faith Life. Unaweza kufikiria ni jambo gani lililotukia Jumapili iliyofuata alipoenda kanisani—watu walimkodolea macho! Watu walisimama katika ukumbi wa kanisa, na kusema huku wakiwa na mshtuko, “Ni kitu gani kilichokutendekeza? Umepata mwili mpya?” Kanisa zima lilipigwa na mshtuko Jumapili hiyo Amy alipokuwa akiongoza ibada, na udhihirisho huu wa Ufalme wa Mungu ulileta wengi kwa Mungu na wengi waliponywa.

Itabidi ukubali kwamba watu wanahitaji kuona Ufalme wa Mungu ukifanya kazi. Katika Matendo 1:8, tunaona kwamba upako, Ubatizo huu wa Roho Mtakatifu ni jambo muhimu.

*Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashabidi Wangu katika Yerusalemu,*

*na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*

—Matendo 1:8

Na kulingana na Yesu, jambo hili ni muhimu kwa ajili ya udhahirisho wa Ufalme wa Mungu.

*Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watahika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*

—Marko 16:17-18

Kushika nyoka na kunywa kitu cha kufisha vinahusu ufalme wa Shetani na vinarejelea woga moja kwa moja. Ufalme wa Shetani umeshindwa. Yesu hasemi kwamba kwa kweli tuwachukue nyoka hatari au kunywa sumu, lakini anatumia msemu huu kama mfano wa uwezo ambao tumepewa juu ya adui. Tunapaswa kuchukua mamlaka na nguvu za Mungu katika milki ya Shetani na kuwaweka watu huru!

Tazama kwamba Yesu anasema **“ishara hizi”** zitafuatana na wale wanaoamini. Watu wanapoona ishara hizi (maonyesho) za Ufalme, watauliza jinsi zilivyotokea. *Ishara* inaashiria jambo. Ishara yenyewe sio jibu, lakini inaelekeza kwa Yesu aliye hai!

Ishara hizi huzuia mabishano yote kuhusu ikiwa Yesu ni Bwana au la—YEYE YUPO! Na watu watakapoona kwamba yupo, watatubu na kumwendea Mungu. Ndiyo maana wewe na mimi tunahitaji Ubatizo wa Roho Mtakatifu, na hatuwezi kuwa na ufanisi wa kweli bila hilo!

Kwa hivyo, kwa kuwa sasa tumeweka msingi mdogo wa sababu tunahitaji Ubatizo wa Roho Mtakatifu, hebu tuchunguze Maandiko yanayorejelea upako huu.



## SURA YA 5

# USHAHIDI WA KIMAANDIKO

Mojawapo ya njia bora ya kupata ufahamu wa Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kufuata wale walioupokea Siku ya Pentekoste kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Matendo. Tunapochunguza kila andiko, imani na ujasiri wako utaongezeka kwamba ubatizo huu upo kwa ajili yako pia.

*Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.*

*Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu. Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe.*

*Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, "Tazama, hawa wote wasemao si Wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo? Warparthi na Wamedi na Waelami, nao wakaao Mesopotamia, Uyahudi na Kapadokia,*

*Ponto na Asia, Frigia na Pamfilia, Misri na pande za Libia karibu na Kirene, na wageni watokao Rumi, Wayahudi na waongofu, Wakrete na Waarabu; tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu!”*

*Wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakiambiana, “Maana yake nini mambo haya?” Wengine walidhibaki, wakisema, “Wamelewa kwa mvinyo mpya.”*

—Matendo 2:1-13

Jambo la kwanza ninalotaka uone ni kwamba Biblia inasema wote walijazwa na Roho Mtakatifu! Pili, **wote** walinena kwa ndimi. Labda umesikia watu wakizungumza kuhusu siku ya Pentekoste na kueleza kwa nini wote walinena kwa ndimi. Wengine wanasisitiza kwamba lilikuwa tukio la mara moja kwa kanisa kwa sababu watu walikuwa wamekusanyika huko kutoka mataifa mengi na hivyo, lugha tofauti zilihajika kuhubiri Injili kwa watu wote wa lugha mbalimbali.

Lakini ukiangalia Maandiko, utaona yanasema wale 120 waliokuwa katika chumba cha juu walikuwa wanazungumza juu ya kazi za ajabu za Mungu. Hawakuwa wakihubiri Injili; walikuwa wakimsifu Mungu tu.

*“Tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu!” Wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakiambiana, “Maana yake nini mambo haya?”*

—Matendo 2:11b-12

Watu waliokuwa wamesimama hapo wakiwasikia wakimsifu Mungu kwa lugha zao za asili walishangaa na kufadhaika. Kisha Petro alisimama na kuhubiri ujumbe wa wokovu, na watu 3,000 waliongezwa kwa kanisa siku hiyo. Sasa, kama wanafunzi wangekuwa *wakihubiri* kwa lugha, Petro hangelizimika kusimama na kuhubiri. Lakini hadi Petro aliposimama kuhubiri, hawakujua walichokuwa wakisikia kilimaanisha nini. Ndimi hazikutumiwa kuhubiri Injili wakati huo, na hazijatumiwa kuhubiri Injili sasa. Tutashughulikia manufaa ya ndimi kwa muumini katika sura inayofuata, lakini kwa sasa, ninazungumzia hoja ya kawaida tu niliyoisikia.

Tena, nataka kueleza hoja kwamba Biblia inasema wote walipokea na wote walinena kwa ndimi. Sasa ikiwa Biblia ingetuacha pale pale, tungeweza kuwa na mashaka fulani kwamba kunena kwa lugha ni kwa ajili

ya kanisa zima. Lakini Biblia haifanyi hivyo. Badala yake, tunakuta jambo hili likiendelea na kutokea kwa kila mtu aliyepokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu baada ya siku ya Pentekoste.

Hebu nikusimulie kuhusu mmoja wa wanaume waliokuwepo Siku ya Pentekoste—jina lake lilikuwa Filipino.

*Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilibubiri neno. Filipino akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo. Na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na Filipino walipoyasikia na kuziona ishara alizokuwa akizifanya.*

—Matendo 8:4-6

Hapa tunamwona Filipino akidhihirisha Ufalme na watu wakimsikiliza. Ndivyo inavyopaswa kuwa leo! Watu *wanapoona* ishara, *wanapoona uthibitisho* wa Ufalme, watasikiliza kwa makini yale unayosema.

*Kwa maana pepo wachafu wakawatoka wengi waliopagawa nao, wakilia kwa sauti kuu; na watu wengi waliopooza, na viwete, wakaponywa. Ikawa furaha kubwa katika mji ule.*

—Matendo 8:7-8

Tazama kwamba Filipino alikuwa akitumia uwezo alikuwa amepokea alipokuwa Yerusalemu. Ishara zilimfuata, maana uweza wa Mungu ulikuwa dhahiri kwa watu wote. Alikuwa amepokea dunamis (neni la Kiyunani linalomaanisha *nguvu*); sasa aliweza kuwa shahidi wa Ufalme wa Mungu.

*Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawaapelekea Petro na Yohana; ambao waliposhuka, wakawaomba wampokee Roho Mtakatifu; kwa maana bado bajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu.*

—Matendo 8:14-17

Mitume huko Yerusalemu waliposikia kwamba Samaria imekubali Neno la Mungu, walituma kwao Petro na Yohana. Walipofika, waliwaomba ili wampokee Roho Mtakatifu kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa bado

hajamshukia hata mmoja wao. Hata hivyo Biblia inasema kwamba mapepo yaliondoka, watu waliponywa, matendo makuu ya Mungu yalikuwa yametokea, na watu walimwamini Yesu na kubatizwa kwa maji. Lakini pia inasema kwamba Roho Mtakatifu alikuwa bado HAJAWASHUKIA hata mmoja wao!

Wajua, Filipo alihubiri wokovu na waliukubali na kuupokea, lakini walikuwa bado hawajapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Walizaliwa mara ya pili, lakini tazama maneno haya: “Roho Mtakatifu; kwa maana bado hajawashukia HATA MMOJA WAO.” Ile tofauti ndiyo hiyo tena kati ya Roho Mtakatifu kuwa *ndani* yetu (yaani kuzaliwa mara ya pili) na Roho Mtakatifu kushuka *juu* yetu na kipaji hicho cha nguvu.

Biblia haisemi kwa nini Filipo hakuwa amewahubiria kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Inawezekana kwamba aliondoka Yerusalemu mwenyewe mara baada ya kubatizwa na Roho Mtakatifu bila kujua kwamba karama hiyo ilikuwa ya kila mtu. Kwa moja au nyingine, ilikuwa dhahiri kwamba watu walikuwa wameamini Injili na kubatizwa kwa maji, hivyo walizaliwa mara ya pili. Lakini tazama jinsi ilivyokuwa muhimu kwa mitume kwamba watu wa Samaria waupokee mara moja Ubatizo wa Roho Mtakatifu kama wao walivyokuwa wameupokea.

Wazo la kwanza walilokuwa nalo halikuwa kuwaambia jinsi ya kuvaa mavazi. Hawakusema, “Hebu tuwaambie jinsi ya kuvaa inavyostahili au wakati wa kuwa na ibada.” Hawakuwa na haja na kanuni za mafundisho. Hoja ya kwanza waliyokuwa nayo ilikuwa nini? Ubatizo wa Roho Mtakatifu! Kwa hiyo walifanya jitihada ya kuelekea huko mara moja na kuwaambia hawa watu wote kuhusu Ubatizo katika Roho Mtakatifu.

Kisha Petro na Yohana wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Hapo hapo wakampokea Roho Mtakatifu. Ushahidi ulikuwa upi? Ninaamini ilikuwa kama mtu yeyote mwingine: kuomba kwa ndimi.

*Hata Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha akisema, “Nipeni na mimi uwezo huu, ili kila mtu nitakayemweka mikono yangu, apokee Roho Mtakatifu.”*

*Lakini Petro akamwambia, “Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali. Huna fungu wala huna sehemu katika jambo*

*hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu! Basi, tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana, ili kama yamkini, usamehewe fikira hii ya moyo wako. Kwa maana nakuona u katika uchungu kama nyongo, na tena u katika kifungo cha uovu.”*

*Simoni akajibu, akasema, “Niombeeni ninyi kwa Bwana, yasinifikilie mambo haya mliyosema hata moja.”*

—Matendo 8:18-24

Simoni alipoona kwamba Roho alitolewa kwa kuwekewa mikono, aliwapa mitume fedha ili wampe uwezo huo. Lazima iwe kwamba Simoni aliona kitu fulani, ushahidi fulani kwamba jambo lilitokea walipompokea Roho Mtakatifu. Alitaka nguvu hizo.

Sasa, Biblia haisemi walinena kwa lugha papo hapo, lakini jambo fulani lilitokea waziwazi ambalo wangeweza kuona. Simoni aliona kitu ambacho kilikuwa na nguvu, na alitaka kuwa na uwezo huo huo wa kuwapa watu kitu hicho. Ninaamini maneno yake yanaonyesha kwamba walipokea ubatizo huo na kama mtu yeyote mwingine aliyepokea Roho Mtakatifu, walianza kunena kwa ndimi. Tena, nataka kuonyesha jinsi kanisa la Yerusalemu lilivyoona Ubatizo wa Roho Mtakatifu—ulikuwa muhimu sana!

Wongofu wa Paulo ulipotukia njiani kwenda Damaski, mtu mmoja aliyeitwa Anania alitumwa kwa Paulo ili kumwombea.

*Anania akaenda zake, akaingia mle nyumbani; akamwekea mikono akisema, “Ndugu Sauli, Bwana amenituma, Yesu, Yeye aliyekutokea katika njia uliyojija, upate kuona tena, ukajazwe Roho Mtakatifu.”*

—Matendo 9:17b

Biblia haisemi kwamba Paulo alinena kwa lugha alipopokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu, lakini tunajua kwamba alinena kwa ndimi, na ninaamini aliupokea kama kila mtu mwingine alivyopokea. Unaweza kuuliza, “Kwa nini niamini hilo?” Jibu ni rahisi. Ni kwa sababu ya kile ambacho Paulo, mwenyewe aliandika katika 1 Wakorintho 14:18.

*“Namshukuru Mungu ya kuwa nanena kwa lugha zaidi ya ninyi nyote.”*

Kwa hiyo, tunaweza kufikia hitimisho kwamba Paulo alinena kwa lugha

alipobalizwa katika Roho Mtakatifu. Unaposoma sura zote za Matendo, utagundua kwamba ubatizo huu uliendelea siku baada ya siku katika kanisa lote. Jambo hili halikutokea Siku ya Pentekoste tu.

Baadaye, katika Matendo 10, Petro alitumwa kwa watu wa Mataifa na kuongozwa kuwahubiria Injili. Kumbuka, hilo halikuwa jambo la kawaida sana kwa Petro, ambaye alikuwa Myahudi, kwenda kwenye nyumba za watu wa Mataifa. Alienda kwa sababu aliongozwa kwenda huko na maono kutoka kwa Roho Mtakatifu.

*Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno. Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu.*

*Ndipo Petro akajibu, “Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi?” Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha.*

—Matendo 10:44-48

Petro alipokuwa akihubiri Injili ya Kristo katika nyumba hii ya watu wa Mataifa, Roho Mtakatifu alikuja juu ya wote waliosikia ujumbe huo. Huwezi kumwona Roho wa Mungu, kwa hivyo walijua Roho Mtakatifu alikuja juu yao? Andiko linasema kwamba waamini waliotahiriwa waliokuja pamoja na Petro walishangaa kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu kilikuwa kimemiminwa hata juu ya watu wa mataifa mengine, kwa kuwa waliwasikia wakinena kwa lugha na wakimsifu Mungu.

Kwa hivyo kulikuwa na ushahidi gani kwamba Roho Mtakatifu alikuwa pale? Petro alipaswa kutambua kile ambacho kilikuwa dhahiri kwake, kwamba Mungu alikuwa amewakubali watu hawa. Ukweli kwamba aliwaona wakinena kwa lugha wakati hakuwa amewahi kuwahudumia chochote kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu, ulikuwa ushahidi pekee aliohitaji. Petro alijua walikuwa wamempokea Roho Mtakatifu kama yeye kwa sababu walikuwa wakiomba katika ndimi.

Utapata tofauti kubwa kati ya kile ambacho kanisa la kisasa linafikiri ni muhimu na kile ambacho kanisa lilifikiri kuwa muhimu katika nyakati za

kibiblia. Mojawapo ya Maandiko ninayopenda sana ambayo yanaonyesha wazi kwamba kila mtu anapaswa kubatizwa katika Roho Mtakatifu, na ni thibitisho bila shaka kwamba ni kazi ya Roho Mtakatifu mbali na kuzaliwa mara ya pili, iko katika Matendo 19:1-2.

*Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika Efeso; akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko; akawauliza, “Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?” Wakamjibu, “La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia.”*

Paulo alipoingia katika mji wa Efeso, alikuta baadhi ya wanafunzi, akawauliza, “Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?” Hii ilikuwa hoja ya kwanza ambayo Paulo alikuwa nayo alipokutana na waumini hawa.

Paulo alitambua kwamba kuzaliwa mara ya pili ni tofauti kabisa na kubatizwa kwa Roho Mtakatifu kukiwemo ushahidi wa kunena kwa lugha.

Kwa nini Paulo akashughulikia jambo hili kwanza kabisa? Kwa sababu ndilo lile lile Yesu alilosema katika Matendo 1:4! Kimsingi aliwaambia, “wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba!” Mitume walifanya nini huko Yerusalemu walipogundua kwamba watu wa Samaria walikuwa wamesikia Neno? Walisema, “Jamani, inukeni mwende kule sasa hivi. Lazima tuhakikishe kwamba jambo hili limeshughulikiwa vyema. Nendeni mhakikishe kwamba wamepokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Paulo alipokuwa akipitia Efeso, aliwakuta baadhi ya wanafunzi, jambo la kwanza aliwauliza, “Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?”

Walipojibu, “La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia,” Paulo aliwauliza ni ubatizo gani waliopokea. Wakamjibu, “Ubatizo wa Yohana.” Paulo alisema ubatizo wa Yohana ulikuwa ubatizo wa toba na aliwaambia watu kumwamini yule aliyekuja baada yake. Yaani wamwamini Yesu.

**SASA, NINAAMINI HII  
NI MADA YENYE UTATA  
KATIKA MAKANISA MENGI  
SI KWA SABABU HAIPO  
KATIKA BIBLIA, LAKINI  
KWA SABABU SHETANI  
ANAICHUKIA SANA.**

Waliposikia hayo, walibatizwa kwa jina la Bwana Yesu (kubatizwa kwa maji). Baadaye, Paulo alipoweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu alishuka juu yao, wakaanza kunena kwa lugha. Tazama kwamba wakati Paulo alipowauliza swali hilo, alidhani walimwamini Yesu. Ndiyo maana aliuliza, “Je! Mlipokea Roho

Mtakatifu mlipoamini?” Alielewa Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa tofauti kabisa na kuzaliwa mara ya pili.

Sasa, ninaamini hii ni mada yenye utata katika makanisa mengi si kwa sababu haipo katika Biblia, lakini kwa sababu shetani anaichukia sana.

Kwa sababu ikiwa huu ndio uwezo, ikiwa huu ndio mlango wa uwezo wa kubadilisha maisha na kuwa shahidi katika ulimwengu, basi ufahamu huu unakuja dhidi ya mungu wa ulimwengu huu, na tunajua maoni yake juu ya jambo hili ni yapi. Ubatizo wa Roho Mtakatifu hutupatia hifadhi ya nguvu, nguvu za Mungu, kufanya kazi za Yesu ili Mungu aweze kutukuzwa!



## SURA YA 6

# JE! WOTE HUOMBA KATIKA NDIMI?

Labda umesikia wengine wakisema kwamba wao hawaneni kwa lugha na hawaamini kwamba kila mtu anaweza au anapaswa. Kisha wananukuu 1 Wakorintho 12:27-30 kama sababu yao ya kuamini hivyo. Wataonyesha kwamba Paulo, mwenyewe alisema kwamba kila mtu haneni kwa ndimi. Vema, hebu tuangalie kifungu hiki ili tuone kama hivyo ndivyo Paulo alivyosema.

*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake. Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha. Je! Wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza? Wote wana karama za kuponya wagonjwa? Wote wanena kwa lugha? Wote wafasiri?*

—1 Wakorintho 12:27-30

Katika barua hii, Paulo aliliambia kanisa la Korintho jinsi ya kufanya kazi kwa utaratibu ili wote wahudumiwe katika mikusanyiko yao ya ibada kanisani. Wakati huo, wote walikuwa katika mashindano kila mmoja kwa vipawa vyake vya kiroho na wahubiri waliowapenda. Paulo alikuwa akiwaelekeza jinsi ya kufanya kazi kama mwili katika umoja na upendo. Sasa hebu tuangalie kwa makini 1 Wakorintho 12:27-28:

*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake. Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa [Ninapendekeza upigie mstari maneno haya], wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha.*

Paulo aliendelea kunena, lakini nitakoma hapo kwa sababu ninataka kuzungumza kidogo kuhusu kifungu hicho cha maneno, “katika kanisa.” Anazungumza kuhusu mkusanyiko halisi wa kanisa. Tunaweza kuthibitisha hilo katika 1 Wakorintho 14:18-19, ambapo Paulo alitumia kifungu hicho hicho cha maneno:

*Namshukuru Mungu ya kuwa nanena kwa lugha zaidi ya ninyi nyote; lakini KATIKA KANISA napenda kunena maneno matano kwa akili zangu, nipate kuwafundisha wengine, zaidi ya kunena maneno kumi elfu kwa lugha.*

—1 Wakorintho 14:18-19

Paulo alisema, “Namshukuru Mungu ya kuwa nanena kwa lugha zaidi ya ninyi nyote, **lakini katika kanisa...**” Ndicho hicho tena, na wakati huu ni wazi kwamba Paulo alizungumza juu ya mkusanyiko halisi wa kanisa na sio mwili wote wa Kristo ulimwenguni. Sote bila shaka tunakubali kwamba Paulo ni sehemu ya mwili mzima wa Kristo, yaani “kanisa.” Na alisema kwamba alifurahi kwamba yeye alinena kwa lugha zaidi ya waumini wote wa Korintho. Alisema hivyo kwa sababu kanisa hilo lilikuwa likifurahia uwezo wao mpya wa kunena kwa lugha, na walikuwa wametoka kwa utaratibu na kusababisha utata.

Kimsingi alikuwa akisema, “Jamani, mimi hunena kwa lugha zaidi ya ninyi nyote, lakini kuna njia ya kutekeleza hili ‘kanisani’ ambayo ina utaratibu na haiteti utata.” Aliendelea kusema kwamba, katika kanisa (mkusanyiko wa waumini), afadhali aseme kwa ufahamu (kwa lugha ya kawaida) ili wengine wapate kujengwa.

Katika ibada kanisani, baadhi ya watu watakuwa na karama ya lugha na ufasiri, kama ilivyoandikwa katika 1 Wakorintho 12, lakini wote hawatafanya hivyo au hawapaswi kufanya hivyo kwa madhumuni ya kuujenga mwili wote. Hata Paulo alisema watu wasiopita watatu ndio waliostahili kunena kwa lugha na ufasiri katika ibada.

*“Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, tena zamu kwa zamu, na mmoja na afasiri.” (1 Wakorintho 14:27)*

Kwa hiyo Paulo aliposema wote wasinene kwa lugha, alikuwa akirejelea, “kanisani,” au kusanyiko la kanisa.

Unahitaji kuelewa kwamba kila mwamini ana uwezo wa kuomba kwa ndimi, lakini si kila mtu ana upako wa kujitokeza na kutumia karama hiyo ya ndimi na ufasiri katika ibada ya kanisa. Iwapo una upako huo wa kutumia karama hiyo katika ibada, Biblia inasema kwamba unapaswa kuomba ili upate ufasiri.

*Kwa sababu hiyo yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kufasiri. (1 Wakorintho 14:13b)*

Ninaamini kwamba anayenena kwa lugha ndiye aliye na uwezo zaidi wa kufasiri katika ibada kwa sababu ujumbe tayari unapita ndani yake.

Kwa nini uombe kwa lugha? Ibilisi anawachukia waumini wanaojua kuomba katika Roho (kwa ndimi), na ninataka kuhakikisha kwamba unaelewa kwa nini.

Paulo aliposema kwamba alifurahi kwamba aliomba kwa lugha zaidi ya mtu mwingine yeyote, lazima kuwe na sababu iliyomfanya ahisi hivyo. Paulo alitoa maoni katika 1 Wakorintho 14 ambayo tunahitaji kusoma.

*“Yeye anenaye kwa lugha **hujijenga** nafsi yake; bali ahutubuye **bulijenga** kanisa.” (1 Wakorintho 14:4)*

Tutazame jambo hili kwa kina zaidi kidogo. Je, ina maana gani kujengwa? Neno jenga linamaanisha “kufundisha au kufaidika, hasa kiadili au kiroho; kuinua.”

Itakupasa kukubali kwamba kuna nyakati nyingi ambapo unahitaji kufundishwa ili kujua njia ya kufuata, kuelewa hali fulani, au kufanya uamuzi unaofaa. Huu ndio msaada unaoweza kupata kupitia kwa kuomba kwa lugha: kujijenga au kuleta mafundisho maishani mwako. Paulo anaweka wazi jambo hili katika Warumi 8:26-27:

*Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuomba kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Na Yeye aichunguzaye mioyo*

*aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu.*

Paulo anatuambia kwamba tuna tatizo na udhaifu: “Hatujui kuomba jinsi itupasavyo.” Labda unauliza, “Kwa nini tuna udhaifu huu?” Tunaweza kuelewa kwa nini tuna udhaifu huu kwa kusoma 1 Yohana 5:14-15.

*Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.*

Bila kujua au kuwa na uhakika wa mapenzi ya Mungu, hatuwezi kuwa na imani (kukubaliana na Mungu), na ikiwa hatuna imani, basi hakika tuko katika hali dhaifu kwa sababu hatutaweza kupata neema au nguvu za Mungu bila imani kuwepo. Kwa hiyo Paulo anasema kwamba kutojua kuomba ni hali dhaifu ambayo kuomba kwa lugha kunaweza kusaidia. Hebu tusome andiko letu tena.

*Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo.*

—Warumi 8:26a

Udhaifu wetu ni kwamba hatujui kuomba! Biblia haituambii ni nani tunapaswa kufunga ndoa naye, tuishi wapi, au tufanye kazi gani. Bila kujua mapenzi ya Mungu, hatuwezi kujua na kuamini kwamba tunapokea kutoka kwa Mungu tunapoomba. Tena, huu ni udhaifu mkubwa! Hatuwezi kuwa imani katika Mungu wakati hatujui mapenzi Yake ni nini. Lakini kuna njia ambayo tunaweza kutambua mapenzi ya Mungu katika kila hali maishani. Kuna njia ambayo tunaweza kuwa na uhakika wa mapenzi ya Mungu ili tuweze kuwa na imani na ujasiri.

Hicho ndicho Paulo anachozungumzia. Kujijenga huku anakozungumzia kunamaanisha kupata maarifa aina hii—maarifa ambayo huja kupitia kwa Roho wa Mungu. Na tunamsikia Roho kwa kuomba katika Roho, au ndimi. Tukifuata ushauri wa Paulo zaidi katika Warumi 8:26b-27, tunasoma yafuatayo:

*Lakini Roho mwenyewe hutuomba kwa kuugua kusikoweza*

*kutamkwa. Na Yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu.*

Sasa Paulo hasemi kwamba tunaugua tunapoomba katika Roho lakini, Paulo anarejelea mistari iliyotangulia.

*Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa. Wala si hivyo tu; ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya Roho, sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukikutazamia kufanywa wana, yaani, ukombozi wa mwili wetu. Kwa maana tuliokolewa kwa taraja; lakini kitu kilichotarajiwa kikionekana, hakuna taraja tena. Kwa maana ni nani anayekitarajia kile akionacho? Bali tukikitarajia kitu tusichokiona, twakingojea kwa saburi.*

*Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu.*

—Warumi 8:22-27

Paulo anatumia neno kuugua hapa kama kielelezo au ulinganisho wa kile kinachotokea ndani yetu. Tunaugua kwa ndani, kama mwanamke anayejifungua. Hiyo ni kusema kwamba, tunazaa kitu kutoka kwa Roho wa Mungu ndani yetu, tunapokea kitu kipya, kitu ambacho hakijawahi kuwepo hapo awali; au unaweza kusema, jambo lisilotoka kwetu sisi wenyewe. Kwa hiyo “tunazaa” ujuzi wa kile ambacho hatujui, kitu kipya, kutoka kwa roho zetu kupitia kwa mchakato wa kuomba katika Roho. Biblia inatambia kwamba Roho wa Mungu huomba mapenzi kamili ya Mungu kwa hali yoyote kupitia kwa roho zetu. Inasema kwamba Mungu, Mwenyewe hutuombea, kwa njia ya roho zetu za kibinadamu, kwa kuugua kusikoweza kutamkwa (kuelezwa kwa maneno yanayoeleweka).

Kwa hiyo kile tunachogundua hapa ni kwamba Roho Mtakatifu hutuombea kwa kuugua (kuzaa) kwa kutumia maneno yasiyoweza kutamkwa, wala kueleweka (au ndimi). Na Yeye aichunguzaye mioyo yetu aijua nia ya Roho kwa sababu Roho (Roho wa Mungu) hutuombea watakatifu sawasawa na mapenzi kamili ya Mungu. Roho wa Mungu

huomba mapenzi kamili ya Mungu kwa kila hali **kupitia roho yako mwenyewe unapoomba kwa ndimi.**

Kwa hivyo, tuko katika hali dhaifu wakati hatujui mapenzi ya Mungu. Imani haiwezi kuachiliwa hadi tujue mapenzi ya Mungu. Paulo anasema kwamba ikiwa tutaomba katika Roho, Roho wa Mungu mwenyewe ataomba kupitia kwetu mapenzi Yake kamili kwa maisha yetu katika hali yoyote.

Roho wa Mungu anapoomba kupitia kwetu kwa ndimi, basi tunawezaje kujengwa maana hatujui tunayoyasema? Jibu linapatikana katika barua nyingine ambayo Paulo aliandika.

Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho.

*Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu. Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohani kwa maneno ya rohani.*

—1 Wakorintho 2:9b-13

Kwanza kabisa, Paulo alisema kwamba tunaweza kuyapata mambo ambayo hatujawahi kusikia, kuona, au kufikiria, kama jinsi nimekuwa nikishiriki nawe. Lakini aliendelea na kutuambia jinsi mambo yalivyo:

*Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu.*

—1 Wakorintho 2:11

Kabla sijashughulikia kipengele hiki cha Maandiko, tunahitaji kwanza kuwa na somo la msingi katika fundisho letu. Kulingana na 1 Wathesalonike 5:23, mwanadamu ana sehemu tatu: roho, nafsi, na mwili.

*Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.*

—1 Wathesalonike 5:23

Roho zetu ni sehemu ya Mungu iliyo ndani yetu; nafsi yetu ni akili, mapenzi yetu, na hisia zetu; na tatu, miili yetu. Paulo alisema kwamba nafsi zetu (akili, mapenzi yetu, na hisia) na roho zetu zimeunganishwa kwa ukaribu sana kiasi kwamba roho zetu zinaweza kufahamu mawazo yetu ni nini.

Kinyume chake ni kweli pia. Akili zetu zinaweza kufahamu mawazo ya roho zetu. Paulo alisema kwamba Roho wa Mungu anajua mawazo ya Mungu na kwamba tumepokea Roho wa Mungu ili tuweze kujua kile ambacho Mungu ametupatia bila malipo.

*Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohani kwa maneno ya rohani.*

—1 Wakorintho 2:12-13

Paulo anaendelea kusema kwamba ufahamu huu tusiokuwa nao unaofunuliwa kwetu na Roho wa Mungu, ni yale tunayoyasema ambayo tunafundishwa na Roho, wala sio maneno tunayoweza kusema ya lugha au ufahamu wetu asili bali maneno ya kiroho. Tunajua kwamba Paulo anazungumzia kuomba kwa ndimi anaposema tuombe kwa maneno ya kiroho kwa sababu alitumia ufafanuzi huo huo kueleza kuhusu kunena kwa ndimi katika 1 Wakorintho 14:14-15:

*Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda. Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; nitaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia.*

Paulo anatumia maneno “kuomba kwa roho” kurejelea kunena kwa ndimi. Tunaweza kuhitimisha kwamba Paulo anarejelea kunena huku kwa lugha anaposema kwamba tunanena kwa maneno tuliyofundishwa na Roho.

*Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake.*

—1 Wakorintho 14:2

Tena, Paulo anasema kuhusu roho zetu kuwa na uwezo wa kunena mambo ambayo hatujawahi kuona, kusikia, au kuwa na ujuzi kuyapata, au kama vile Paulo asemavyo, “siri.” Pia tazama katika mstari huu Paulo anasema tunaomba siri katika roho zetu wenyewe, wala sio Roho wa Mungu. Je, jambo ambalo hatukujua huingiaje katika roho zetu? Jibu ni rahisi! Kupitia kwa Roho wa Mungu, ambaye sasa ni kitu kimoja na roho zetu.

*Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu.*

—1 Wakorintho 2:11

Roho zetu zinapopata mawazo ya Mungu, akili zetu pia hupokea mawazo haya. Akili zetu zinapotafakari mawazo ya Mungu, tunaita hilo “ufunuo,” “kutiwa nuru,” au, kama Paulo asemavyo, “kujengwa.” Sasa unajua kwa nini Paulo alisema alifurahi kwamba aliomba kwa lugha zaidi ya mtu yeyote mwingine; alipata faida ya kujua mapenzi ya Mungu katika kila hali.

**UBATIZO WA ROHO  
MTAKATIFU NI SILAHA YA  
SIRI YA MUNGU! ANAWEZA  
KUSHUSHA MAPENZI  
YAKE DUNIANI BILA  
SHETANI KUJUA NI NINI  
KINAENDELEA.**

Hili ndilo Paulo analorejelea katika 1 Wakorintho 2:15-16.

*“Lakini mtu wa rohoni huyatambua yote, wala yeye hatambuliwi na mtu. Maana, ‘Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimish?’ Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.”*

Hatuzuiliwi na hukumu ya kibinadamu, lakini tunaweza kufanya maamuzi kuhusu mambo yote kupitia kwa msaada wa Mungu. Hii ni habari njema ajabu! Tunao uwezo, kwa kuomba katika Roho (ndimi), kupokea siri, mambo ambayo hatukujua; na kwa ujuzi huo, tunaweza kufanya maamuzi sahihi kuhusu mambo yote!



Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni silaha ya siri ya Mungu! Anaweza kushusha mapenzi Yake duniani bila shetani kujua ni nini kinaendelea. Hakika kuomba katika Roho kumeorodheshwa kama sehemu ya silaha zetu za kiroho katika Waefeso 6:18a:

*Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho.*

Kuomba katika Roho hutupatia fursa ya kupata mikakati ambayo itatuwezesha kumweka adui kando, au kupiga hatua kwenda mbele kwa kutumia mbinu za kipekee na zisizo za kawaida.

Faida inayodokezwa ni kwamba tutaweza kufanya maamuzi yanayofaa maishani kwa kutumia akili ya Kristo. Nafikiri inakupasa ukubali kwamba hili ni jambo muhimu! Limekuwa muhimu kwangu!

Kwa mfano, ninakumbuka nilipokuwa na hitaji la kufanya uamuzi mkubwa kuhusu biashara yangu. Mwakilishi wa uuzaji niliyefanya kazi naye, ambaye aliwakilisha mmoja wa wachuuzi wangu, alikuwa akitishia kupeleka kampuni yangu mahakamani kwa sababu sikutaka kumfuata alipojiunga na kampuni nyingine. Alinitaka niendeleo kufanya biashara naye huku akiachana na mchuuzi ambaye siku zote nimefanya biashara naye. Nilipenda mwakilishi wangu wa uuzaji, lakini nilihisi uaminifu wangu ulikuwa kwa kampuni aliyofanyia kazi, wala si kwake. Hata hivyo, kampuni aliyofanyia kazi walimwambia kwamba wateja wake wote wangeweza kuhama naye kwenda kwa hiyo kampuni mpya. Kwa hiyo nisingekuwa nikifanya chochote kibaya kwenda naye, lakini bado sikujisikia vyema kulazimishwa kwenda naye. Kampuni aliyokuwa akifanyia kazi ilikuwa imenitendea haki kila wakati kufikia hapo.

Alikuwa akitishia kunishtaki kwa sababu miezi michache awali alikuwa ametaja kuhusu suala hilo la kujiunga na kampuni mpya na akaniuliza ikiwa ningenda naye. Bila kufikiria vyema, nilikuwa nimekubali kufanya hivyo. Alisema alikuwa akitegemea biashara yangu alipofanya uamuzi wa kubadili makampuni. Lakini sasa alipokaribia tarehe ambayo alikuwa akiondoka, nilihisi wasiwasi kuhusu hilo. Kwa hivyo niliomba katika Roho kwa siku kadhaa. Lakini bado sikuweza kusikia jibu nililohitaji.

Mimi na Drenda mara nyingi huwapeleka watoto wetu kwenye uwanja mkubwa wa burudani ulio umbali wa masaa machache unaoitwa *Cedar Point*. Kwa kweli ni uwanja mkubwa zaidi mwenye vijigari vidogo vinavyoenda kwa kasi kwa mzunguko au miteremko huku vikiwa vimeunganishwa nchini Marekani, na kwa kawaida huwa tunaenda huko mara kadhaa kwa

mwaka. Ilikuwa Ijumaa usiku, na nilipaswa kuwa na jibu Jumatatu asubuhi kuhusu kile cha kufanya. Niliamua ingekuwa vyema kuondoa mawazo yangu kwa jambo hilo na kuyaweka kwa kitu kingine kwa muda mfupi, hivyo niliamua kuchukua Drenda hadi bustani jioni hiyo. Nilipokuwa nimesimama kwenye laini, bila hata kufikiria juu ya uamuzi ule niliipaswa kufanya kabla ya Jumatatu asubuhi, ghafla, nilijua cha kufanya. Ilikuwa dhahiri kama mng'ao wa siku. Roho Mtakatifu alinena nami, na nikabaki katika ile kampuni ya kwanza. Kampuni mpya ya mwakilishi wangu wa uuzaji ilifungwa chini ya muda wa miezi michache.

Kwa hiyo hapa kuna ufunguo muhimu wa mafanikio—omba! Omba katika Roho mara kwa mara ili kila kitu kikuendee vizuri na ufanye maamuzi sahihi, pamoja na kupokea siri za kimkakati unazohitaji ili kushinda.

*Ombeni bila kukoma.* (1 Wathesalonike 5:17)

## SURA YA 7

# SANDUKU LA HAZINA

Nakumbuka siku ya kwanza nilipokutana na Dan. Alikuwa amesimama nyuma ya kanisa, katika safu ya mwisho kabisa, pamoja na binamu yangu Jennifer. Niligundua baadaye kwamba walikuwa wakichumbiana. Hata hivyo, niliweza kuona kwamba Dan alihisi hakuwa mahali palipomfaa. Kwa kweli, alionekana kutokuwa starehe. Niligundua baadaye kwamba kanisa letu lilikuwa tofauti kidogo na kanisa lake la kimadhehebu alilohudhuria. Lakini alipoanza kusikia kuhusu Ufalme, alianza kuonekana kuwa starehe na, hatimaye, akamuoa binamu yangu.

Wakati huo, Dan alikuwa akifanya ukilima kwenye shamba la ekari karibu 1,400 katika sehemu ya kati ya Ohio, na hilo halikuwa likiendelea vyema. Hakuwa akipata faida na alikuwa na wasiwasi sana. Lakini alipoendelea kusikia juu ya Ufalme na jinsi Roho Mtakatifu anavyoweza kuwa msaada, siku moja alimwambia Jennifer, “Nataka kuongeza utoaji wetu maradufu.” Jennifer alishtuka lakini alifurahi sana. Basi wakafanya hivyo.

Mwaka huo, mavuno yao kwenye ekari hizo hizo 1,400 yalikuwa juu kwa 128% kuliko mwaka uliokuwa umepita. Mazao yalikuwa juu sana, kiasi kwamba waliweza kulipia gari pesa taslimu na kununua, na pesa taslimu, shamba lingine, jambo ambalo lilimaanisha kupanda ekari zaidi mwaka uliofuata. Dan alifurahi sana! Alisema ingemchukua babake miaka 10 kulipia shamba hilo jipya, lakini yeye alikuwa amelilipia pesa taslimu. Kwa hiyo nilimuuliza Dan anisimulie na kunieleza jinsi hilo lilivyotokea.

Inaonekana kwamba baada ya Dan na Jennifer kuanza kutoa matoleo maradufu, pia walikuwa wakiomba Mungu awaonyeshe cha kufanya. Dan alisema siku moja alipokuwa akipitia rundo la kawaida la barua alizokuwa akipokea kila siku, nyingi zikiwa ni matangazo ya masoko kwa wakulima,

alikuwa ametupa kadi ndogo kwenye pipa la taka alipohisi kuitoa humo. Hakukuwa na kitu maalum kuhusu kadi hiyo ndogo, lakini ilikuwa na tangazo kuhusu vifaa cha kutumia shambani. Tangazo hilo liliwaalika wakulima kwa mkutano wa kujadili kifaa hicho.

Dan alihisi hamu ya ajabu ya kwenda, na, baadaye alinunua kifaa hicho kilichotangazwa. Kilikuwa kifaa kipya katika soko kilichosaidia katika upanzi, kuweka mbegu ardhini na kutayarisha udongo. Dan alijaribu kunieleza sababu za kisayansi ya ufanisi katika ongezeko la mavuno ya mazao, wala sikuelewa kila jambo aliloeleza. Lakini yeye alielewa, na hilo ndilo lililokuwa muhimu. Dan aliniambia kwamba alikuwa mkulima wa pili kununua kifaa hicho huko Ohio wakati huo. Naam, kilisababisha ongezeko la asilimia 128% katika mavuno. Dan aliendelea kununua ardhi zaidi, na leo, ni mkulima wa maelfu ya ekari. Sasa ana hadithi nyingi za jinsi Roho Mtakatifu alivyomsaidia kufanya maamuzi ambayo yalimsukuma kwa kasi zaidi kuliko vile alivyofikiria.

Kwa hiyo Dan alibadilishaje shamba lake mbovu na kulifanya shamba lenye faida kubwa? Alifuata ushauri wa Mshauri wake, Roho Mtakatifu. Jambo la kusikitisha ni kwamba Wakristo wengi husikia hadithi hii na hawaelewi jinsi lilivyotokea, ndiyo maana niliona ni muhimu sana kuandika kitabu hiki. La, Wakristo wengi watasherehekea jinsi Mungu alivyo mkuu, huku wakikubali kwamba hilo lilikuwa jambo ajabu la Mungu, lakini bila ufahamu wa jinsi ya kuliiga. Kisha tunakuwa na kikundi cha Wakristo waliokatishwa tamaa na Mungu na kumlaumu kwa ajili ya shida zao. “Mungu yuko wapi? Sijui kwa nini Mungu hajanisaidia,” ndivyo huwa ninasikia mara nyingi.

Natumai kufikia hapa tayari umetambua hivi, Ufalme hufanya kazi kupitia kwa sheria wala si kwa upendeleo. Mungu hachagui wale atakaowabariki na wale ambao hatawabariki. Dan sio mmoja wa wateule spesheli wala hana umaalum zaidi kukuliko wewe mbele za Mungu. Una haki za kisheria sawa na Dan katika Ufalme. Jinsi vile kila mtu ana haki ya kupanda mbegu na kukuza mimea, Ufalme wa Mungu hufanya kazi kwa ajili ya yeyote anayejua jinsi ya kutumia sheria zake. Wewe ni mshiriki wa nyumba ya Mungu na raia wa Ufalme Wake mkuu na una kibali cha kupata yote aliyo nayo.

**Kwa hivyo acha nikuambie kwa nini watu wengi wa Mungu hukosa kufaulu maishani. Hawajui jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi ingawa wanajua jinsi ya kumsikia Roho Mtakatifu.**

*Bwana, Mkombozi wako, mtakatifu wa Israeli, asema hivi;  
“Mimi ni Bwana, Mungu wako, nikufundishaye ili upate faida,  
nikuongozaye kwa njia ikupasayo kuifuata.*

—Isaya 48:17

Mafanikio ya Dan hayakutokea kwa sababu Dan aliyawazia. Ilikuwa mbinu tu ya kipekee ya Roho Mtakatifu aliyoitambua Dan maana alichukua hatua za kutumia sheria ya Ufalme, na yeye na mke wake walikuwa wakimsikiliza Roho Mtakatifu azungumze ili kuwapa mpango. Nataka uandike hili.

## ROHO MTAKATIFU ANA MPANGO!

**Hakuna kitu chenye nguvu zaidi kuliko kuwa na mpango. Bila mpango, picha ni ndoto, lakini ukiwa na mpango, ndoto inaweza kutekelezwa.**

Familia inaweza kuwazia kuwa na nyumba nzuri, yenye vyumba vingi vya kulala, sebule kubwa, jiko kubwa la kisasa, na umaridadi. Lakini wakati huo, hiyo ni ndoto tu, yaani picha. Picha hiyo inabidi kuchorwa, kisha kutengenezwa kuwa ramani, yaani mpango. Mjenzi akishakuwa na ramani, nyumba inaweza kujengwa. Kwa sababu moja au nyingine, Wakristo wengi wana kile ninachokiita mtazamo wa sanduku la barua. Wanapomwomba Mungu pesa wanazohitaji, kama Dan alivyofanya, wanatarajia zijitokeze kwenye sanduku lao la barua, au hata vibaya zaidi, wanatarajia mtu awape pesa hizo. Hawana fununu kuhusu mchakato unaohitajika.

Ndio, kwanza, unapaswa kuwa na picha. Lakini kuna mchakato wa kufanya picha hiyo kuwa kitu halali ambacho unakifurahia. Jibu ni kuwa na mpango au mkakati unaohitajika ili kuitimiza picha hiyo. Hebu nikupe mfano. Ikiwa ningekuambia ninaweza kusuluhisha masuala yako ya kifedha haraka sana kwamba ninataka uchukue kalamu na karatasi yako ili nikwambie unachohitaji kufanya, ungefanya hivyo haraka ili kusikia jibu lako. Pia ikiwa ningeweza kuwaambia watu wengi wanaosoma kitabu hiki kwamba ninachotaka kuwaambia labda kinaweza kuondoa shinikizo lao la kifedha pamoja na kuwatoa kwa madeni kabisa kabla ya mwaka kuisha. Sasa, mikono yao ingeshikilia kalamu kwa nguvu zaidi, na wangejikaza ili kuhakikisha wasikose kile ninachotaka kusema.

Kwa kweli jibu ni rahisi sana, nitaeleza. Mwaka huu pata faida ya jumla ya dola milioni 10. Pengine utanitazama kwa muda kisha uanze kucheka.

Kisha nifikiri kwa kucheka kwako kwamba dola milioni 10 hazitoshi, kwa hivyo niongeze, “Vema, ikiwa hazitoshi, basi acha iwe dola milioni 25.” Kwa hili, unianza kucheka kwa sauti kubwa. Kwa nini? Acha nikuambie kile ambacho kimetokea. Kwa watu wengi, dola milioni 10 zinaweza kuwaweka huru kweli kutokana na madeni, lakini kicheko kiko pale kwa sababu hawawezi kujiona wakiwa na faida ya dola milioni 10 kwa mwaka mmoja. Kuwa na dola milioni 25 kunaleta kicheko kwa sababu ni mbali sana na mtazamo wao.

Lakini hebu tuseme kwa mfano ninamiliki kampuni ya kuuza bidhaa nje ya nchi, na nilijitolea kukulipa \$1,000 kwa kila mpira utakaotia kwenye kisanduku kwa ajili ya usafirishaji. Hebu pia tuseme kwamba unaweza kuandaa takriban masanduku 500 kwa siku, na pia tuwe na mkataba wa miezi 12 kwa malipo sawa. Nimetia chumvi sana kwa madhumuni ya kielelezo tu, lakini hili litaeleza hoja yangu vyema.

## **ACHA NISEME TENA— NAFIKIRI UNAHITAJI KUSIKIA HILI TENA— MUNGU ANA MPANGO WAKO!**

Sasa, hebu tuseme kuwa hakika una mkataba na mimi, na nitoe kauli niliyokupa awali, kwamba jibu lako la kifedha ni kuwa na mapato halisi ya dola milioni 10 mwaka ujao, jibu lako litakuwaje? Sasa, hutacheka. Badala yake utakuwa na kelele za furaha na msisimko mkubwa. Kwa nini? Kwa sababu kuwa na mapato ya dola milioni 10 itakuwa rahisi. Kwa kweli, itakuwa rahisi kuwa na mapato ya dola milioni 25, au hata dola milioni 100 pia. Ni nini kilibadilika? Jambo moja tu—una mpango. Kama vile nilivyosema hapo awali, kwamba mtu yeyote anaweza kuvua samaki ikiwa Yesu atamwonyesha mahali na jinsi ya kuvua, ndivyo ilivyo kwako sasa. Ukishakuwa na mpango, mpango unaoweza kujiona ukiutekeleza, tatizo lako limetatuliwa.

*“Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi,” asema Bwana, “ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.” (Yeremia 29:11)*

Acha niseme tena—nafikiri unahitaji kusikia hili tena—Mungu ana mpango **WAKO!**

Miezi michache iliyopita, nilipata fursa ya kukutana na mmoja wa washirika wa huduma yangu katika kanisa nililokuwa nimeenda kufundisha. Alikuwa mwishoni mwa ibada na swali, au niseme kauli. “Haikufanya kazi!

Nilitoa matoleo yangu, kisha nikakubaliana na mume wangu kuhusu kupata fahali wangu, na sikupata hata mmoja.” Aliniambia jinsi alivyotoa matoleo kwa ajili ya fahali hususa, na dume ambaye ningempiga risasi rahisi. Kwa hiyo nilianza kuuliza maswali zaidi na mwishowe nikamuuliza ikiwa labda alikuwa amemwona siku aliyokuwa ameenda kuwinda. Alisema, “Ndio, aina ya dume hasa niliyekuwa nimetolea matoleo alikuja akasimama karibu nami kwa umbali rahisi wa kumpiga risasi.”

Sasa, nilishtuka kidogo kusikia hilo, kwa hivyo nikamuuliza kilichotokea baadaye. Alisema alipiga risasi vyema kabisa, lakini alikuwa amemwomba rafiki yake alenge bunduki yake vizuri, na, katika kudhani kwamba rafiki huyo alikuwa amefanya hivyo, hakuangalia bunduki yeye mwenyewe na hivyo risasi haikumpiga yule mnyama. Kwangu ilikuwa dhahiri sana, lakini cha kushangaza, haikuwa hivyo kwake.

Nafikiri hapa ndipo waumini wengi walipo. Kwa sababu moja au nyingine, hawaelewi vyema mchakato, yaani sehemu yao katika kupata mavuno. Ilinibidi nimweleze kwamba Mungu alikuwa amefanya sehemu Yake, lakini alikuwa amekosea katika kutekeleza sehemu yake. Wajua, Mungu anaweza kukupa mpango, lakini unapaswa kutekeleza kwa njia sahihi sehemu yako katika mpango huo ili uweze kutimia. Ni wewe pamoja na Mungu!

*Tena ufalme wa mbinguni umefanana na hazina*  
**ILIYOSITIRIKA** katika shamba; ambayo mtu alipoiona, aliificha;  
na kwa furaha yake akaenda akauza alivyo navyo vyote, akalininua  
shamba lile.

—Mathayo 13:44

Kuna ukweli mwingi kuhusu Ufalme katika Maandiko haya! Kwanza kabisa, hebu tufafanue neno hazina. Kulingana na kamusi, hazina ni kitu chenye thamani au bei ghali cha aina yoyote ile. Kwa hiyo hazina si lazima iwe kipande cha dhahabu; inaweza kuwa kitu chochote unachohitaji wakati huo. Maandiko haya yanasema kwamba Ufalme wa mbinguni ni kama hazina, au unaweza kusema kwamba kila kitu unachohitaji katika maisha kiko katika Ufalme huu. Kwa hivyo Ufalme uko wapi? Katika Maandiko haya, Yesu anasema umefichwa shambani. Lo, si ungependa kujua mahali shamba hilo liko wapi? Habari njema ni kwamba Yesu anatuambia shamba hilo liko wapi na pia jinsi ya kupata hazina iliyofichwa humo.

Tukienda kwa Mfano wa Mpanzi katika Marko 4, tunampata Yesu

akifundisha jinsi imani inavyozalishwa katika moyo wa mwanadamu. Analinganisha roho ya mwanadamu na ardhi na Neno la Mungu kama mbegu iliyopandwa ardhini. Kwa kutumia ulinganisho huo huo, naweza kusema kwamba msingi unaorejelewa hapa katika Mathayo 13 unamaanisha roho ya mwanadamu. Nataka kuchukua muda mfupi kukukumbusha yale tuliyojifunza katika sura ya 6, kwamba tunapozaliwa mara ya pili, roho yetu ya kibinadamu hufanyika kitu kimoja na Roho wa Mungu, jambo linalotuwezesha kupata mawazo ya Mungu. Kwa hiyo hazina iliyo shambani haina vikomo vya kibinadamu, bali inajumuisha yote Mungu aliyo nayo maana tuko kitu kimoja naye katika Roho.

*Lakini, kama ilivyoandikwa, mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu. Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu.*

—1 Wakorintho 2:9-12

Kisha 1 Wakorintho 2:16 inaongeza kwamba sisi tuna nia ya Kristo! Yesu anathibitisha mahali hazina hii ilipo katika Luka 17:20-21.

*Ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza ... kwa maana, tazama, ufalme wa Mungu umo ndani yenu.*

—Luka 17:20-21

*Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.*

—1 Wakorintho 6:19-20

Hebu nifanye muhtasari wa kile ninachosema.



## KUNA HAZINA NDANI YAKO!

Hazina kiasi gani? Hazina zaidi ya ndoto zako kubwa! Hazina isiyo na kipimo!

*Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu.*

—Waefeso 3:20

Sasa, hapa ndipo tutalazimika kujizoeza kwa njia tofauti. Hazina hii ni zaidi kuliko tunavyoweza kufikiria! Kwa kawaida, tunapohitaji kitu au msaada, tumejizoeza kuangalia nje ya nafsi zetu kupata jibu. Lakini sasa, Roho Mtakatifu, ambaye ni Mungu Mwenyewe, anaishi ndani yetu na ndiye msaada wetu. Tayari tumejadili jinsi kuomba katika Roho au kwa lugha kunavyoleta mafundisho na kufunua siri. Lakini watu wengi wana wakati mgumu kufahamu jinsi msaada huu ulivyo wa thamani sana au kwamba Mungu anataka kweli kuwa jibu lao katika kila eneo la maisha yao.

**RAFIKI YANGU,  
TAYARI YOTE NI YAKO,  
UFALME WOTE. MUNGU  
Hawezi kuongeza  
CHOCHOTE KATIKA KILE  
ALICHOKWISHA KUKUPA.  
TAYARI UNAYO YOTE!**

Lakini ulipozaliwa mara ya pili, ulifanyika mshiriki wa nyumba ya Mungu mwenyewe na raia wa Ufalme Wake mkuu. Tayari amekupa kila kitu alichonacho! Luka 12:32 inasema hakuna sababu ya kuogopa au kuwa na woga maana Baba yako amefurahia kukupa Ufalme. Ufalme upi? Ufalme Wake!

*“Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme.” (Luka 12:32)*

Rafiki yangu, tayari yote ni yako, Ufalme wote. Mungu hawezi kuongeza chochote katika kile alichokwisha kukupa. Tayari unayo yote! Watu wengi hufikiri kwamba wanamsumbua Mungu wanapomshirikisha katika maisha yao ya kila siku. Lakini huo ni ujinga mtupu tu. Ikiwa ningekuambia kwamba wewe ni raia wa Marekani, kisha ukasema, “Vema, lakini sijui. Kama ningefungua duka hapa, ninahofia kuwasumbua watu kwa kutaka kutumia baadhi ya sheria za nchi ambazo zitaniwezesha kufungua biashara yangu hapa.” Kama raia, tayari una sheria na haki zote ambazo nchi nzima

inapaswa kukupa. Zote ni zako! Usisite. Nyakua faida zote zilizo zako tayari!

### **Kwa nini Ufalme wa Mungu unalinganishwa na hazina?**

Kwa sababu ikiwa una maarifa ya mbinguni, unaweza kujua ni nini cha kufanya katika kila hali kwa kutumia mikakati ya kipekee na isiyo ya kawaida ambayo umepewa na Mungu. Hebu nikupe mfano mwingine wa jinsi jambo hili linavyofanya kazi.

Mimi na Drenda tulipoanza kujifunza kuhusu Ufalme, maisha yetu yalibadilika sana. Kutoka kwa madeni kabisa kulikuwa kama kupumua hewa safi, na maisha yetu yalipata harufu mpya kabisa. Ajabu ya kulipia ekari zetu 55 pesa taslimu ilikuwa kama ndoto, ilishangaza sana, lakini bado tulihitaji kujenga nyumba juu yake. Hatukujua chochote kuhusu kujenga nyumba, na hatukujua kabisa mahali pa kuanzia. Lakini tulianza kuomba kuhusu JINSI ya kujenga nyumba tuliyohitaji katika shamba hilo. Ilitubidi tumwamini Roho Mtakatifu atusaidie.

Katika kutaka kukaa bila madeni kabisa, tulianza kuchunguza njia zisizo za kawaida za kujenga nyumba. Njia moja ya kujenga nyumba nzuri ya bei ya chini ilikuwa kuweka nyumba ya mbao. Nyumba aina hii huandalwa kwa visehemu katika kiwanda kisha kusafirishwa na kuunganishwa kwenye shamba lako. Nyumba aina hii ni bora kama nyumba za mbao lakini bei yake ni nafuu kutokana na mbinu bora za ujenzi zinazotumika kiwandani. Kwa hivyo tulichunguza kampuni mbili au tatu za ujenzi na miundo waliyokuwa nayo. Baada ya kutafiti na kuangalia nyumba hizi, tulihisi hiyo ndiyo njia ya kufuata na tukachagua kampuni na muundo ambao tulifikiri ungetoa nyumba nzuri kwenye shamba letuu. Tulikuwa tayari kutia sahihi mkataba baada ya kurudi nyumbani kutoka kwa mkusanyiko wa shule ya nyumbani tulioalikwa kuzungumza huko Virginia. Tuliamua kubeba mipango pamoja nasi ili kujadili maelezo yoyote ambayo hatukufahamu na kuwa na uhakika kwamba hiyo ndiyo njia ya kufuata kabla ya kusaini mkataba mara tuliporudi.

Sikumbuki jinsi ilivyotokea kwamba tulialikwa kuzungumza katika mkutano kule Virginia, lakini tulialikwa kukaa na moja ya familia za shule ya nyumbani tulipokuwa huko. Tulipofika katika nyumba yao nzuri ya muundo wa nyumba za Kusini na kukutana na marafiki wetu wapya, tulianza kutoa maoni juu ya jinsi nyumba yao ilivyokuwa ya kupendeza. Katika mazungumzo hayo, tuligundua kwamba walikuwa wameijenga wenyewe. Nilishtuka mwanzoni. “Kwani nyinyi ni wakandarasi?” Nikauliza. “La,” wakasema. Baba huyo alitufahamisha kwamba alikuwa mhasibu katika kampuni kubwa ya eneo hilo. “Kweli, ulijuaje jinsi ya kujenga nyumba

yako mwenyewe?” Nikauliza.

Walianza kusema mambo mbalimbali, na katika mazungumzo hayo, tuliwaambia tulitaka kujenga nyumba pia na tulikuwa karibu kutia saini mkataba mara tu tuliporudi mjini kwetu. Walifurahi kusikia hivyo na wakaanza kutuuliza kuhusu nyumba hiyo. Tulianza kuwaeleza kuhusu Ufalme na jinsi maisha yetu yalivyokuwa yamebadilika. Tulishiriki jinsi tulivyolipia ekari zetu 55 pesa taslimu na jinsi tulivyokuwa na shauku ya kutoka kwenye nyumba ile nzee ya mashambani.

Tulitaja kwamba tulikuwa na mipango halisi, nao wakatuuliza ikiwa wangeweza kuiona, na bila shaka, tulifurahi kupata maoni yao. Kwa hivyo tuliweka mipango yetu kwenye meza yao ya jikoni na tukaketi kuijadili. Baada ya muda usio mrefu mke wa baba huyo alianza kusema mambo kama, “La, eneo hili ni dogo sana,” au “mnahitaji jiko kubwa zaidi,” au “mmefikiria nini kuhusu nyumba hii watoto wenu watakapokuwa wakubwa? Nyinyi kama wachungaji, mnahitaji sana eneo kubwa la burudani.” Kimsingi, walituonyesha kwa nini hatukufaa kujenga nyumba aina hiyo, na ilibidi tukubaliane na kila hoja waliyotoa. “Sawa, tunawezaje kujenga nyumba kubwa zaidi na pesa tulizo nazo?” “Hilo ni jambo rahisi,” wakasema. “Jengeni nyinyi wenyewe!” Niliposikia maneno hayo, karibu nicheke. “Mimi nijenge nyumba yangu mwenyewe?” Kama nilivyosema awali, sikujua chochote kuhusu ujenzi wa nyumba! Lakini walianza kututia moyo, wakisema haikuwa kazi ngumu. Walituambia kuhusu kitabu kiitwacho, *Save up to \$50,000 or more as your own General Contractor: How to Plan, Subcontract and Build Your Dream House* by Warren V. Jaeger. (Okoa hadi \$50,000 au zaidi kama Mkandarasi Mkuu wa Nyumba Yako: Jinsi ya Kupanga, Kuajiri mkandarasi msaidizi na Kujenga Nyumba ya Ndoto Yako na Warren V. Jaeger.)

Kwa hivyo tuliporudi nyumbani, tuliamua kutotia saini mkataba wa kujenga nyumba hiyo ya mbao. Tuliagiza kitabu walichokipendekeza na tukakisoma, huku tukitafakari kila sura. Tulianza kuchunguza mipango ya nyumba za kawaida pia. Hatimaye, tulipata mpango wa nyumba ambao tulioupenda na tukaanza kuugawanya hatua kwa hatua. Tulizungumza na marafiki na watu ambao tulijua walikuwa wamejenga nyumba pia. Hatimaye, tuliamua kufuata njia hiyo! Tuliangalia mipango ya ujenzi na kujiuliza, “Tunaweza kufanya nini sisi wenyewe ili kuingiza nyumba hii katika bajeti yetu?” Ajabu, niliamua kuunganisha nyaya za umeme kwa nyumba nzima, ingawa sikuwa nimewahi kushika uzi wa waya maishani mwangu. Rafiki ambaye alielewa kazi hii aliniambia ni rahisi na angenionyesha jinsi ya

kufanya hivyo.

Kwa sababu nilikuwa na shughuli nyingi katika biashara yangu, Drenda aliamua kuwa mkandarasi mkuu ambaye angefanya kazi na wakandarasi wadogo. Tulitafuta mkandarasi msaidizi wa kututengenezea fremu ya ndani ya nyumba, na mengine yote yalikuwa juu yetu. Kilichofuata ni baadhi ya siku zenye kazi nzito lakini za kusisimua maishani mwetu. Ili kufupisha hadithi ndefu, tulikamilisha nyumba yetu ikiwa na miraba mara mbili zaidi ya ule mpango wa awali. Tulikuwa na milango imara ya mbao; sakafu ngumu ya mbao; mapambo imara ya mbao ya kufunika sehemu ambayo kuta na dari zinakutana; na jikoni letu lilijaa makabati ya kupendeza na maalum, na vifaa vipya vya chuma cha pua. Tuligundua kwamba tuliokoa zaidi ya \$200,000 kwa kujijengea nyumba sisi wenyewe!

Leo, nina furaha sana kwamba tulimwomba Roho Mtakatifu atupatie mpango. Matokeo yalikuwa ya kiwango cha juu sana kuliko chochote ambacho tungeweza kuota peke yetu. Bado ninastaajabu jinsi Mungu alivyopanga safari hiyo hadi Virginia na kutuweka pamoja na wenzi hao ambao walikuwa wamemaliza kujenga nyumba yao wenyewe. Nina uhakika kama hilo halingefanyika, labda tungejenga nyumba ya mbao. Sisemi kwamba nyumba ya mbao haingetufaa kwa muda, lakini baada muda mfupi haingetutosha. Nyumba tuliyojenga bado ni ushuhuda kwangu wa mfano wa jinsi Roho Mtakatifu atakavyokusaidia katika kila hali, huku akikupa mpango na mwelekeo utakaopita matarajio yako!

Kwa hivyo hebu niseme mara moja tena...

### **Mungu ana mpango WAKO!**

Lakini labda unaweza kusema, “Gary, haya yote ni mazuri, lakini Mathayo 13:44 inasema mpango huo umefichwa!” Ndio, ni hivyo, na hilo ni kwa faida yako. Angalia kile Yesu anachosema katika Mathayo 13:10-11.

*Wakaja wanafunzi, wakamwambia, “Kwa nini wasema nao kwa mifano?” Akajibu, akawaambia, “**Ninyi mmejaliwa** kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakujaliwa.”*

—Mathayo 13:10-11

Ufahamu huu wa siri ni kwa ajili yako na sio kwa shetani au watu waovu ambao wangeutumia vibaya au kuzuia mipango ya Mungu. Biblia inasema kwamba Shetani atabadili mbinu akigundua yale ambayo Mungu anafanya.

**KILA MARA MIMI HUSEMA  
KWAMBA SIRI ZA MUNGU  
ZIMEFICHWA KWA AJILI  
YAKO, SIO KUTOKA KWAKO!  
SHETANI ANAISHI GIZANI  
WALA HAJUI MIPANGO  
YA MUNGU.**

*Bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu; ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangaliijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu.*

—1 Wakorintho 2:7-8

Kila mara mimi husema kwamba siri za Mungu zimefichwa kwa ajili yako, sio kutoka kwako! Shetani anaishi gizani wala hajui mipango ya Mungu. Yeye huwa dhihi ya yale ambayo Mungu anafanya tayari. Huwa amechelewa sana anapogundua yale yanayotokea! Kwa hiyo wakati mwingine unapohisi woga kidogo muda unapoyoyoma na bado huna jibu lako, jua kwamba Mungu hachelewi, na kile unachofikiri kinachelewa kinakufanyia kazi kwa kuficha jibu mpaka wakati wa kufichuliwa utakapofika.

*Tena ufalme wa mbinguni umefanana na hazina **ILIOSITIRIKA** katika shamba; ambayo mtu alipoiona, **aliificha**; na kwa furaha yake akaenda akauza alivyo navyo vyote, akalininua shamba lile.*

—Mathayo 13:44

Tumejadili shamba ni nini na mahali lilipo na kwa nini hazina imefichwa. Pia tumejadili jinsi ya kusikia kutoka kwa Ufalme wa Mungu siri hizo zilizofichwa kwa kuomba katika Roho na kusikiliza sauti ya Roho Mtakatifu. Lakini kuna kanuni nyingine muhimu katika mchakato huu iliyoorodheshwa katika Maandiko yetu ambayo unapaswa kujua. Kutoizingatia kumesababisha kutofaulu kwa mipango mingi mizuri na kuleta uharibifu mkubwa katika maisha ya watu. Ikiwa uliona katika Maandiko yetu, mara mtu anaposikia kuhusu hazina, wazo, mwelekeo, au mpango kutoka kwa Mungu, anauficha tena. HUCHUKUI HATUA papo hapo! Haanzi kuwaambia marafiki na majirani zake wote kuhusu yale ambayo amesikia kutoka kwa Bwana au mipango yake mipya na ya kuisisimua. Biblia inasema kwamba aliificha tena, akaenda akauza mali yake yote, kisha akanunua shamba hilo. Kwa maneno rahisi, hataki kufunua eneo la hazina hiyo kwa mtu mwingine yeyote hadi atakapoimiliki. Kwa kungoja

hadi aimiliki, ana hakikisho kwamba hakuna mtu anayeweza kumwibia.

Maandiko pia yanafunua kwamba anapopata hazina hiyo kwa mara ya kwanza, kwa kweli hana uwezo wa kuilipia hazina hiyo na lazima apitie mchakato wa kujiandaa ili kuweza kuinunua. Kanuni hii inapita pesa na uwezo wa kununua kitu. Inatufundisha kanuni muhimu ya maisha na jinsi unavyopaswa kufanya inapohusu yale ambayo Roho Mtakatifu anakuonyesha ikiwa unataka kufanikiwa.

Maandiko yanasema kwamba mara tu unaposikia wazo au mwelekeo, haupaswi kuchukua hatua hadi utakapokuwa na uwezo. Nafikiri sote tunaweza kuona jinsi jambo hili linavyofanya kazi inapohusu pesa. Ikiwa huna pesa za kutosha kumiliki shamba hilo, hakika hupaswi kumwambia mtu kwamba kuna hazina juu yake. Neno likitoka kwamba kuna hazina juu yake, unaweza kuwa na uhakika kwamba mtu mwingine atalinunua kabla yako. Badala yake, nenda ufanye kila uwezalo ili upate pesa za kulinunua, huku ukijiweka ukweli kuhusu hazina iliyofichwa humo.

Kanuni hii hii ni kweli kwa kila mwelekeo au maagizo ambayo Mungu anakupa. Mara nyingi, Wakristo hukosea mwanzo hadi mwisho. Mara nyingi, Roho Mtakatifu hutufunulia wazo, sio kwamba tuanze kulitekeleza wakati huo bali ili tujiandae kunyakua fursa hiyo. Awamu ya maandalizi ya jitihada yoyote ni sehemu muhimu zaidi katika mchakato. Katika michezo, ushindi au kushindwa huja kadri ya jinsi timu zilivyojiandaa wakati wa mazoezi, wakati hakukuwa na watazamaji. Lakini utakubali kwamba mazoezi hayafurahishi; ni mazito na yanachosha. Lakini kila mtu anapenda msisimko wa mchezo, umati wa watu, taa, na furaha ya ushindi.

Cha kusikitisha ni kwamba, ndoto hizi hugeuka na kuwa maumivu na huzuni ikiwa maandalizi hayajazingatiwa. Siwezi kukuambia ni watu wangapi ambao nimewaona wakiharibu maisha yao kwa kutojua kanuni hii. Nimeona watu walioitwa na Mungu kweli, watu waliopakwa mafuta, wakizindua na kuanzisha kanisa wakati hawajajiandaa kihisia au kifedha, na kuishia na maafa badala ya ndoto waliyoiwazia. Nimeona watu ambao walimsikia Mungu akiwapa wazo la biashara, na, wakiwa na uhakika wa kufaulu, wakaacha kazi zao bila uangalifu unaostahili au maandalizi na hatimaye wakafilisika. Sehemu ya kuhuzunisha ya hadithi hizi ni kwamba Mungu hulaumiwa, na watu wanaohusika hukatishwa tamaa kujihusu na Mungu pia. Sina hakika kwa nini watu wengi hufikiri mafanikio huja mara moja. Lakini watu lazima wafundishwe taratibu za mafanikio zilizo katika Andiko hili rahisi.

Watu huja kwangu na kusema, “Habari Mchungaji, Mungu aliniambia

kwamba hili ndilo kanisa langu.” Kisha siwaoni tena. “Habari Mchungaji, Mungu alinipa wazo kubwa la biashara.” Punde si punde ninasikia kwamba nyumba yao imeorodheshwa kuuzwa na wamenyang’anywa gari lao. Mungu HANA mambo kama haya kwa ajili yako.

Tunaposikia wazo kutoka kwa Roho Mtakatifu, haimaanishi kwamba tunapaswa kulifanyia kazi wakati huo. Mara nyingi, anatuongoza tufiche ndoto hiyo na kujiandaa kuinyakua. Kwa kawaida, huwa hatuna yote tunayohitaji ili kufaulu katika kumiliki maono hayo. Maandalizi yanaweza kuchukua wiki moja au hata miaka kulingana na kile ambacho Mungu amekuonyesha ufanye. Lazima uelewe kwamba maandalizi na wakati mwafaka ni muhimu au hata muhimu zaidi kuliko wazo lenyewe!

Najua kwangu, niliitwa kuhubiri Injili nilipokuwa na umri wa miaka 19. Nilipata maono wazi ambapo nilijiona nimeshika Biblia na Bwana akisema, “Ninakuita ulihubiri Neno Langu” mara tatu. Lilikuwa tukio halisi na la nguvu kweli. Lakini Bwana hakuniambia nianze kuhubiri wakati huo. Badala yake, aliniambia niende chuo kikuu. Wajua, kimsingi niliacha shule ya upili na wastani wa 1.3. Pia nilikuwa mwenye haya sana na niliepuka kuwa karibu na watu. Acha niwe wazi kabisa. Sikuwa na ukomavu unaohitajika kuwachunga watu hata kidogo! Kwa hiyo nilienda chuo kikuu, na masomo yalikuwa magumu, magumu sana—lakini nilivumilia na nikamaliza shahada yangu ya miaka minne.

Mara baada ya kutoka chuo kikuu, nilijiuliza ikiwa wakati wa kuhubiri ulikuwa umefika. Lakini Bwana aliniambia alitaka nifanye kazi na kampuni ya kifedha iliyouza bima na dhamana. Ingawa hilo halikuwa na maana kwangu, nilijua ni sauti ya Mungu niliyokuwa nimesikia, na nilichukua kazi hiyo. Ilikuwa ngumu zaidi kuliko chuo kikuu. Ilinibidi kupiga simu bila furaha kila siku hadi nikajifunza kushinda woga wangu wa watu. Kuishi maisha ya kulipwa kamisheni pia lilikuwa jambo gumu, na, kwa kweli, nilitaka kujiuzulu kila siku, lakini nilijua haingefaa nifanye hivyo. Hatimaye, baada ya miaka michache, nilielewa vyema kile nilichokuwa nikifanya. Ofisi yangu na Drenda ilichukua nafasi ya kwanza kati ya ofisi 5,000 kote nchini katika kampuni hiyo.

Ilikuwa wakati huo ambapo Mungu aliniambia kwamba sasa nilikuwa tayari kuzindua kanisa. Nilikuwa nimefika umri wa miaka 40 wakati huo. Mungu alichukua miaka 21 kunitayarisha kwa ajili ya maono aliyonipa nilipokuwa na umri wa miaka 19. Mara tu nilipoanza kazi ya uchungaji, nilielewa kwa nini maandalizi mengi sana yalihatijika. Kazi ya uchungaji ilikuwa ngumu kuliko nilivyofikiri. Lakini kwa sababu ya mafunzo yangu

juu ya watu na kupitia kukataliwa katika biashara, niliweza kuwa mwaminifu kwa wito wa Mungu maishani mwangu. Kila mwito hautachukua miaka 21 ya kujiandaa, lakini kanuni ya maandalizi ni ileile.

Kwa sababu ya kanuni hii ya maandalizi, napenda kufafanua Mathayo 13:44 kama ifuatavyo:

*Ufalme wa mbinguni ndani yako hukupa maarifa au upatikanaji wa maarifa ya siri, au mambo yaliyofichika ambayo Mungu anayajua. Ujuzi huu unapatikana kutoka kwa Roho wa Mungu, Mwenyewe aliye ndani yako. Mwanadamu anapopata au kusikia maarifa hayo ya siri ambayo ni hazina na jibu kwake, yeye huyaficha tena moyoni na akilini mwake. Kisha katika furaha yake yeye huenda kwa nguvu zake zote kufuatilia, kwa maandalizi makini, mwelekeo na maelekezo yaliyofunuliwa kwake, na hivyo kushika na kunyakua jibu lake.*



## SURA YA 8

# MAHALI PAGUMU PA KUPANDISHWA CHEO

Rafiki yangu Mchungaji Peter na mkewe, Bev, ambao wanachunga kanisa kubwa huko New Zealand, walikuwa na ziara fupi hapa Marekani. Ulikuwa msimu wa Krismasi, na walipanga kukaa Colorado Springs kwenye hoteli inayoitwa Broadmoor kwa siku kadhaa ili kupumzika na kufurahia mandhari ya Krismasi. Ikiwa hujatembelea Broadmoor, ni mojawapo ya vituo bora vya mapumziko vya Amerika na iko mbele ya milima inayoitwa Rocky; na inajulikana kuwa na mapambo ya kifahari ya Krismasi. Mchungaji Peter alitupigia simu kutufahamisha kwamba wangukuwa pale na wakatuuliza ikiwa tungetaka kujiunga nao. Tulichukua fursa hiyo na tukawa na siku tatu za kupendeza sana huko.

Wakati wowote ninapokuwa na Mchungaji Peter, huwa tunatumia muda mwingi kuzungumza kuhusu huduma maana yuko kwenye bodi yangu. Tulizungumza kuhusu mipango yetu ya mwaka uliokuwa ukija na tukabadilishana mawazo. Hatimaye, wakati wa kuagana ulifika, jambo ambalo sikuzote huwa linahuzunisha maana wao ni marafiki wapendwa. Drenda na mimi huwatembelea huko New Zealand mara moja kwa mwaka, au angalau baada ya mwaka mmoja, lakini mwaka huo, tayari nilikuwa na shughuli nyingi na sikuwa na mpango wa kufanya hivyo.

Kwa hivyo tulifika nyumbani tayari kuukabili mwaka mpya kwa hamu kubwa. Ajabu ni kwamba, mnamo Januari 9, niliota ndoto ambayo niliambiwa kwamba Mchungaji Peter angenialika kuhubiri kanisani kwake mnamo Februari. Nakumbuka nilifikiri hilo halingewezekana maana

nilikuwa pamoja naye siku tatu hivi karibuni, wala hakuwa ametaja jambo hilo, na Februari ilikuwa imesalia wiki chache tu. Nilimwambia Drenda kile ambacho Bwana aliniambia nilipokuwa nikielekea jikoni kula kifungua kinywa.

Niliwasha kompyuta yangu ambayo ilikuwa juu ya meza ya jikoni. Nikiwa ninakunywa kikombe cha kahawa, niliona barua pepe kutoka kwa Mchungaji Peter ikiingia. Nilipoifungua nilishangaa kuona kwamba Mchungaji Peter alikuwa akinikaribisha kuhubiri kwenye mkutano wake wa kifedha wa kila mwaka, ambao ungefanyika baada ya wiki tatu tangu wakati huo. Bila shaka nilishangaa, lakini kwa sababu ya ile ndoto sikushtuka. Nilitazama kwa haraka ratiba yangu ili kuona kama hilo lingewezekana maana nilikuwa na safari nyingi mwezi huo karibu wakati ulerule ambao Peter alikuwa amenialika niwe New Zealand. Mimi na Drenda tayari tulikuwa na mpango wa kusafiri kwa ndege hadi Buenos Aries, nchini Argentina, siku chache kabla ya kwenda Auckland, nchini New Zealand. Njia pekee ambayo ningeweza kufikia mkutano huo ilikuwa kuondoka mara tu baada ya mkutano wa Buenos Aries na kusafiri kwa ndege moja kwa moja hadi Sydney, Australia, kisha kupanda ndege nyingine hadi Auckland. Kwa kawaida singepanga safari kama hiyo, lakini kwa sababu Bwana alikuwa amenena nami, nilijua kwamba tulipaswa kwenda.

Safari yetu nchini Ajentina ilifadhiliwa na mmoja wa wachuuzi wangu ambaye kampuni yangu inafanya biashara naye. Tulikuwa na wakati mzuri wa kupatana na marafiki wengine ambao kwa kawaida huwa tunaonana mara moja kwa mwaka au zaidi. Ajentina wakati huo ilikuwa ikikabiliana na masuala mazito ya kifedha, na kulikuwa na ghasia fulani katika jiji hilo, lakini kwa ujumla, ilikuwa safari nzuri kwa sababu sikuwa nimewahi kwenda huko awali. Safari yetu ya ndege hadi Sydney ilikuwa ya masaa 16 angani, safari ndefu zaidi ya ndege ambayo nimewahi kuchukua. Ilijumuisha kupaa juu ya Ncha ya Kusini, jambo ambalo nilifikiri lilikuwa la kustaaajabisha maana nilitarajia kuona sehemu hiyo ya ulimwengu kutoka angani.

Wakati wa safari yetu ya ndege, nikitazama barafu na theluji tupu chini yetu nje ya dirisha, niligundua kwamba hiyo ilikuwa ndege ya shirika la ndege la Ajentina, shirika la ndege ambalo pia lilikuwa na matatizo ya kifedha katika nchi ambayo ilikuwa ikijitahidi kujidumisha kifedha. Wazo lilinjia kwa sekunde moja kwamba ikiwa kampuni hii ilikuwa imetumia njia za mkato kukarabati mandege yake na hilo litufanye tuanguke katika sehemu hiyo ya ulimwengu, hiyo haingekuwa picha nzuri. Lakini nilijua nilikuwa katika mikono salama sana naana Bwana, Mwenyewe alikuwa

**“KWA KUWA WOTE  
WANAOONGOZWA NA ROHO  
WA MUNGU, HAO NDIO  
WANA WA MUNGU.”  
—WARUMI 8:14**

amenielekeza nichukue safiri hiyo.

Tulipofika Sydney, tulipiga simu haraka kwa Mchungaji Peter na Bev, na tukashtuka kusikia kuwa Mchungaji Peter alikuwa hospitalini kwa sababu alikuwa amepigwa na mshtuko mkubwa wa moyo. Hangeweza kuhubiri hata kidogo na akaniomba kama ningeweza

kufundisha katika kongamano lake zima la kifedha. Sasa nilijua kwa nini Bwana alikuwa amenielekeza kuja New Zealand, na nilishangaa jinsi Roho Mtakatifu alivyoelekeza hatua zetu. Hii ni kumbukumbu kubwa ya kile ambacho Warumi 8:14 inasema.

*“Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.” (Warumi 8:14)*

Tena, tunazungumzia kuwa na uwezo wa kusikia mwelekeo, mawazo, na dhana kutoka kwa Roho Mtakatifu. Hakuna hadithi bora zaidi katika Biblia inayoeleza somo langu linalofuata la jinsi kusikia Roho Mtakatifu kunavyoweza kukupa majibu unayohitaji kuliko hadithi ya Danieli. Hebu tufuate hadithi hii kwa kuanza katika Danieli 2:1–6.

*Hata katika mwaka wa pili wa kumiliki kwake Nebukadreza, Nebukadreza aliota ndoto; na roho yake ikafadhaika, usingizi wake ukamwacha. Ndipo mfalme akatoa amri kuwaita waganga, na wachawi, na wasihiri, na Wakaldayo, wapate kumweleza mfalme ndoto zake. Basi wakaingia, wakasimama mbele ya mfalme. Mfalme akawaambia, “Nimeota ndoto, na roho yangu imefadhaika hata niijue tafsiri yake.”*

*Ndipo hao Wakaldayo wakamwambia mfalme, kwa lugha ya Kiaramu, “Ee Mfalme, uishi milele; tuambie sisi watumishi wako ile ndoto, nasi tutakuonyesha tafsiri yake.”*

*Mfalme akajibu, akawaambia Wakaldayo, “Neno lenyewe limeniondoka; msiponijulisha ile ndoto na tafsiri yake, mtakatwa vipande vipande, na nyumba zenu zitafanywa jaa. Bali kama mkinionyesha ile ndoto na tafsiri yake, nitawapa zawadi na thawabu*

*na heshima nyingi; basi nionyeshe ni ile ndoto na tafsiri yake.”*

—Danieli 2:1-6

*Wakaldayo wakajibu mbele ya mfalme, wakasema, “Hapana mtu duniani awezaye kulionyesha neno hili la mfalme; kwa maana hapana mfalme, wala bwana, wala liwali, aliyetaka neno kama hili kwa mganga, wala kwa mchawi, wala kwa Mkaldayo. Ni neno la ajabu, hili analolitaka mfalme, wala hapana mwingine awezaye kumwonyesha mfalme neno hilo, ila miungu, wasio na kikao pamoja na wenye mwili.”*

*Basi kwa hiyo mfalme akaghadhibika sana, akaona hasira nyingi, akatoa amri kuwaangamiza wenye hekima wote wa Babeli. Basi ile amri ikatangazwa, na hao wenye hekima walikuwa karibu na kuuawa; watu wakamtafuta Danieli na wenzake ili wauawe.*

—Danieli 2:10-13

*Ndipo Danieli akaenda nyumbani kwake, akawapasha habari kina Hanania, na Mishaeli, na Azaria wenzake; ili waombe rehema kwa Mungu wa mbinguni kwa habari ya siri hiyo, ili kwamba Danieli na wenzake wasiangamizwe pamoja na wenye hekima wa Babeli. Ndipo Danieli alipofunuliwa siri hiyo katika njozi ya usiku. Basi Danieli akamhimidi Mungu wa mbinguni. Danieli akajibu, akasema, “Na libimidiwe jina la Mungu milele na milele; kwa kuwa hekima na uweza ni Wake. Yeye hubadili majira na nyakati; huuzulu wafalme na kuwamilikisha wafalme; huwapa hekima wenye hekima; huwapa wenye ufahamu maarifa; **Yeye hufunua mambo ya fumbo na ya siri; buyajua yaliyo gizani, na nuru hukaa Kwake.**”*

—Danieli 2:17-22

Danieli alikuwa katika hatari ya maisha na kifo, mahali pa mauti. Lakini hapa kuna jambo muhimu kuhusu kupandishwa cheo kwako kunakofuata. Mungu alitumia tukio hili kumpandisha cheo, wala si kumwangusha. Danieli aliweza, kwa ujuzi wa siri wa Roho Mtakatifu, kumpa Mfalme Nebukadreza ndoto na tafsiri. Mfalme alisisimka, kama tunavyoona katika kifungu kifuatacho.

*Ndipo Nebukadreza, mfalme, akaanguka kifudifudi, akamsujudia Danieli, akatoa amri wamtotee Danieli sadaka na uvumba. Mfalme akajibu, akamwambia Danieli, “Hakika Mungu wenu ndiye Mungu wa miungu, na Bwana wa wafalme, awezaye kufumbua siri, kwa kuwa wewe uliweza kuifumbua siri hii.”*

***Basi mfalme akamtukuza Danieli, akampa zawadi kubwa nyingi sana, akamfanya kuwa mkubwa juu ya uliwali wote wa Babeli, na kuwa liwali mkuu juu ya wote wenye hekima wa Babeli. Tena, Danieli akamwomba mfalme, naye akawaweka Shadraka, na Meshaki, na Abednego, wawe juu ya mambo yote ya uliwali wa Babeli; lakini huyo Danieli alikuwa akiketi katika lango la mfalme.***

—Danieli 2:46-49

Matokeo ya Danieli kuweza kusikia sauti ya Mungu yalikuwa yapi? Kupandishwa cheo na utajiri!

Tunapata matokeo sawa na haya katika hadithi nyingine kwa Biblia, hadithi ya Yusufu. Alikuwa katika hali kama hiyo, ambapo alipewa fursa ya kufasiri ndoto ya Farao. Baada ya kufaulu kufasiri ndoto na kisha pia kutoa mpango wa usimamizi wa kuokoa Misri kutokana na ukame uliokuwa ukija jinsi ndoto ilivyokuwa imefunua, tunapata jibu la Farao katika Mwanzo 41:39–40.

*Farao akamwambia Yusufu, “Kwa kuwa Mungu amekufahamisha hayo yote, hapana mwenye akili na hekima kama wewe. Basi wewe utakuwa juu ya nyumba yangu, na kwa neno lako watu wangu watatawaliwa. Katika kiti cha enzi tu nitakuwa mkuu kuliko wewe.”*

—Mwanzo 41:39-40

Katika hadithi hizi zote mbili, ukosefu wa tumaini ulikuwa jaribu halisi mwanzoni, lakini mwishowe matokeo yalikuwa kupandishwa cheo na utajiri. Kwa maneno rahisi, ulimwengu huwalipa pesa nyingi watu wanaotatua matatizo makubwa. Roho Mtakatifu ndani yetu hupenda kutuweka katikati ya matatizo makubwa! Usianze kuogopa hilo linapotokea, bali anza kumsifu Bwana, kwani atakusaidia kama alivyowasaidia Danieli na Yusufu! Wakati wote mimi husema kwamba Mungu hupata utukufu, na

mimi hupata malipo! Napenda kile Danieli alichosema kumhusu Bwana, **“Yeye hufunua mambo ya fumbo na ya siri; huyajua yaliyo gizani, na nuru hukaa Kwake.”** Danieli alisema kwamba nuru hukaa Kwake. Hiyo inamaanisha, ikiwa unatembea nje gizani, unapowasha taa, unaweza kuona unakoenda! Hofu inashindwa na nuru na unaona mahali pa kukanyaga unapotembea. Paulo anadokeza katika mstari huu kwamba Mungu hunena nasi na kutusaidia katika wakati wetu wa taabu.

*Mwajua ya kuwa mlipokuwa watu wa Mataifa,  
mlichukuliwa kufuata sanamu zisizonena, kama mlivyoongozwa.  
(1 Wakorintho 12:2)*

Paulo anasema kwamba sanamu hazineni, bali Mungu ndiye hunena!

Sasa, labda unashangaa kwa nini niliita sura hii “Mahali Pagumu pa Kupandishwa Cheo.” Ni kwa sababu ni katika mahali pagumu ambapo Roho Mtakatifu ndani yako huleta majibu. Ni mahali pagumu panapokupa fursa nzuri ya kupata suluhu. Mahali pagumu ni usanidi mzuri wa kupandishwa cheo kwako! Cha kusikitisha ni kwamba, waumini wengi huepuka maeneo magumu. Wengi hufikiri kwamba wanapojikuta katika hali ngumu, wamemkosa Mungu.

Nakumbuka tulipoanza huduma ya televisheni, na bili zilikuwa karibu \$9,000 kwa mwezi. Doh! Nilifikiri hizo zilikuwa pesa nyingi sana kutumika kila mwezi, kisha zikafika zaidi ya \$20,000, halafu \$50,000. Siku moja, sote tulikuwa katika maombi, Amy, binti yangu, alianza kunena kupitia kwa karama ya unabii:

“Mavuno ni makubwa mno kwako. Ninakunyoosha. Ni kupitia kwa Roho Wangu pekee utaweza kuelewa kile kinachokaribia kutokea! Je, utapiga hatua kwenda mbele kwa kuniruhusu nikupitisha katika mambo magumu, na yasiyowezekana kupita ufahamu wako?”

Kabla sijakusimulia hadithi, kulingana na kile unachojua sasa, unaweza kuniambia maana ya swali hilo? KUPANDISHWA CHEO! Napenda kwamba Mungu aliniruhusu nichague. Alikuwa anauliza kama nilikuwa tayari kwenda umbali wote pamoja Naye. Alikuwa akitaka nikubali kwanza. Ikiwa ningekataa, nina uhakika angeenda kwa mtu mwingine. Lakini ningependelea kupandishwa cheo, sivyo?

Naam, nikasema, “Ndio, Bwana, unajua nitafanya hivyo.” Wiki chache baada ya hapo, mtandao wa Daystar ulitupa nafasi ya kila siku ilhali hapo awali tulikuwa tukifanya kipindi kimoja kila wiki. Kuchukua fursa hiyo

kungemaanisha bili zetu za televisheni zingeongezeka hadi karibu \$200,000 kila mwezi. Basi kwa kuzingatia neno lile la kinabii na kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu ndani yangu, nilikubali. Baada ya kuanza kufanya vipindi kila siku kila mtu aliniambia kwamba kwa miezi kadhaa tungechelewa kulipa bili zetu hadi watu wavizoe. Hilo ndilo lililotokea, lakini labda hata zaidi ya jinsi sisi sote tulivyotarajia. Katika miezi mitano, sikuwa nimelipa bili yetu ya televisheni ya \$500,000. Aliyetupa fursa ya kupeperusha vipindi vyetu alinitumia barua pepe ikisema kwamba mawakili wake walikuwa wakipata wasiwasi juu ya kuchelewa kwa malipo yetu.

Nilianza mapambano mengi na Mungu kuhusu hili maana kipindi chetu kinaitwa *Fixing the Money Thing!* (Kusuluhisha Suala la Fedha!) Nilianza kukata tamaa kidogo na kumwambia Drenda kuwa huenda nikahitaji kupunguza vipindi. Lakini akajibu, “Mungu alisema nini? Alisema atalipa, sivyo?” Kwa siku kadhaa, ndivyo tu alivyosema wakati wowote nilipozungumza naye kuhusu jambo hilo. Tulisali, na ingawa sikuwa na jibu lolote wakati huo, nilihisi amani ya Mungu. Wiki hiyo, niliota ndoto ambapo niliona rundo la hundi. Jambo la kushangaza katika ndoto hiyo sio tu kwamba niliona rundo la hundi lakini pia niliona kiasi cha pesa zilizokuwa zimeandikwa kwenye hundi hizo na majina ya wale walioziandika. Nilipoamka nilijua kwamba bili za vipindi vya televisheni zilikuwa zimelipwa, kisha nikapata amani. Naam, wikendi hiyo, ambayo ilikuwa ya kawaida tu, tulipata \$500,000 kama vile ndoto ilivyoniyesha. Kiasi nilichoona na majina ya wale walioandika hundi hizo vyote vilikuwepo.

Tazama, maeneo magumu sio jambo baya! Ni mahali pa kupandishwa cheo, rafiki yangu. Watu huniambia kwamba wanahofu kuingia katika maeneo magumu kwa sababu wanaogopa kufanya makosa. Lakini Roho Mtakatifu ana uwezo wa kukuonya kuhusu kosa linaloweza kutokea ikiwa utamsikiliza.

Nakumbuka, nilipokuwa na kampuni yangu ya rehani miaka michache iliyopita, mteja wangu alitaka kukopa fedha za kuendeleza nyumba yake ili kuziwekeza katika kampuni ambayo sikuhihi vyema kuihusu. Nakumbuka nilipokuwa nikipanda ngazi kwenye ofisi yangu, mmoja wa wawakilishi wangu aliniarifu kuhusu jambo hilo. Ghafila, nilihisi Roho Mtakatifu akiniambia cha kufanya. Nilimwambia mwakilishi wangu, “Unaweza kuendelea na mpango huo, lakini mwambie mteja atie sahihi barua itakayoambatana na mkopo huo, ambayo itasema hatuna uhusiano na kampuni hiyo ya uwekezaji bali tunatoa mkopo tu kwa ombi la mteja.” Tulisema zaidi kwamba hatukuwa na jukumu lolote kuhusu usalama au utendakazi wa uwekezaji huo, wala

kupendekeza mteja awekeze katika kampuni hiyo. Naam, baada ya takiban miezi sita, kila kitu kilienda mrama. Kampuni ya uwekezaji ilipoteza pesa zote za mteja huyo. Kesi ilifunguliwa dhidi ya kampuni ya uwekezaji na kampuni yangu pia. Hata hivyo, wakili wao alipoona barua ambayo mteja wetu alikuwa ametia saini, tuliondolewa kwenye shtaka hilo.

Roho Mtakatifu ndiye aliyenimamisha siku ile kwenye ngazi na kuniamuru nimwambie mwakilishi wangu aiweke barua hiyo kwenye mkopo huo. Unaweza kumwamini Roho Mtakatifu akusaidie na kukuongoza katika kila hali. Kama vile Yesu alivyosema, “Usiogope.”

Nimesimulia hadithi hii katika mojawapo ya vitabu vyangu vingine, lakini inafaa niurudie katika mjadala huu. Wikendi moja, familia yetu ilikuwa ikisafiri kwenda kwa mapumziko ya siku tatu. Kila mtu alikuwa ndani ya gari, na nilipoenda kuwasha injini, ghafla, Roho Mtakatifu alisema nisogeze gari langu. Magari yetu mengine mawili yalikuwa kwenye kijibarabara chetu. Kisha Roho Mtakatifu akasema nisogeze moja ya magari hayo hadi kwenye nyasi. Hilo lilikuwa jambo la ajabu sana. Nikawaza, “Mbona Roho Mtakatifu ananiambia nifanye hivi?” Sikuelewa. Lakini nilikuwa na hisia yenye nguvu zaidi! Basi nilimweleza Drenda kile nilichotaka kufanya, kisha nikatoka nje na kulisogeza gari hilo moja kutoka kwa kijibarabara chetu na kulipeleka uani kwenye nyasi. Sikufikiria sana hadi tuliporudi nyumbani Jumapili jioni. Mahali gari lile langu lilikuwa awali sasa palikuwa na mti mkubwa wa michongoma uliokuwa umeanguka pale. Gari nililokuwa nimesogeza kwa nyasi lilikuwa sawa kabisa maana mti haukuliangukia. Kama singelizogeza, lingepondwa-pondwa kabisa.

Mimi na Drenda, bila shaka, tulikuwa mfano wa picha ya kile cha kutofanya na pesa. Lakini tulichohitaji ni mikakati michache ya siri na hekima ya siri ya kutuweka juu ya hali zetu. Sasa, sina budi kutabasamu maana kipindi chetu cha televisheni, kinachoonekana kote ulimwenguni, kinaitwa *Fixing the Money Thing!* (Kusuluhisha Suala la Fedha!)

Rafiki yangu, hatima yako leo ndiyo hii.

*“Walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaiifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni.”* (Waebrania 11:34b)

Maeneo magumu na yasiyowezekana sio magumu na kutowezekana wakati unajua jibu!



## SURA YA 9

# SAUTI NDOGO, TULIVU

Ninapoanza kufundisha kuhusu sauti ya Roho Mtakatifu, watu wengi huniambia kwamba hawajawahi kusikia sauti ya Mungu. Lakini mimi huwaambia kila mara, “Ndio, umewahi!” Ikiwa unahisi hivyo kama watu wengi, kwamba hujawahi kusikia sauti ya Mungu, basi tafadhali rejea 1 Wafalme 19:11–12.

*Akasema, “Toka, usimame mlimani mbele za Bwana. Na tazama, Bwana atapita.”*

*Upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima, ukaivunja-vunja miamba mbele za Bwana; lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule; na baada ya upepo, tetemeko la nchi; lakini Bwana hakuwamo katika lile tetemeko la nchi; na baada ya tetemeko la nchi kukawa na moto; lakini Bwana hakuwamo katika moto ule; na baada ya moto sauti ndogo, ya utulivu.*

—1 Wafalme 19:11–12

Ingawa nimesikia sauti ya Roho Mtakatifu katika viwango tofauti vya nguvu, sauti ya kawaida ya Roho Mtakatifu hunong’ona kwa upole. Ni sauti ndogo, tulivu. Kama nilivyosema awali, kwa kawaida, sauti ya Mungu husikika kama wazo lenye sauti tofauti. Kama vile unavyoweza kutambua sauti ya mtoto wako katika umati, unanza kumjua Roho Mtakatifu vya kutosha kiasi cha kujua sauti Yake anaponena pia. Lakini katika sura hii nataka kuzungumza nawe kuhusu sauti ya Mungu ambayo watu wote wameisikia bila kufikiri ni sauti ya Mungu.

Nilipokuwa chuoni katika Chuo Kikuu cha Oral Roberts, nilisoma

mafundisho kadhaa yaa theolojia maani somo langu kuu lilikuwa Agano la Kale. Kulikuwa na habari nyingi ambazo sikuwa nimewahi kujifunza hapo awali; ama kwa kweli, sikuwa nimewahi kujifunza juu ya nyingi yao kabla ya wakati huo. Kwa sababu kwa kawaida sikupenda kusoma na pia sikuwa nimemaliza shule ya upili, nilikuwa chini ya shinikizo kubwa la kujaribu kuelewa kila kitu, haswa wiki ya mwisho kabla ya mtihani. Katika darasa hili moja, nilipaswa kuandika kirasmi juu ya mada fulani ya Agano la Kale, ambayo sikumbuki sasa. Hilo liliniogopesha sana. Mwaka wangu wa kwanza katika chuo kikuu, nilipaswa kuandika mada yangu ya kwanza, na iliporudishwa, kulikuwa na “F” kubwa juu yake katika wino mwekundu, na maneno yafuatayo yalikuwa yameandikwa mwishoni mwa taarifa yangu, “Je! Kuna uwezekano kwamba ulienda sekondari?” Kiingereza changu na sarufi vilikuwa vya kutisha sana kiasi kwamba mwalimu alishangaa jinsi nilivyoweza kuingia katika chuo hicho kikuu. Ilibidi nisaidiwe kujifunza lugha ya Kiingereza ili niweze kumaliza mwaka huo wa kwanza.

Sasa, katika shinikizo hilo la wiki ya mwisho, nilikuwa na mada nyingine ya kuandika. Jamani, niliogopa mradi huo sana. Nilikuwa nikiketi kuandika lakini sikuwa nimewahi kufundishwa chochote kuhusu jinsi ya kufanya hivyo; kwa hiyo nilikuwa nikifanya utafiti na kunakili maneno moja kwa moja huku nikirekebisha kidogo tu ili mtu asije akasema kwamba nilikuwa nimenakili maandishi yangu mengi kutoka kwa vyanzo anuwai. Moyo wangu ulikuwa wazi maana sikufikiri haikuwa sawa kufanya hivyo, na niliandika tena kile nilichokuwa nikisoma kwa maneno yangu mwenyewe; lakini ukweli ni kwamba sikujua kuandika.

Naam, wakati huu sikuwa na muda. Rafiki yangu mmoja ambaye tulikuwa darasa moja lakini wakati tofauti wa siku hakuwa mbali nami ukumbini. Kila mtu darasani alitakiwa kuandika juu ya mada moja, kwa hiyo nilimuuliza rafiki yangu kama ningeweza kuona jinsi alivyopanga maandishi yake. Sasa, kwa sababu moja au nyingine, mara aliponipa karatasi yake, nilikuwa na ufahamu kwamba singeweza kuandika vyema kama yeye kwa hivyo nikaamua kuinakili. Najua, najua, umeshtuka. Kumbuka, nilikuwa Mkristo mchanga wakati huo. Kweli, sikunakili kila kitu, lakini nilinakili karibu nusu moja kwa moja kwenye karatasi yangu. Mwishoni mwa wiki hiyo ya fainali, nilimpa profesa wangu karatasi yangu, huku nikihisi nafuu kwamba tulikuwa tumemaliza mtihani huo. Lakini jambo fulani lilitokea baadaye ambalo lilinifundisha somo muhimu katika kusikia sauti ya Mungu.

Usiku huo sikuweza kulala. Dhamiri yangu ilikuwa ikinena kwa nguvu

sana kiasi cha kunikosesha usingizi. Nilitambua kwamba nilichofanya hakikuwa sahihi na niliiba na kusema uwongo. Pia sikuwa nimemheshimu rafiki yangu na nilikuwa nimemvunjia heshima. Nilihuzunika sana! Saa 3:00 asubuhi, nilienda kwa chumba cha rafiki yangu na kumwamsha, na kumwambia nilichokuwa nimefanya kilikuwa makosa, kisha nikamwomba msamaha. Alinitazama kwa macho yenye usingizi na kusema, “Rudi kitandani, Gary.” Kisha akajipindua tu na kurudi kulala.

Siku iliyofuata, nilienda kwa profesa wangu na kukiri nilichokuwa nimefanya. Bila shaka, ilimbidi anipe “F” kwa mtihani huo, lakini alitabasamu na kusema alithamini kwamba nilimwendea kuhusu hilo. Kisha akasema kwa kuwa nilikuwa nimemwendea, bado angenipa “B” katika masomo ya mwaka huo. Ni kitulizo kilichoje, na nilihisi bora zaidi kunyamazisha sauti ya hukumu na kupata uhuru na amani.

Kwa hiyo acha nikuulize swali, “Kwa nini rafiki yangu angeweza kujipindua na kulala tena nilipokuwa katika maumivu makali ya kihisia moyoni? Kwa nini yeye pia hakuhisi uchungu? Kwa nini sikuweza kulala, na kwa nini nilikuwa na huzuni nyingi?” Sauti ilikuwa ikinisemesha kila nilipojaribu kulala. Dhamiri yangu ilikuwa inahisi kutiwa hatiani! Ufafanuzi wa neno dhamiri ni: ujuzi wa kiasili wa mema na mabaya. Linamaanisha “kujua pamoja na” au “kuwa na ujuzi wa.”

Kama mshumaa, nuru yake huangaza ili kufichua giza. Dhamiri hurekodi kikamilifu kila mawazo na matendo ambayo umewahi kufanya. Kama shahidi katika chumba cha mahakama, dhamiri hushuhudia yale yaliyofichwa kabisa. Inanena na kukukumbusha kufanya yaliyo mema na kuepuka mabaya. Dhamiri ni sauti ya ndani ya Mungu ndani ya kila mtu. Dhamiri inamtaka kila mtu atoe hesabu kwa ajili matendo yake. Dhamiri humwita kila mtu, kama katika chumba cha mahakama, kutoa hesabu mbele ya Mungu. Kama vile shahidi anavyoitwa kutoa ushahidi, ndivyo dhamiri yetu inavyozungumza kwa niaba yetu (kututetea) au kutuhukumu (kutushtaki).

Utafiti uliochapishwa na Medical Xpress ulithibitisha ukweli huu:

“Nadharia iliyopo sasa juu ya maendeleo ya binadamu ni kwamba wanadamu huanza maisha yao na ‘hali tupu kimaadili,’ lakini utafiti mpya unapingana na maoni haya. Watafiti wamegundua watoto wachanga wenye umri wa miezi sita tayari wanafanya maamuzi ya kimaadili, na wanafikiri tunaweza kuzaliwa tukiwa na kanuni za maadili zilizounganishwa katika akili zetu.”

## **DHAMIRI NI SAUTI YA MUNGU KATIKA KILA MWANADAMU, CHAPA YA MUUMBA NA MATAKWA YAKE ILI KUISHI MAISHA TULIYOUMBWA KUISHI.**

*Katika hili tutafahamu ya kwamba tu wa kweli, nasi tutaituliza mioyo yetu mbele Zake, ikiwa mioyo yetu inatuhukumu; kwa maana Mungu ni Mkuu kuliko mioyo yetu naye anajua yote. Wapenzi, mioyo yetu isipotuhukumu, tuna ujasiri kwa Mungu; na lolote tuombalo, twalipokea Kwake, kwa kuwa twazishika amri Zake, na kuyatenda yapendezayo machoni Pake.*

—1 Yohana 3:19-22

Dhamiri ni sauti ya Mungu katika kila mwanadamu, chapa ya Muumba na matakwa Yake ili kuishi maisha tuliyoumbwa kuishi. Hakuna mtu anayeweza kuepuka dhamiri yake. Mara nyingi nilikuwa nikistaajabu kwamba mtu aliyeya au kuiba benki na kutoweka angejisalimisha ghafla. Lakini sasa najua hakuna mateso makubwa kuliko dhamiri inayomhukumu mtu kuwa na hatia! Paulo anasema katika 2 Wakorintho 1:12 kwamba dhamiri hushuhudia na kunena.

*Kwa maana kujisifu kwetu ni huku, ushuhuda wa dhamiri yetu, ya kwamba kwa utakatifu na weupe wa moyo utokao kwa Mungu; si kwa hekima ya mwili, bali kwa neema ya Mungu; tulienenda katika dunia, na hasa kwenu ninyi.*

—2 Wakorintho 1:12

Labda unaweza kusema, “Dhamiri hunena kwa mamlaka gani? Kwa nini ushuhuda wake unaweza kusimama katika mahakama ya sheria ya kiroho?” Kwa sababu ni sauti ya Mungu. Paulo, tena, katika Warumi 2:14-15, anatuambia dhamiri hunena nasi mara nyingi.

*Kwa maana watu wa Mataifa wasio na sheria wafanyapo kwa tabia zao yaliyo ndani ya torati, hao wasio na sheria wamekuwa sheria kwa nafsi zao wenyewe. Hao waionyesha kazi ya torati iliyoandikwa mioyoni mwao, dhamiri yao ikiwashuhudia, na mawazo yao, yenyewe kwa yenyewe, yakiwashitaki au kuwatetea;*

—Warumi 2:14-15

Kila mtu ana dhamiri. Unaweza kutokubaliana. Unaweza kujua

watu ambao huonekana kwamba hawana hisia. Lakini ninakuhakikishia hawakuanzia hapo. Mtu anapoendelea kupinga sauti ya dhamiri yake, sauti hiyo huanza kupunguka na kupunguka.

*Kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe.* (1 Timotheo 4:2)

Paulo anasema watu hawa wamechoma dhamiri zao, au wamejifanya wasiweze kuhisi au kusikia dhamiri zao kwa kuifanya mioyo yao kuwa migumu dhidi yake. Fikiria ngozi yako. Ukiichoma, haiwezi kuwa na hisia mpaka ngozi mpya itakapokua na ngozi ngumu ya zamani kuanguka. Ndivyo ilivyo kuhusu dhamiri yetu. Dhamiri haiwezi kukulazimu ufanye chochote—inanena tu. Unaweza kuipuuza au kwenda kinyume nayo. Lakini Paulo anaonya kwamba ukipuuzwa dhamiri yako, hilo linaweza kukuletea matatizo makubwa; au, kama Paulo alivyosema, maisha yako yataangamia.

*Mwanangu Timotheo, nakukabidhi agizo hilo liwe akiba, kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako, ili katika hayo uwipige vile vita vizuri; uwe mwenye imani na dhamiri njema, ambayo wengine wameisukumia mbali, **wakaangamia** kwa habari ya imani.*

—1 Timotheo 1:18-19

Kimsingi, watu wanaojifanya wagumu dhidi ya sauti ya dhamiri zao wamepoteza uwezo wao wa kuelekeza maisha yao. Dira yao imeharibika na haifanyi kazi tena. Hawajui wanaelekea upande gani tena. Paulo anasema tunahitaji kudumisha dhamiri njema, iliyo safi, ili kuhakikisha kwamba tunaelekea njia sahihi. Kwa sababu tunaweza kuifanya mioyo yetu kuwa migumu na kupoteza uwezo wetu wa kubaini kati ya mema na mabaya, Paulo anasema ni muhimu kufuata sheria na kufanya yaliyo sahihi.

*Kwa hiyo ni lazima kutii, si kwa sababu ya ile ghadhabu tu, ila na kwa sababu ya dhamiri.* (Warumi 13:5)

Ukiasi sheria, dhamiri yako itakuhukumu. Kwa hiyo Paulo anasema tutii sheria, na kufanya yaliyo sahihi ili dhamiri zetu zibaki laini na nyororo na ziweze kufanya kazi jinsi Mungu alivyopanga, ili kutulinda kutokana na hatari.

Kuhusu dhamiri, ninakumbuka jambo lingine la kipumbavu nililofanya linalodhihirisha kanuni hii. Tukio hili lilitokea kabla ya kuanza kazi ya uchungaji. Mara tu utakaposikia hadithi hii utagundua kwa nini Mungu bado hakuwa ameniachilia niwe mchungaji. Hadithi hii inahusu gari ambalo nilimiliki. Lilikuwa gari aina ya Peugeot coupe 505 ambalo nililipenda sana. Basi siku moja mtu alinigonga kutoka nyuma nilipokuwa kwa mataa ya trafiki. Sehemu ya nyuma ilibondeka, na fremu ikapinda, na kulikuwa na uharibifu mwingine kwa mwili wa gari kutokana na ajali hiyo. Wakala wa bima wa yule mtu aliyenigonga alikuja nyumbani kwetu mashambani ili kukagua gari na kunipa makadirio ya ukarabati.

Kabla sijakuambia kilichotokea mara tu alipofika, ninahitaji kukuambia kuwa wiki chache kabla ya ajali hii kutokea, kifaa cha kupunguza sauti ya gari kilikuwa kimeanguka. Kifaa cha kuendesha paa la juu la kuingiza jua kwa gari, ambacho kilikuwa kwenye shina, pia kilikuwa kimeacha kufanya kazi wiki chache kabla ya wakala kuja kushughulikia madai hayo. Wakala wa bima alipokuja aliniuliza kama kifaa hicho cha kupunguza sauti ya gari alichokiona hapo chini kando ya gari (nilikiweka pale ili akione) kilikuwa sehemu ya ajali hiyo. Nilihisi hatia niliposema, “Ndio, Bwana.” Kisha akaniuliza ikiwa kifaa cha kuendesha paa, ambacho nilimwambia hakifanyi kazi pia, kiliathiriwa na ajali. Tena, nikasema, “Ndio.”

Katika roho yangu, nilisikia dhamiri yangu ikipiga kelele, “Gary, unafanya nini? Unasema uwongo!” Sasa, sikiliza jinsi nilivyojidanganya. Kwa kweli nakumbuka nikiwaza niipuuze sauti hiyo, huku nikijiambia kwamba itaondoka. Leo, siwezi kuamini nilifikiri hivyo wakati huo. Doh, si unafurahi kwamba bado sikuwa mchungaji? Nina hakika Mungu alifurahi!

Hata hivyo, gari lilipeleka kufanyiwa ukarabati, na baada ya karibu wiki moja waliniita niende kuchukua gari. Nilipoona gari langu nilifurahi sana. Lilipendeza kwelikweli! Nililipeleka nyumbani nikiwa na furaha sana kwamba kila kitu kilikuwa kimerekebishwa. Baada ya wiki moja au zaidi, niliamua kwenda nyumbani haraka kula chakula cha mchana pamoja na Drenda na watoto. Nyumba yetu ilikuwa kama maili mbili tu kutoka kwa ofisi yangu ambayo nilikuwa nimekodisha kwa ajili ya kampuni yangu ya fedha. Niliingia katika kijibarabara chetu na kuegesha gari nyumbani karibu na mlango wa mbele, kisha nikaingia ndani ya nyumba na kula chakula kizuri cha mchana.

Nilipokuwa nikitoka nyumbani ili kwenda nje kupitia mlango wa mbele, niliona kwamba gari langu halikuwepo. Nilichanganyikiwa. Gari langu limeenda wapi? Nilitazama pande zote kisha nikalionga. Nyumba

yetu ilikuwa juu ya kilima na, inaonekana, nilikuwa nimesahau kuweka breki. Ingawa sikuwa nimewahi kufanya hivyo hapo awali, lazima iwe nilifanya hivyo wakati huu maana lilikuwa limeviringishwa nyuma kwenye kijibarabara chetu kirefu na kugonga mti. Nilipoteremka kuelekea kwenye gari, nilipigwa na mshtuko. Sehemu ya nyuma ilikuwa imegongwa, na uharibifu ulilingana na ule wa ile ajali kabla ya kufanyiwa ukarabati. Fremu ilikuwa imepinda kama ilivyokuwa hapo awali, kifaa cha kupunguza sauti ya gari kilikuwa kimeanguka chini, na kifaa cha kuendesha paa la gari kilikuwa kimeharibika pia. Kila kitu kilikuwa kama kilivyokuwa kabla ya gari kwenda kufanyiwa ukarabati kutokana na ile ajali.

Nikiwa nimesimama pale, ghafla nilipata ufahamu kisha nikaanza kucheka. Mungu alikuwa ananifundisha somo ambalo kijana huyu mhubiri alihitaji kujifunza kabla ya kuongoza watu. Sikulikarabati gari hilo tena. Badala yake, nililiuza tu kama lilivyokuwa kwa ajili ya sehemu zingine ambazo zilikuwa sawa. Ninakumbuka wakati mwingine maishani mwangu ambapo dhamiri yangu ilinipigia kelele kingi nikome. Ninaiita hadithi ya baiskeli.

Natumai hadithi hizi zinakusaidia. Najua, hungelikiria ningeweza kwenda chini hivyo kufanya mambo kama haya, lakini utakuwa umekosea. Nina furaha kwamba nimeokoka kwa sababu ninahisi maisha yangu yangukuwa tofauti kabisa kama singeokoka.

Hadithi ya baiskeli ilitokea miaka kadhaa baada ya hadithi hiyo nyingine niliyokuambia hivi punde, na ndio, nilikuwa nimeanza kuchunga kanisa letu jipya. Nilikuwa nimeenda nyumbani kwa babangu Jumamosi alasiri na sasa nilikuwa nikiondoka, huku nikirudi nyuma na gari letu aina ya Dodge Caravan, yenye rangi ya fedha ili kuingia kwenye barabara kuu yenye njia mbili ambapo babangu alikuwa akiishi. Nyumba ya babangu ilikuwa chini ya kilima kidogo kilichokuwa pande zote za barabara. Kwa sababu moja au nyingine, sikumwona mwendesha baiskeli ambaye alikuwa akiteremka kilima hicho. Nilikuwa nimeteremka polepole, wala hakuwa nyuma yangu, lakini kwa sababu alikuwa akiteremka kwa kasi, alinifikia nilipokuwa nimeanza kuendesha gari kwenda mbele ili kuondoka.

Wakati huu wote sikuwa nimemuona, lakini, ghafla, nilisikia sauti kubwa BAM, BAM, BAM katika upande mmoja wa gari. Nilitazama kwenye kioo cha nyuma, na hapo nikamwona mwendesha baiskeli nyuma ya gari akiwa ameinua mikono yake miwili na kunitukana akitumia vidole vyake vya kati vya mikono yake miwili, kisha kunipa laana kwa sauti kubwa. Nilishangazwa sana na kuhisi kutukanwa kabisa kwamba mtu huyu angeweza kufanya hivyo. Nilijua kwamba angeweza kupunguza mwendo

virahisi alipokuwa akiteremka na kuniona nikirudi nyuma. Pia nilijua kwamba kama angetaka, angeweza kunizunguka kwa mwendo huo wake wa kasi aliokuwa nao. Lakini badala yake, aliamua kutoa hoja.

Nilishtuka sana kwamba alidhani angeweza kushindana na gari. Basi nilihisi kwamba mtu alihitaji kumfundisha somo mtu huyu mwenye kiburi, kwa hivyo nilipunguza mwendo na kungoja afike karibu na gari, kisha nikakanyaga breki. Nilihisi kuridhika nilipomtazama akinyakua ghafla nguzo ya breki ya baiskeli yake, huku akijaribu kuepuka kugonga nyuma ya gari langu. Naam, hilo lilimfanya aanze kutukana na kulaani jinsi sikuwa nimewahi kuona au kusikia hapo awali. Aliendelea na kuendelea, na kuendelea.

Niliendesha gari langu taratibu kwa barabara hiyo kisha nikaingia kwenye kijibarabara kingine na upande wa nyuma ili gari langu litazame barabara. Lilikaa pembeni, likimlenga yule mwendesha baiskeli ambaye alikuwa akielekea upande wangu. Aliponiona nikimsubiri, huku nikimlenga na gari langu, ghafla alinyamaza. Nafikiri hatimaye alipata ufahamu kwamba alikuwa juu ya baiskeli na magari ni makubwa zaidi kuliko baiskeli. Niliteremsha dirisha kisha nikamngoja asogee karibu na gari langu. Aliponikaribia nilimpigia kelele kwamba ikiwa ningemwona tena kwenye barabara hiyo, ningemkanyaga. Kwa hayo, nilikanyaga mafuta ya gari, ambayo wakati huo nilikuwa nimeilekeza kwake kwa umbali wa futi 15. Nilihisi gari likigwaruza baiskeli yake huku nikikosa kidogo tu kumgonga. Nilihisi kutolewa lawama kwa kiasi fulani. *Hakika nilimuonyesha*, niliwaza, lakini si kwa muda mrefu.

Kutoka rohoni mwangu, nilimsikia Roho Mtakatifu akisema kwa sauti yenye nguvu na yenye mamlaka, “Gary, unafanya nini?” Kuona maneno haya yakiwa yamechapishwa hapa hakuna nguvu kama yalivyosikika kwangu wakati huo. Ghafla, niliingiwa na ufahamu kwamba ningeweza kumuua mtu huyo. Nilitazama nyuma kwenye kioo changu cha kutazama nyuma na alikuwa pale, akijikokota polepole sana, kichwa chini, na akionekana kuwa amejeruhiwa au kushangaa tu kwamba bado alikuwa hai. Sina uhakika. Niliendelea na safari yangu, lakini dhamiri yangu haikuniachilia. Kama mchungaji mpya, nilitambua kile ambacho kingeweza kutokea. Niliwaza kuona magazeti yakisema, “Mchungaji wa Kanisa la Faith Life amkanyaga mwendesha baiskeli katika tukio la ghadhabu ya barabarani.” Roho Mtakatifu alinikumbusha kwamba ilikuwa kwa ajili ya watu kama yeye kwamba Mungu alikuwa ameniita nianzishe kanisa huko. Kwa kweli nilishtushwa na matendo yangu mwenyewe, na nilitubu mbele za Bwana



kwa machozi.

Kwa hivyo, hebu tukubaliane kwamba, kweli umesikia sauti ya Mungu hapo awali. Lakini unahitaji kudumisha wororo katika dhamiri hiyo na usiiruhusu iwe ngumu ili uweze kumsikia Mungu kila wakati. Biblia inasema kwamba watu wa Israeli walifanya mioyo yao kuwa migumu dhidi ya Mungu na hawakuweza kamwe kuingia katika Nchi ya Ahadi. Mwandishi wa Waebrania anatuonya sisi waumini wa Agano Jipya tusifuatue mfano wao.

*Kwa hivyo, kama anenavyo Roho Mtakatifu, “Leo, kama mtaisikia sauti Yake, msifanye migumu mioyo yenu, kama wakati wa kukasirisha, siku ya kujaribiwa katika jangwa.”*

—Waebrania 3:7-8

Onyo hili limerudiwa angalau mara tatu katika sura ya tatu na ya nne. Mbona onyo? Kwa sababu Mungu anataka kukubariki na anataka uwe na yote ambayo Yesu alilipia.

**KWA HIYO, KAMA ANENAVYO ROHO MTAKATIFU, “LEO, KAMA MTAISIKIA SAUTI YAKE, MSIFANYE MIGUMU MIOYO YENU, KAMA WAKATI WA KUKASIRISHA, SIKU YA KUJARIBIWA KATIKA JANGWA.”**

Kuwa na moyo mgumu hunikumbusha mtoto wa farasi niliyekuwa naye nilipokuwa mvulana. Alikuwa mnyama mbaya sana kuliko yeyote nimewahi kuona, na mwerevu pia. Mimi tu ndiye niliyeweza kumpanda, au niseme kuthubutu kumpanda. Nakumbuka siku moja nilikuwa na rafiki ambaye alidai kupenda farasi na angeweza

kudhibiti farasi yeyote. Alisisitiza kwamba alitaka kumpanda Tony, (hilo ndilo lililokuwa jina lake). Baada ya muda, aliweza kunishawishi nimruhusu ajaribu, kwa hiyo nikamtayarisha Tony. Jina la kijana huyo lilikuwa Jackie, na sitasahau kamwe kilichotokea alipoketi kwenye tandiko la kukalia Tony. Alipoketi juu ya Tony, waliondoka. Tony alitoka mbio moja kwa moja hadi kwenye bwawa lililokuwa karibu yadi 50 kutoka nyumbani kwetu. Jackie alikuwa akihema kwa nguvu kadiri awezavyo huku akiwa ameshikilia kamba za kumwelekeza farasi na kupiga kelele kwamba Tony asimame, lakini Tony hakumjali. Badala yake, Tony alikimbia kwa mwendo wa kasi moja kwa moja hadi kwenye kidimbwi hicho kisha ghafla akasimama huku kichwa chake kikiwa kimeinamishwa chini kwenye ukingo wa maji. Kweli, bila

shaka Jackie alirushwa moja kwa moja juu ya farasi hadi ndani ya bwawa. Kisha Tony akageuka na kuanza kutafuna nyasi kana kwamba hakuna kilichotokea.

Wajua, kamba za kuelekeza Tony zilikuwa zimevutwa mara nyingi sana kiasi kwamba hakuhihi maumivu mdomoni tena. Alikuwa amezoea hilo na hivyo hakujali. Kama mtoto wa farasi, Tony hakuwa na thamani kwa mtu yeyote ila mimi. Kwa nini? Kwa sababu, kama nilivyosema awali, alikuwa mwerevu. Mimi ndiye niliyekuwa nikimpa chakula. Na alijifunza njia pekee ya kutoka kwenye kibanda chake kwenda kwenye hewa safi na nyasi za kijani ambazo alipenda kuzitafuna ni kuniruhusu nimpande. Ingawa bado ilibidi nichunge sana. Alikuwa akitembea huku kichwa chake kikiwa amekiegemeza upande mmoja ili aweze kunitazama ninapomkalia. Alikuwa anangoja nigeuze kichwa changu upande mwingine. Hapo ndipo angegeuza kichwa nyuma haraka na kuniuma mguu. Na hebu nikuambie kwamba hilo liliumiza, kwa hivyo ilibidi nikimtaazame wakati wote. Lakini kuhusu kuwa na manufaa, hakuwa na yoyote.

Tukiruhusu mioyo yetu iwe migumu, tutakuwa watu wasioweza kutumiwa na Mungu, kama vile Tony alivyokuwa. Wakati mmoja, tulikuwa tumemfunga Tony na mnyororo. Baba yangu alikuwa akimmiminia Tony maji kwenye ndoo. Baba yangu alipogeuka ili aondoke, Tony alivuta kichwa mbele na kumng'ata upande wa nyuma. Babangu hakuwa mwongofu na alikuwa mwenye hasira. Kulikuwa na jiwe la chumvi lililokuwa karibu na ndoo ya maji. Babangu alichukua jiwe hilo na kumrushia Tony kwa nguvu zote. Lakini Tony alinusurika. Nilimwamini Tony? La hashu!

Na ndivyo ilivyo katika maisha ya watu. Wao hufikiri kwamba wanaasi au kuwa kinyume na dhamiri zao mara moja tu, lakini wasichotambua ni kwamba wanasababisha kovu kila mara wanapofanya hivyo. Siku moja, watakuwa kama Tony na hawatasikia maumivu yoyote au majuto ikiwa watachagua kutomtii Mungu au kufanya kile asemacho. Suluhu ni kuwa mwepesi wa kutubu unapogundua kuwa uko kinyume na dhamiri yako.

Zaburi ya 51 iliandikwa na Mfalme Daudi baada ya kufanya dhambi na Bathsheba. Ni zaburi ya toba.

*Ee Mungu, unirehemu, sawasawa na fadhili Zako. Kiasi cha wingi wa rehema Zako, yafute makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, unitakase dhambi zangu. Maana nimejua mimi makosa yangu na dhambi yangu i mbele yangu daima. Nimekutenda dhambi Wewe peke Yako, na kufanya maovu mbele za macho Yako.*

*Wewe ujulikane kuwa una haki unenapo, na kuwa safi utoapo hukumu. Tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu; mama yangu alinichukua mimba hatiani. Tazama, wapendezwa na kweli iliyo moyoni; nawe utanijulisha hekima kwa siri, unisafishe kwa hisopo nami nitakuwa safi, unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe, mifupa uliyoiponda ifurahi. Usitiri uso Wako usitazame dhambi zangu; uzifute hatia zangu zote. Ee Mungu, **uniumbie moyo safi**, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala Roho Yako mtakatifu usiniondolee. Unirudishie furaha ya wokovu Wako; unitegemeze kwa roho ya wepesi.*

—Zaburi 51:1-12

Daudi alimlilia Mungu aumbe ndani yake moyo safi, roho iliyovunjika, moyo wa toba. Kimsingi, Daudi alisema kwamba alitaka moyo unaoweza kuhisi tena. Lakini Daudi hangejiingiza kamwe katika matatizo aliyoyapata ikiwa angesikiliza dhamiri yake. Kwa hivyo kumbuka, ukiiipuuza dhamiri yako, utaufanya moyo wako kuwa mgumu, na itakuwa rahisi kufanya hivyo wakati ujao, na wakati ujao, na wakati unaofuata hadi huwezi kumsikia Mungu hata kidogo.

Dhamiri ni njia mojawapo tu ya kumsikia Mungu. Bila shaka, Roho Mtakatifu hunena nasi moja kwa moja kwa mafundisho na maelekezo. Na kama nilivyosema tayari, nimemsikia Roho Mtakatifu akinirekebisha kwa sauti kuu, yenye mamlaka na pia sauti ndogo tulivu. Nimemsikia akisema kwa njia ya ndoto na maono pia, ambayo nitazungumzia katika sura inayofuata. Lakini katika sura hii, tumejifunza ikiwa tunataka kumsikia Mungu, tunahitaji dhamiri zetu ziwe bila lawama, kwa kutubu haraka ili ziendelee kuwa laini na nyororo!



## SURA YA 10

# MAONO NA NDOTO

Niliamka ghafula na kuketi kitandani kisha nikamwambia Drenda, “Una mimba ya mtoto wa kike!”

Kati ya watoto wote watano tuliowazaa, ni mara moja tu ambapo Mungu ametuambia jinsia ya mtoto—Polly, mtoto wetu wa nne. Naamini ilikuwa hivyo ili tuweze kumtunza vyema maana familia yetu ilihusika katika ajali ya barabara wakati Drenda alikuwa na ujauzito wa Polly wa takriban miezi sita. Tukiendesha gari kwa mwendo wa kilomita 55 kwa saa kwenye njia iliyokuwa na barabara mbili, kijana mmoja alijitokeza na gari lake mbele yetu. Hakukuwa na wakati wa kusimama, tuligonga gari lake kwa nguvu. Hakuna aliyeumia sana, lakini sote tulienda hospitalini. Drenda, ambaye alikuwa mjamzito, alipigwa na mkanda wa kiti na ukaathiri tumbo lake. Alikuwa na wasiwasi kuhusu Polly. Kwa sababu Mungu alikuwa amenena nasi kumhusu Polly, tulihisi amani na tukajua kwamba Polly alikuwa sawa, na ndivyo alivyokuwa.

Ninapozungumza juu ya Polly, nakumbuka wakati yeye, kama mke, alikuwa na ujauzito wa mtoto wake wa kwanza. Ilikuwa imetubidi mimi na Drenda tusafiri nje ya nchi kikazi. Kwa bahati mbaya, tarehe ya kuzaliwa kwa Polly ilikuwa katikati ya safari hiyo ya biashara. Sasa, ikiwa unamjua mke wangu, Drenda, hatakosa kuwepo wakati mmoja wa binti zake anapojifungua. Kwa hiyo tulifikiri kughairi safari lakini baada ya kufanya maombi, Roho Mtakatifu alinena nami kwamba tarehe hiyo haikuwa sahihi, na kwamba mtoto angezaliwa siku moja baada ya kurudi kwetu. Nilimwambia Drenda kile ambacho Bwana alikuwa amesema kuhusu tarehe hiyo, kisha tukaendelea na safari. Tuliporudi nyumbani, Polly alipata uchungu wa kujifungua katika tarehe hususa ambayo Bwana alikuwa

amesema. Ivory, mjukuu wetu mpya, alizaliwa kwa wakati ufaao.

Hii ni mifano ya wakati maneno ya Roho Mtakatifu kuhusu masuala ya maisha yanapotoka katika roho zetu binafsi. Lakini kuna njia zingine Roho Mtakatifu anazungumza nasi ambazo tunapaswa kufahamu.

*Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono; tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile, nitamimina Roho Yangu.*

—Yoeli 2:28–29

Nabii Yoeli alisema kwamba siku inakuja ambapo Mungu atamimina Roho Yake juu ya wanadamu wote. Tunaishi katika siku hiyo sasa. Katika Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu alikuja juu ya wale waliokuwa wakingoja katika chumba cha juu. Umati wa watu ulipowaona wote waliokuwa katika chumba cha juu wakinena kwa lugha na kumsifu Mungu, walifikiri kwamba wamelewa, kisha wakauliza, “Ni nini hiki?” Petro alisimama na kuhutubia umati.

*Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake, akawaambia, “Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu. Sivyoy mnavyodhani; watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana; lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli, ‘Itakuwa siku za mwisho,’ asema Mungu, ‘nitawamwagia watu wote Roho Yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto. Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi Wangu wanaume na wanawake Roho Yangu, nao watatabiri.*

—Matendo 2:14–18

Ndoto na maono ni sehemu kubwa sana ya jinsi Roho Mtakatifu anavyonena nasi. Sina hakika kwa nini wakati mwingine Roho Mtakatifu hunena kwa sauti ndogo, na tulivu na wakati mwingine hunena katika ndoto. Nafikiri labda ni kwa sababu sote tuna shughuli nyingi sana. Wakati tuko kimya, Yeye huwa na uwezo wa kupata usikivu wetu. Au huenda ikawa ni kwa sababu tuko katika hali ya kuchanganyikiwa au hali zinatufanya

kuwa na ugumu wa kusikia sauti hiyo ndogo na tulivu. Roho Mtakatifu hutaka kuhakikisha kwamba tumepokea ujumbe. Picha ina thamani ya maneno elfu. Kwa sababu yoyote ile, namshukuru Mungu kwa ndoto na maono. Ndoto na maono ni kitu kimoja. Zote mbili ni picha tunazoziona, tofauti ikiwa tunaona maono tukiwa macho, na ndoto ni picha tunazoziona tukiwa tumelala.

Kuhusu maono, nimekuwa na machache tu ambayo ningeyaita maono wazi, ambayo mtu huona akiwa macho kana kwamba ni halisi. Maono ya maana zaidi ambayo nimepata ni wakati nilipoitwa kuhubiri nikiwa na umri wa miaka 19. Nilikuwa nimebatizwa katika Roho Mtakatifu mwezi mmoja au zaidi kabla ya haya kutokea. Bila shaka, haya yote yalikuwa mapya kwangu maana kanisa la kimadhehebu nililohudhuria halikufundisha sana juu ya Roho Mtakatifu.

Lakini ilikuwa siku yangu ya kuzaliwa, na nilikuwa nimealikwa kula chakula kizuri cha jioni pamoja na marafiki fulani. Tulipoketi kula, tulishukuru kwa chakula, na ghafla, nilihisi Roho Mtakatifu akinijia kwa nguvu sana. Tena, nilikuwa mgeni kwa mambo kama haya, lakini nilifahamu kutokana na kubatizwa katika Roho Mtakatifu jinsi Roho Mtakatifu alivyokuja juu ya mtu. Sikujua la kufanya wakati huo, kwa hiyo niliomba radhi niondoke mezani na nikatoka nje maana kulikuwa na mlango ulioelekea nje nyuma yangu.

Nilipotoka nje, uwepo wa Mungu ulizidi kuwa na nguvu zaidi, kisha nikaona maono wazi, ambayo inamaanisha niliona mambo kana kwamba nilikuwa nikitazama kitu katika hali ya asili. Niliona kwamba nilikuwa nimesimama nyuma ya jukwaa dogo, na nilikuwa nikihutubia watu chumbani. Chumba hicho kilikuwa na watu wapatao 35 hadi 40, na wote walikuwa wameketi kwa viti vya kukunja. Niliweza kutambua kwamba ilikuwa usiku kwa sababu nilipotazama madirisha kulikuwa na giza tupu nje. Kisha sauti ikanena na kusema, "Ninakuita ulihubiri Neno Langu." Tukio hili lilirudiwa mara tatu kisha picha ikatoweka na upako ukainuliwa. Niliporudi chumbani, marafiki zangu waliniuliza ikiwa kulikuwa na shida yoyote, nami nikasema, "Nafikiri nimeitwa kuhubiri!"

Nakumbuka nilienda nyumbani usiku huo na kumwambia babangu kilichotokea. Alisema kwamba wahubiri hawana pesa nyingi. Hicho ndicho tu alichosema. Hakuwa Mkristo wakati huo, lakini, Mungu asifiwe, alitoa moyo wake kwa Yesu alipokuwa na umri wa miaka 80 na sasa yuko mbinguni.

Katika hali hii, naamini Roho Mtakatifu alinena nami katika maono

wazi kwa sababu, kwanza kabisa, nilikuwa kijana. Alifahamu ningekumbana na mateso mengi katika familia yangu kwa ajili ya kumtumikia Yeye na kwamba nilihitaji nanga hiyo kwa ajili ya safari iliyokuwa mbele yangu. Na hakika maono hayo yameendelea kunena nami miaka hii yote.

Ono lingine la wazi nililokuwa nalo lilitokea katika nyumba ile yetu kuukuu ya mashambani tulimoishi. Tulikuwa tumeishi katika nyumba hiyo kuukuu na mbovu kwa karibu miaka tisa, na mwingi wa wakati huo tulikaa katika umaskini mbaya. Lakini tulipoanza kujifunza jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi, tulianza kufanikiwa na tukatoka kwa madeni kabisa.

Ulikuwa wakati huu ambapo Mungu alitimiza maono yale niliyokuwa nayo nilipokuwa na umri wa miaka 19 aliponiita kuhubiri. Ulikuwa ni wakati huu, miaka 21 baada ya kuitwa kuhubiri ambapo Mungu aliniambia nianzishe kanisa. Hadi wakati huu, nilikuwa nimeenda chuo kikuu na kufanya kazi katika sekta ya kifedha kwa miaka hiyo 21. Lakini sasa nikiwa na umri wa miaka 40, Mungu alinena nami nianzishe kanisa langu.

Tulizindua kanisa letu katika chumba cha chini katika kituo cha redio cha Kikristo, na usiku wa kwanza tulipokutana huko, ulifanana na maono Mungu aliyokuwa amenipa miaka 21 awali. Katika ibada hiyo ya kwanza, niliona watu walewale niliowaona katika maono wakiwa wameketi kwenye viti vya kukunja na madirisha yaleyale ambayo yalikuwa na giza kwa sababu tulikutana usiku. Pia niliona jukwaa lilelile dogo.

Mimi na Drenda tulizindua kanisa letu na tulifurahia sana Ufalme kiasi kwamba hatukujali sana mahali tulipoishi. Tulijua kwamba hatimaye tungeondoka kwenye shamba hilo maana familia yetu ilikuwa imeongezeka na kufikia watoto watano, na hatukuwa na nafasi. Hata hivyo, tulikuwa na shughuli nyingi za kuendeleza biashara na kanisa letu, kiasi cha kutufanya tuwe na furaha.

Lakini siku moja niliporudi kutoka kanisani, niliingia sebuleni na kuketi kwenye kochi. Nikiwa nimeketi, ghafla chumba kilichokuwa pembeni kilitoweka, niliona chumba kilekile nilichokuwemo lakini sasa hakikuwa na samani hata moja ndani yake. Mlango niliokuwa nimeingilia ulifunguka kuelekea upande wa chumba cha kula chakula, na kochi nililokuwa nimekalia lilitazama mlango huo. Niliweza kuona ndani ya chumba cha kula kutoka pale nilipokuwa sebuleni. Sebule ilikuwa tupu kabisa na pia chumba cha kula kilikuwa tupu. Ono hilo lilidumu kwa takriban sekunde tano tu, na nilipotafakari hilo, nilijua kwamba wakati wa kuondoka mashambani ulikuwa umefika. Maono yalipoisha, mara moja



nilimwambia Drenda kilichotokea na kumwambia kwamba ulikuwa wakati wa kuondoka.

Tena, ninaamini kwamba katika tukio hili ono lilitumiwa kuwasilisha mpango wa Mungu na kuufanya kuwa wazi. Tulikuwa na shughuli nyingi, na ingekuwa rahisi kuahirisha mambo. Lakini ono lilikuwa na uharaka, “Ni wakati wa kwenda!!!” Baadaye ndipo tulipoelewa uharaka huo. Tulikuwa tumekodisha nyumba hiyo kwa miaka tisa, na tulifahamu tulipaswa kuondoka wakati uboreshaji wa nyumba uliokuwa umepangwa ulipoanza, lakini hakuna aliyejua hilo lingefanyika lini hasa.

Kwa hiyo, ili kufupisha hadithi ndefu, Mungu alituelekeza kwenye ardhi maridadi ambako tulikuwa tukijenga makao yetu mapya. Mipango yetu ilikuwa kujenga nyumba polepole kwa sababu tulikuwa na wakati wa kuitengeneza vyema, kwa labda mwaka mmoja au miwili. Hata hivyo, baada ya kuanza kutengeneza nyumba yetu kwa muda wa karibu miezi sita, tulipokea simu kutoka kwa mwenye nyumba, ambaye alitupatia mwezi mmoja tuhame kutoka kwa nyumba hiyo. Tulimwambia tunajenga nyumba mpya na tukauliza ikiwa angeweza kutuongeza muda wa miezi miwili au mitatu, jambo ambalo alikubali lakini bila neema baada ya hapo.

Basi tulifanya kila kitu haraka na tukahamia nyumba yetu mpya mwishoni mwa muda wao wa ziada. Ikiwa Mungu hangetuambia tuhame wakati ule, tungelazimika kuhama mara kadhaa katika kipindi hicho; na maana tulikuwa na shughuli nyingi, hilo lingekuwa tatizo.

Bila shaka, hadithi ya ukungu wa rangi ya samawati niliyoizungumzia mwanzoni mwa kitabu hiki, (tukio lililobadili maisha yangu) ilikuwa ono wazi pia. Ilikuwa tofauti kidogo maana sikuona picha ya maisha yangu ya baadaye, lakini nilikuwa nimeketi ndani ya ukungu huo na kusikia kwa uwazi maneno ya Roho Mtakatifu akiniita kwa mataifa.

Nina hakika kuna maono mengine machache ambayo nimekuwa nayo, lakini ndoto ndizo zimekuwa nyingi zaidi kwangu. Nilipokuwa nikienda Albania, karibu juma moja kabla ya kusafiri, nilikuwa na ndoto kuhusu safari hiyo. Wakati huo katika maisha yangu, sikuwa nimesafiri sana kama nifanyavyo sasa; na kabla ya Mungu kunena nami siku hiyo, sikuwa nimewahi kutamani kusafiri.

Lakini wiki moja kabla ya kuondoka, niliota hivi. Katika ndoto, nilikuwa katika ofisi ya daktari na nilikuwa nimelala kwenye meza ya kufanyiwa uchunguzi, kisha muuguzi akaja na kuniambia kwamba alihitaji kuchukua damu kutoka kwa mkono wangu. Kwa hivyo akaushika mkono wangu, akachukua kidole changu cha kati ili kukibandika ili aweze kutoa

damu, jambo ambalo nilifikiri lilikuwa geni. Lakini unajua jinsi ndoto zilivyo; kuna mambo ambayo unayajua kwenye ndoto.

Katika ndoto hii, nilifahamu kabla ya kuondoka ulimwenguni kwamba kila kidole changu kingetolewa damu. Hili lilinea nami kwa sababu katika shule ya Biblia, nilifundishwa kwamba mkono unaweza kutumika kukukumbusha juu ya ofisi tano za kanisa: kidole gumba kikiwa utume, kidole cha pili huonyesha kazi ya unabii, kidole cha kati ni uinjilisti, kidole cha pete ni uchungaji, na kidole cha mwisho kinahusu mwalimu ambaye anafanya kazi pamoja na mchungaji.

Kwa hiyo nilielewa kile muuguzi alichokuwa akiniambia. Nilifahamu kwamba katika maisha yangu, angalau wakati fulani maishani mwangu, ningefanya kazi katika kila ofisi ya kanisa. Mimi ni mchungaji na mwalimu, bila shaka, lakini pia najua kwamba nina neno la kinabii kwa kanisa kuhusu Ufalme na fedha. Hivi ndivyo Yesu alivyoniitia nilipokuwa Albania. Ndoto hiyo ilionyesha muuguzi akinidunga kidole cha kati, kwa hivyo nilipata ufahamu kwamba nilikuwa nikitumwa na Habari Njema ya Injili kama mwinjilisti katika taifa la Albania. Sasa hivi naanza kufanya kazi katika eneo la utume maishani mwangu.

Katika ndoto hiyo baada ya kunidunga kidole cha kati, muuguzi alichukua mikono yake na kuiweka pamoja kama vile mtoto anavyofanya wakati anapoomba, na kunitazama na kusema neno *omba* kwa midomo yake bila kulitamka kwa sauti. Alifanya kama mtu unavyofanya ukiwa mahali ambapo huwezi kuzungumza. Kutokana na ndoto hiyo, nilielewa kwamba nilikuwa nikitumwa kama mwinjilisti katika taifa la Albania, na nilipaswa kuomba kuhusu safari hiyo.

Nimeota ndoto nyingi sana siwezi kuzitaja zote hapa, lakini ndoto ni sauti ya Roho Mtakatifu. Sasa, nimekutana na watu ambao huota kila siku na hufanya kila kitu kuonekana kuwa cha “kiroho” sana. Ninaamini bila shaka kwamba unapaswa kupambanua ndoto, na baadhi ya watu wanaotamani kuonekana kuwa wa kiroho huwa na kiburi cha kiroho na hivyo huota ndoto zisizotoka kwa Mungu. Mimi huwa sioti mara nyingi. Kwa mwaka mzima, mimi huwa na ndoto nne hadi kumi na mbili ambazo ninajua zinaniambia jambo muhimu kutoka kwa Mungu. Bila shaka nambari hiyo inaweza kubadilika kuwa ndoto zaidi au chache kwa mwaka. Sifikiri kuna umuhimu wowote kuhusu idadi ya ndoto, lakini kile unachojifunza ndicho kilicho muhimu.

Ndoto iliyobadili maisha yangu kabisa ilikuwa wakati Mungu aliponiambia niache kufanya kazi katika kampuni ya kifedha ambapo

nilikuwa nimefanya kazi kwa miaka minane. Aliniambia nizindue kampuni yangu binafsi ya kusaidia watu kutoka kwa madeni. Hiyo hakika ilikuwa muhimu.

Kisha kumekuwa na ndoto zenye onyo. Nakumbuka moja ya ajabu sana ambayo ilikuwa onyo. Ilitokea wakati fedha za huduma zilikuwa kidogo na kulikuwa na shinikizo la kifedha. Nilikuwa nimelala kitandani karibu kushika usingizi. Mlango wa chumba cha kulala ulikuwa wazi, kisha nikasikia kelele kidogo ukumbini (katika ndoto yangu) na nilipotazama mlango niliona pepo mdogo, mwenye urefu wa futi tatu na nusu, akivuta begi la kitambaa lililojaa pesa nyuma yake. Mfuko ulifanana ule ambao Santa Claus wa Krismasi hutumia. Mfuko ulikuwa ukiburutwa chini nyuma ya pepo huyo, na ulikuwa umejaa. Hakuwa akielekea nje ya nyumba, lakini nilimsikia akipiga kona na kwenda kwenye ghorofa yetu ya tatu. Nilipoamka na kutafakari ndoto hiyo, nilitambua kwamba Bwana alikuwa akinionyesha kwamba fedha zilikuwa zikiibiwa au kupotea.

Inashangaza kwamba katika ndoto nilikuwa na wazo la kiasi cha fedha kilichokuwa kwenye mfuko. Nakumbuka kwamba nilijua kulikuwa na takriban \$25,000 humo. Pia nilihisi kwa sababu yule pepo hakutoka nje ya nyumba bali alichukua pesa hizo ghorofani kwamba mtu au watu waliokuwa wakiiba au kuruhusu pesa zitumiwe vibaya walikuwa sehemu ya nyumba, yaani sehemu ya huduma yetu. Basi kitu cha kwanza nilichofanya siku iliyofuata ni kumpigia simu mzee wetu mkuu wa kanisa na kumwomba achunguze hesabu zetu katika idara ya fedha. Kwa kufanya hivyo, tulipata gharama nyingi zisizohitajika kila mwezi ambazo zilikuwa zimepuuzwa. Tulipojumlisha gharama hizo, tulipata takriban \$25,000 kwa mwezi. Tuliitambua kwamba hakuna mtu aliyekuwa akiiba, bali kwa kupuuzwa, pesa hizo zilikuwa zikipotea au kulikuwa na hitaji la kupunguza matumizi ili kuokoa pesa. Tulihitaji pesa hizo katika kipindi hicho maana mambo yalikuwa magumu sana.

## **NDOTO ZINAWEZA PIA KUTUMIWA NA MUNGU KUKUPA MKAKATI.**

Ndoto zinaweza pia kutumiwa na Mungu kukupa mkakati. Mwaka uliopita, 2018, nilikuwa na ndoto rahisi sana ambapo kile nilichosikia ni maneno, “Ita merikebu.” Niliandika hilo lakini sikuwa na uwezo wa kupambanua maana yake. Niliendelea kumuuliza Bwana kuhusu jambo hilo, wala sikumwambia yeyote isipokuwa Drenda. Katika mkutano wetu wa wanaume wa Januari, nilikuwa nikiorodhesha majukumu yangu ya mwaka mzima kukiwemo mpango wa kitaifa wa kuwa na kikundi kidogo

ambacho nilikuwa nimekiwazia kwa miaka kadhaa lakini nilihisi huo ndio uliokuwa mwaka wa kutekeleza hilo. Baada ya mkutano, mmoja wa wanaume alinjia na kusema alihisi kuwa mpumbavu kwa kutaka kuniambia alichotaka kuniambia, lakini alisema, “Bwana alisema wewe ni kama Helen wa Troy.” Sikujua alikuwa akizungumzia nini, kwa hivyo alianza kunieleza alichomaanisha. Nilimwomba anitumie barua pepe na kurudia yale aliyoniambia ana kwa ana. Hii hapana ndiyo barua yake pepe aliyonitumia.

*Mfalme wa Sparta, jina lake Menelaus aliamuru meli 1,000 zizinduke ili kumwoko mke wake, Helen, kutokana na Watroja wa nchi ya Troy. “Uso uliozindua meli elfu” ni msemo unaojulikana sana na unamrejelea Helen wa Troy.*

*Siku ya Jumatano, Januari 30, 2019, Mchungaji alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa wanaume wa Apex, Bwana alinena nami kwamba hii ni kama hadithi ya Helen wa Troy, kwamba mfalme anazindua meli 1,000 kuokoa waliopotea, waliopotea katika imani, waliopotea kifamilia, na waliopotea kifedha.*

*Katika huduma Yake,*

*Aaron*

Alinitumia barua nyingine pepe baada ya siku moja.

*Mchungaji,*

*Nataka kutoa mtazamo wa kijeshi kuhusu hadithi ya Helen wa Troy. Kwa watu wengi, ni hadithi ya mfalme ambaye alizindua meli 1000 ili kuokoa mke wake aliyepotea kutoka kwa Watroja. Lakini kwa mtu mwenye mawazo ya kijeshi, hii ilikuwa kazi ya kijeshi iliyoitwa Operesheni Helen wa Troy. Kila kikosi cha kijeshi hupewa jina lake. Kwa mfano, Timu ya Sita ya wanajeshi wenye ujuzi baharini, angani na ardhini, iliyotumwa kuvamia nyumba ya Osama Bin Laden iliitwa Operesheni Neptune Spear. Nimehusika katika misheni zenye majina ya kupendeza kama vile Operesheni Enda Mbele Mike, Elvis Marshall, na Santa Claus.*

*Vikosi hivi hupewa majina ya operesheni ya kijeshi ili kuwifanya viweze kutambulika rahisi, au kuweka wazi aina ya operesheni vinavyohusika nayo, na ni nani anayeendesha au kutekeleza operesheni hiyo. Wakati Bwana aliposema ulikuwa kama Helen wa Troy, akili yangu ya kijeshi ilitafsiri kwamba unatumia Operesheni Helen wa Troy, ambayo ni misheni ya kuzindua meli 1,000 kuokoa waliopotea, waliopotea katika imani, kifamilia, na kifedha.*

*Zaidi ya hayo, ninaposikia kwamba meli 1,000 zinatumwa, ninawaza pia kuhusu idadi ya wapiganaji, wafanyakazi wasaidizi, mafunzo, vifaa, na michakato ya kusimamia kazi hiyo inayohitajika ili kuzindua kila meli. Hakuna mtu mwingine mwenye uwezo wa kuamuru kikosi hiki na kupeleka jeshi hili kwa Ufalme wa Mungu kuliko wewe. Umetumia miaka mingi kutufunza kwa ajili ya wakati huu. Nina hakika familia yangu na mimi pamoja na Mwili wote wa Kristo una shauku ya kutekeleza hili.*

*Katika huduma YAKE,*

*Aaron*

Aaron alikuwa mwanajeshi mwenye ujuzi wa bahari, anga, na ardhi na alitumwa kwa operesheni 9 huku akihudumu kwa miaka 21 jeshini. Ana hadithi kuu ya jinsi nguvu ya msalaba ilivyoleta mabadiliko makubwa maishani mwake. Hakujua chochote kuhusu yale ambayo Bwana alikuwa ameniambia katika ndoto, yaani “kuita merikebu.” Lakini “neni lake la ujuzi” lilinithibitishia kwamba nilikuwa nimesikia kwa usahihi kutoka kwa Bwana na hilo lilisaidia kuniweka kwenye njia ambayo Mungu alikuwa ameniandalia. Kusudi letu ni kukuza vikundi 1,000 vidogo katika nchi nzima ambavyo vitahubiri habari njema ya Ufalme. Ikiwa ungependa kuhusika na jeshi hili, wasiliana nami kupitia kwa tovuti yangu, Garykeese.com.

Nafikiri umelewa. Ndoto ni njia yenye nguvu ambayo Mungu hunena na watu Wake, ili kuwasaidia kupata mwelekeo, mkakati, onyo, na faraja.

Kabla ya sura hii kuisha, ningependa kuongeza njia moja nyingine ambayo Mungu hutumia kusaidia kuelekeza mkakati, na hiyo ni karama ya unabii. Aaron alipokea neno la maarifa kuhusu mipango yangu ya kuzindua mradi mpya. Neno la maarifa ni kile linachoitwa tu, neno la maarifa.

Haya ni maarifa unayopewa kutoka kwa Roho wa Mungu, yaani mambo usiyoweza kujua wewe mwenyewe. Neno la maarifa limeorodheshwa katika 1 Wakorintho 12 kama moja ya karama tisa za Roho Mtakatifu. Sasa, nia yangu si kufundisha kuhusu karama hizo za kiroho katika kitabu hiki, lakini nataka kutaja mojawapo, ambayo ni neno la unabii.

Watu wengi huchanganyikiwa maishani kwa kutolewa karama hii na ndio maana nazungumza kuihusu. Watu wanapofikiria kuhusu unabii, huwa wanafikiri kwamba nabii atawaita na kuwanyooshea kidole usoni huku wakisema kitu kama, “Unapaswa kwenda Afrika” au “Umeitwa kuwa mchungaji.” Taarifa hizi zote mbili zinaweza kuwa kiwakilishi sahihi cha unabii wa kweli, lakini zote mbili zinaweza kuwa na makosa pia. Inategemea jinsi unavyozielewa. Ikiwa kauli hizi ni za kutoa mwelekeo, basi zote ni makosa, lakini ikiwa zinathibitisha jambo, basi zinaweza kuwa sahihi. Paulo anaeleza kusudi la unabii.

**“BALI YEYE  
AHUTUBUYE, ASEMA  
NA WATU MANENO  
YA KUWAJENGA,  
NA KUWAFARIJI, NA  
KUWATIA MOYO.”**

**–1 WAKORINTHO 14:3**

*“Bali yeye ahutubuye, asema na watu maneno ya kuwajenga, na kuwafariji, na kuwatia moyo.” (1 Wakorintho 14:3)*

Ndiyo hayo. Hakuna neno humo linaloonyesha kwamba unapaswa kupata mwelekeo kupitia kwa unabii, lakini hivyo ndivyo watu wengi wanavyouona unabii, kwamba unatoa mwelekeo. Lakini kulingana na Paulo, unabii unapaswa kuthibitisha mwelekeo, wala si kutoa mwelekeo. Wajua, mara tu unapozaliwa mara ya pili, Roho Mtakatifu aliye ndani yako ndiye atakayekuambia cha kufanya. Huhitaji mtu akwambie kile ulichoitiwa kumfanyia Yesu. Neno la unabii linaweza kuthibitisha jambo unalofahamu tayari.

Kwa hivyo kwa mfano, katika mfano nilioutoa, “Unapaswa kwenda Afrika,” nilisema huo unaweza kuwa mfano halisi wa neno la unabii, ikiwa Roho Mtakatifu tayari alikuwa amekwambia hilo na alikuwa akithibitisha kupitia neno hilo. Lakini kama kwenda Afrika hakukuwa akilini mwako na hiyo ndiyo mara yako ya kwanza kusikia hivyo, basi huo si mfano halisi wa neno la unabii katika kanisa la Agano Jipya.

Ni jambo la kichaa sana unaposikia watu wakizungumza. Nimekuwa na Wakristo ambao wamenijia na kusema, “Mungu aliniambia kwenye

mkutano kwamba ninapaswa kufanikiwa.” Naam, ndio, lakini huhitaji mtu akupe neno la kukuambia kwamba utafanikiwa; Biblia inatuambia hivyo tayari. Mimi huona Wakristo wakizunguka hapa na pale kuuliza watu ikiwa wana neno kuwahusu. Huhitaji mtu akupe neno! Roho Mtakatifu ndani yako atanena nawe na, ndio, Mungu anaweza kutuma neno la unabii la uthibitisho ili kukutia moyo, lakini sio kukuongoza.

Mfano wa kushangaza zaidi kuhusu hilo kutokea maishani mwangu mwenyewe ni wakati nilikuwa nikichumbiana na Drenda. Nilikuwa nikielekea Georgia ili kukutana na familia yake huko kwa ajili ya kumwomba tufunge ndoa. Nilipokuwa huko, nilitaka kutembelea kanisa lake la mtaani pamoja naye. Wakati huo, nilikuwa nimepata kazi katika sekta ya huduma za kifedha ambayo nilikuwa nikipambana nayo. Nilikuwa nimeitwa kuhubiri nikiwa na umri wa miaka 19 na nilikuwa nimemaliza chuo kikuu na digrii katika masomo ya Agano la Kale, lakini nilihisi ilinipasa kuchukua kazi hiyo ya kifedha. Sikujua cha kufanya, nilichanganyikiwa.

Baada ya ibada ya Jumapili asubuhi katika kanisa la mtaani la Drenda, mwanamke ambaye sikumfahamu, lakini Drenda hakika alimjua, alinikaribia na kusema alikuwa na neno langu. Alisema, “Una ofa ya kazi. Kazi hii ina vipengele 10 vifuatavyo, na akataja kikamilifu kila kitu ambacho ningefanya katika kazi hiyo mpya.” Alisema, “Unapaswa kuchukua kazi hiyo, maana Bwana yu ndani yake.” Katika tukio hilo, tayari nilihisi kuichukua kazi hiyo lakini sijui kwa nini nilihisi kuchanganyikiwa. Neno lake la unabii lilinifariji na kunitia moyo, na lilithibitisha mwelekeo niliipaswa kufuata. Tena, Roho Mtakatifu aliye ndani yako atakuongoza na kuwa Mshauri wako.





## SURA YA 11

# ROHO MTAKATIFU HUSIKIKA KAMA BOSI WANGU

Kanisa langu lilipokuwa dogo, nilikuwa na familia fulani lililohitaji kazi. Lilikuwa familia jema na kila mara walitaka kusaidia katika kazi zilizohitaji kufanywa kanisani. Lakini walionekana kuwa na masuala ya kifedha kila wakati. Baba hakuwa na kazi tena, kwa hivyo nikaamua kuwasaidia. Nilikuwa katika harakati za kujenga nyumba yangu wakati huo na nilifanya kazi zote za kuunganisha waya za umeme mwenyewe. Niligundua kwamba baba huyo alijua mambo machache kuhusu kazi ya umeme, na nilijitolea kumlipa ikiwa angefanya kazi kwa masaa fulani kwa sababu familia yake haikuwa na chakula. Kwa hivyo alikuja na alifanya kazi nzuri ya kuunganisha waya za umeme za nyumba yangu.

Sikufikiria sana kuhusu hilo, lakini baada ya karibu mwezi mmoja, nilipokea simu kutoka kwake. Alisema kwamba watu wachache walikuwa wakikusanyika kufanya maombi kwa ajili yangu. Nikasema, “Vipi?” Alisema kulikuwa na baadhi ya mambo yaliyohitaji kubadilishwa kanisani mwetu, kisha akasema kulikuwa ana orodha ya mambo 10 waliyokuwa wakijadiliana. Ya kwanza kwenye orodha ilikuwa kwamba nyumba yangu ilikuwa kubwa sana. Aliniuliza kwa uwazi kanisa lilikuwa likinilipa pesa ngapi kununua nyumba kama hiyo. Nilimwambia haraka kwamba kanisa halikuwa linanilipa hata senti moja, kwamba sikupokea malipo kutoka

kanisani. Baada ya kusema hivyo, kukawa ukimya kwa muda. Kisha akasema, “Kanisa halikulipi hundi ya malipo?” “Hiyo ni kweli,” nilijibu. Tena kukawa kimya hadi mwishowe akasema. “Naam, labda wanapaswa kufanya hivyo.” Na huo ukawa mwisho wa mazungumzo yetu.

Basi, ilikuwa baada ya karibu juma moja hivi niliposikia kuhusu kazi katika kampuni ambayo nilifikiri huenda ingekuwa katika eneo lake alilopenda, kwa hivyo nilimwambia jambo hilo. Alienda huko na kuomba kazi na akaipata. Sasa kumbuka, familia yake ilikuwa karibu kufukuzwa kutoka nyumbani kwao. Kwa hiyo jumapili ya wiki aliyoajiriwa kazi alipokuja kanisani na kuniambia kwamba aliacha kazi, nilipigwa na mshtuko. “Uliacha; kwa nini?” Aliniambia kuwa siku ya Ijumaa alasiri wakati alikuwa amemaliza kazi yake walimtaka afaagie sakafu. Aliniambia kwamba papo hapo aliamua kuacha kazi, huku akiwaambia kwamba hakujitandikisha kufagia sakafu. Sikuamini nilichokuwa nikisikia. Nilifahamu kijana huyu angepitia magumu maishani ikiwa alitaka kufanikiwa. Kila wakati nilimuonea huruma mke wak. Baada ya muda mfupi waliondoka kanisani, na sijui ni nini kilichowapata. Walakini, labda naweza kukisia vyema. Kulingana na mtazamo wake wa kiburi na kutotaka kufanya kazi, naweza kukisia kwamba wasifu wake ulikuwa na maingizo machache ya kazi, mengi yao yakiwa ya muda mfupi. Kiwango chake cha utajiri hakikuwa zaidi ya kuishi maisha ya kunusurika. Sasa, usikose kunielewa vyema. Watu hubadilika, na ninatumaini kwamba alibadilika. Lakini hili ndilo nijualo kwamba nilipomjua, alikuwa akielekea kwenye njia potovu. Wajua, alikuwa akipuuza sauti ya Mungu.

Unaweza kuuliza, “Ni sauti gani ya Mungu unayoizungumzia?” Nina hakika angeuliza hivyo ikiwa ungemwambia kuhusu hilo, kwa sababu wakati huo, hakujua chochote. Lakini alikuwa akipuuza mojawapo ya mbinu kuu za Mungu za kuwafunza na kuwatayarisha watu kwa ajili ya hatima zao: kujifunza kujitiisha. Najua kichwa cha sura hii kinaweza kuwa kimekuchanganya. Bosi wangu ana uhusiano gani na Roho Mtakatifu? Katika sura hii utagundua kwamba bosu wako anahusika sana na uwezo wako wa kumsikia Roho Mtakatifu!

Ninataka kuanza somo letu la mada hii muhimu katika Mathayo 8:5-10.

*Hata alipoingia Kapernaumu akida mmoja alimjia, akamsihi, akisema, “Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani, mgonjwa wa kupooza, anaumwa sana.”*

*Yesu akamwambia, “Nitakuja, nimponye.”*

*Yule akida akamjibu, akasema, “Bwana, mimi sistabili wewe uingie chini ya dari yangu; lakini sema neno tu, na mtumishi wangu atapona. Kwa maana mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia huyu, ‘Nenda,’ huenda; na huyu, ‘Njoo,’ huja; na mtumwa wangu, ‘Fanya hivi,’ hufanya.”*

*Yesu aliposikia hayo, alistaajabu, akawaambia wale waliomfuata, “Amin, nawaambieni, sijaona imani kubwa namna hii, kwa yeyote katika Israeli.”*

—Mathayo 8:5-10

Kwa nini mtu huyu aliamini virahisi kwamba Yesu angeweza kumponya mtumishi wake? Alijibu swali hilo mwenyewe. “*Kwa maana mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia huyu, ‘Nenda,’ huenda; na huyu, ‘Njoo,’ huja; na mtumwa wangu, ‘Fanya hivi,’ hufanya.*” Ni kwa sababu alijua jinsi mamlaka yanavyofanya kazi. Jinsi alivyokuwa chini ya mamlaka, ndivyo watumishi wake walivyokuwa chini ya mamlaka yake. Alielewa kwamba maneno ya bosi wake yalikuwa na sauti ya Kaisari. Hakika, ukweli ni kwamba sauti ya bosi wake ilikuwa sauti ya Kaisari. Pia alielewa kwamba sauti yake kwa watumishi wake ilisikika kama sauti ya Kaisari kwao. Hivyo ndivyo mamlaka yanavyofanya kazi. Kwa hiyo, kwa sababu alielewa maana ya kujitiisha kwa mamlaka, alielewa kwa urahisi jinsi Yesu angeweza kuchukua mamlaka dhidi ya hali hiyo kwa kuinenea. Hilo tu ndilo alilopaswa kufanya pia. Ikiwa angemwambia mtumishi afanye jambo fulani, angelifanya. Ilikuwa rahisi hivyo. Hapa kuna ukweli unaopaswa kujifunza:

### **UNAWENZA KUWA NA MAMLAKA UNAPOJITIISHA CHINI YA MAMLAKA!**

Ikiwa Shetani angeweza kuondoa heshima yote kwa mamlaka na kumshawishi kila mtu kufanya chochote apendacho wakati apendapo, basi ulimwengu ungeanguka na kuwa machafuko na uharibifu. Hiki ndicho alichokuwa akimpa Hawa changamoto nacho kwenye bustani, “Je, kweli Mungu alisema...?” Sikiliza, kila mtu katika sayari hii yuko chini ya mamlaka au chini ya mamlaka mbalimbali. Kutambua upo chini ya mamlaka ya nani kutakusaidia kujua ni nani unatakiwa kumsikiliza na ni nani usiyepaswa

kumsikiliza. Lakini leo, kila mtu anataka kuwa na mamlaka bila kuwa chini ya mamlaka, na hilo haliwezekani.

Hivi majuzi, nilizungumza na mwanakandarasi ambaye aliniambia jinsi anavyolipa watu pesa taslimu ili kuepuka kulipa kodi na ada ya fidia ya wafanyakazi. Lakini tayari najua jinsi matokeo yatakavyokuwa. Siku moja, mfanyikazi mmoja ataumia kisha ataomba kulipwa fidia ya wafanyikazi lakini atagundua kwamba bosi wake hakuwa amewahi kulipa pesa yoyote kwa ajili ya mpango wa Fidia unaohitajika kwa ajili ya Wafanyakazi, na atamshtaki mkandarasi huyo kwa sababu sheria inataka Fidia ya Wafanyakazi ilipwe. Wanakandarasi kadhaa katika kanisa langu wamepitia jambo hilo.

Wiki iliyopita, nilizungumza na mwanamke ambaye alikuwa akisema habitaji mchungaji; kwamba uhusiano ulikuwa kati yake tu na Roho Mtakatifu. Kweli? Vema, afadhali amwulize Yesu kuhusu hilo kwa sababu Yeye ndiye aliyeweka wachungaji na kuanzisha kanisa la mtaani katika Waefeso sura ya 4. Ikiwa anajitiisha kwa Yesu, basi anapaswa kufuata mamlaka ambayo Yesu alianzisha. Ukweli ni kwamba hajajitiisha kwa Yesu na anataka kufanya mambo yake mwenyewe. Kuna uwezekano mkubwa wa kuingia katika udanganyifu na nyakati ngumu kwa sababu ya jambo hilo.

Sio muda mrefu sana uliopita, nilizungumza na muuzaji ambaye alikuwa akianzisha kampuni yake mwenyewe na alikuwa akichukua wateja wote kutoka kwa kampuni alipokuwa, ingawa walikuwa wametia saini bila pingamizi wakisema kwamba hawatafanya hivyo. Je, watafanikiwa katika kufanya hivyo? Huo ni wizi tu!

Najua unaweza kukosa kupenda sura hii kama zile zingine nilipoeleza mambo ya ajabu, mazuri ambayo Roho Mtakatifu anafanya, lakini usipoelewa sura hii sawasawa, sahau mengine yote kwa sababu ni Mungu anayeinua watu.

Nakumbuka mwanamke mmoja alipokuja kwangu katika mkutano wa maombi akiwa anatokwa machozi, na kuniuliza kwa nini sikumwita afanye maombi. Nilishtuka! Kwa nini lilikuwa jambo kubwa sana kuitwa kuomba isipokuwa, bila shaka, utambulisho wake ulitegemea kuonwa na watu?

Na, bila shaka, ningemwambia kwa nini sikumwita baada ya dakika moja kama angekuwa anamsikiliza mtu yeyote. Mwanamke huyu

hakumheshimu mumewe na mara kwa mara alikuwa akiweka upungufu wake wa kiroho chini katika vikao vya uvumi ambavyo alihusika navyo kila wakati. Ndiyo maana sikumwita. Ukweli kwamba alitokwa na machozi kwa sababu hakuonwa kuwa mwanamke wa kiroho kama alivyofikiri mbele ya kundi zima kulifichua kwamba hakuheshimu mamlaka na, hivyo, alikuwa mwanamke hatari.

Basi hebu nikuulize swali. Je, una sifa ya kwenda unakotaka kwenda, mahali ambapo ndoto zako zinataka kwenda? Je, nikimuuliza mchungaji au bosu wako maoni yake kuhusu uaminifu wako, atasema nini? Wajua, huwezi kuwa na mamlaka hadi upite jaribio la utiishaji. Sikusema hili; bali ni Yesu.

*Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia. Basi, kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli? Na kama hamkuwa waaminifu katika mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?*

—Luka 16:10-12

### **Je, unaweza kuaminiwa na mamlaka? Ushahidi uko katika kujitiisha kwako.**

Hebu tuangalie hadithi katika Biblia ambayo inaweza kuwa na athari kubwa juu ya mafanikio yako maishani.

*Nao Wafilisti wakakusanyana ili wapigane na Waisraeli, magari thelathini elfu, na wapanda farasi sita elfu, na watu kama mchanga ulio ufuoni mwa bahari kwa wingi wao; wakapanda juu, wakapiga kambi yao katika Mikmasi, upande wa mashariki wa Beth-aveni. Hata Waisraeli walipoona ya kuwa wako katika dhiki, (maana watu walifadhaishwa), ndipo hao watu wakajificha katika mapango, na katika vichaka, na katika miamba, na katika mashimo, na katika mabirika. Hata baadhi ya Waebrania walivuka Yordani, wakaingia nchi ya Gadi na Gileadi.*

*Lakini Sauli alikuwa angali huko Gilgali, nao watu wote wakamfuata wakitetemeka. Akangoja siku saba, kwa kadiri ya muhula uliowekwa na Samweli lakini Samweli hakuja Gilgali; na*

*hao watu wakatawanyika mbali naye. Sauli akasema, “Nileteeni hapa sadaka ya kuteketezwa na sadaka za amani. Akaitoa sadaka ya kuteketezwa.”*

—1 Samweli 13:5-9

*Naye Samweli akamwambia Sauli, “Umefanya upumbavu; hukuishika amri ya Bwana, Mungu wako, aliyokuamuru; kwa maana Bwana angaliufanya ufalme wako kuwa imara juu ya Israeli milele. Lakini sasa ufalme wako hautadumu; Bwana amejitafutia mtu aupendezaye moyo Wake, naye Bwana amemwamuru yeye kuwa mkuu juu ya watu Wake, kwa sababu wewe hukulishika neno lile Bwana alilokuamuru.*

—1 Samweli 13:13–14

Sauli alikataliwa kwa sababu hakujitiisha chini ya mamlaka. Kwa hiyo tena tunaona ikiwa huwezi kujitiisha kwa mamlaka, huwezi kuwa na mamlaka. Ninataka kutaja jambo muhimu sana hapa. Bwana alitafuta mtu aliyependeza moyo Wake. “Kupendeza moyo Wake” kunamaanisha nini?

*Na alipokwisha kumwondoa huyo, akamwinua Daudi awe mfalme wao ambaye alimshuhudia, akisema, “Nimemwona Daudi, mwana wa Yese, mtu anayeupendeza moyo Wangu, atakayefanya mapenzi Yangu yote.”*

—Matendo 13:22

Je, Mungu anamfafanua je mtu aliye na moyo wake? Kimsingi, ni mtu anayechukia kile ambacho Mungu anachukia na kupenda kile anachokipenda, mtu anayefanya kile ambacho Mungu angefanya kama angekuwepo. Kwa maneno mengine, ikiwa Mungu anachukia dhambi, wanachukia dhambi. Ikiwa Mungu anataka kufanya jambo fulani, wanataka kulifanya. Katika ulimwengu wetu, tunafikiri mtu anayependeza moyo wa Mungu ni mtu mwenye karama nyingi za kiroho. Huwa tunafikiri kuwa mtu wa kiroho ni kusikiliza muziki mwororo wa kuabudu. Lakini Mungu anasema wazi kwamba kutii ni ibada ya kiroho.

*Naye Samweli akasema, “je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu sawasawa na kuitii sauti ya Bwana? Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia kuliko mafuta*

*ya beberu. Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi, na ukaidi ni kama ukafiri na vinyago. Kwa kuwa umelikataa neno la Bwana, Yeye naye amekukataa wewe usiwe mfalme.”*

—1 Samweli 15:22–23

Kwa hiyo tena, acha niseme kwamba sauti ya Mungu husikika kama bosu wako! Mungu huruhusu mwikio wako kwa mamlaka kujaribiwa wakati hakuna anayekujua. Watu wengi hawaelewi jinsi haya yote yanavyofanya kazi. Hawaoni kazi yao ndogo ya muda kuwa muhimu; sio kitu cha thamani. Lakini wasichokijua ni kwamba wanajifunza kuwa na utifu wa kibinafsi, kuhukumu ikiwa kitu kinastahili kutiishwa kulingana na viwango vyao kwa kuzingatia matakwa na malengo yao. Watu hawafundishi kwamba mara tu wanapokubali wanapoaminiwa kufanya kazi hiyo ndogo ya muda, wanakubali kufanya hivyo kana kwamba ni yao wenyewe. Hivyo siyo watu wengi wanavyoona mambo. Wanalenga malengo makubwa zaidi. Hata hivyo, hii ni kazi ya muda tu ya kuwapa pesa za ziada, wala sio mradi mkubwa. Makosa!!!!

Hakuna kazi isiyo na maana. Hakuna kazi ndogo. Daudi alikuwa na kazi ndogo kuchunga kondoo ambayo haikuwa na maana. Lakini haikuwa ndogo kwake; alihatarisha maisha yake angalau mara mbili ili kuwalinda kondoo hao. Kwa maneno mengine, alichukua uaminifu aliopeva kama biashara kubwa sana. Ingawa hakuna mtu aliyejua yeye ni nani, Mungu alimjua! Na Mungu alijua mahali alipokuwa kila wakati.

Mungu anajua mahali ulipo pia, na anajua moyo wako inapohusu mamlaka. Jambo la msingi ni kwamba ikiwa huwezi kujitiisha kwa mtu unayeweza kumuona, hutajitiisha kwa Mungu usiyemuona. Watu wengi sana ninaowaona wana mawazo ya kustahili jambo, wana mawazo ya waathirika; daima kila kitu ni kosa la mtu mwingine. Kila wakati wao husema kwamba makosa yalikuwa ya bosu au serikali, na hufanya kazi wanapolazimishwa tu au kile kinachotosha ili kulipwa mshahara. Kawaida wana mawazo ya usindikaji, ya kuambiwa nini cha kufanya badala ya kufikiria wenyewe. Hivi ndivyo ilivyokuwa kwa wana wa Israeli, ambao, baada ya kutoka katika utumwa wa miaka mingi, waliendelea kufikiri kama watumwa ingawa walikuwa wamewekwa huru. Mawazo yao ya utumwa hayangefanya kazi walipokabili majitu ya Nchi ya Ahadi. Mungu alipaswa kuwafundisha kuhusu jinsi ya kufanikiwa kabla yao kufika kwenye Nchi ya Ahadi. Itambidi akufundishe pia kabla hujafika kwenye nchi yako ya ahadi. Nchi ninayoizungumzia ni hatima yako. Kwa hiyo, je, aliwafunza?

*Akakutweza, akakuacha uone njaa, akakulisha kwa mana, usiyojua wewe wala baba zako hawakuijua; apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana.*

—Kumbukumbu 8:3

*Aliyekulisha jangwani kwa mana, wasiyojua baba zako; apate **kukutweza**, apate **kukujaribu**, ili kukutendea mema mwisho wako.*

—Kumbukumbu 8:16

Mungu aliwanyenyekesha, ambayo inamaanisha aliwafanya wasiwe na ya kutosha, na wahitaji msaada. Ilibidi wajifunze kumtegemea Mungu wala si kujitegemea wenyewe. Mbele yao kulikuwa na vita vikali kuliko kutafuta chakula cha kula tu. Kulikuwa na majitu makubwa na majiji yenye kuta mbele yao ambayo yangewatisha virahisi kama hawangeona kwamba Mungu ni mkuu kuliko shida zao.

Pili, ilibidi wajifunze kufanya maamuzi sahihi peke yao bila kulazimishwa kufanya hivyo. Leo, mimi huona kwamba wazazi wanafanya makosa wanapojaribu kufundisha watoto wao kuhusu utendaji badala ya kufundisha mioyo yao. Mtoto akiambiwa asafishe chumba chake, yeye hufunga mlango kwa nguvu akiwa na mtazamo mbaya, huku akitii lakini kwa moyo wa uasi wala sio moyo wa kujitiisha. Wazazi wanaotaka kuwa marafiki na watoto wao huingia chumbani mwa watoto wao na kuona chumba kisafi kisha wanawaambia watoto kwamba wamefanya kazi nzuri. Makosa!! Mtoto alijifanya kutii, wala sio kutoka kwa moyo wake. Kujitiisha ni kazi ya moyo. Siku moja, mzazi hatakuwepo ili kumlazimu kufanya uamuzi sahihi. Mzazi akiacha kumfunika mtoto, yeye atakuwa huru kufanya apendavyo. Kilicho moyoni sasa kitafichuliwa. Hapa ndipo wazazi wengi hupata mtoto wao katika matatizo na kuchanganyikiwa. Wao husema kwamba siku zote watoto wao wadogo walikuwa watoto wazuri sana, na wanashtushwa na tabia zao wanapoenda katika chuo kikuu au kuondoka kuishi peke yao.

Biblia inasema kwamba Mungu alikuwa akiwajaribu Wasraeli ili mambo yawaendee vyema mwishoni. Hili ndilo hasa tunalolizungumzia. Tofauti na mzazi anayehangaikia zaidi kuhusu kupendwa na mtoto, Mungu anahangaikia hali njema ya muda mrefu ya mtoto. Atarekebisha mitazamo midogo midogo ya moyo kabla haijakuwa tabia ya kudumu. Hili ndilo



lililomaanishwa Maandiko yanaposema kwamba Mungu angewajaribu. Mungu angeweza kuwasahihisha wakati nia za mioyo yao zilipofichuliwa walipoambiwa wajitiishe.

Kila mtu lazima apite jaribio la kujitiisha! Kwa hiyo Mungu hutufunzia wapi leo maana hakuna jangwa la kuvuka? Tunaweza kusikia sauti Yake wapi ili tuweze kujifunza kujitiisha na kustahili kupandishwa cheo? Kumbuka kile alichosema Mungu kuhusu Sauli? Kutii ni bora kuliko sadaka. Matendo yako katika ibada kanisani sio msingi wa kupandishwa cheo kwako. Je, Mungu anaweza kukuamini inapohusu mamlaka? Hilo linaanzia wapi? Nyumbani.

*Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, upate heri, ukae siku nyingi katika dunia.*

—Waefeso 6:1–3

Kwa nini kuwatii wazazi wako kunafanya uwe na maisha marefu na mafanikio maishani? Je, Mungu anakupa pointi unapotii? La, lakini ukijifunza kuheshimu na kuwastahi wazazi wako, ambao wana mamlaka juu ya maisha yako, basi utamheshimu na kumstahi Mungu. Ikiwa unaheshimu mamlaka ya Mungu katika maisha yako, utamtii na mambo yatakuendea vyema kwako. Kwa hiyo ninaweza kusema kwamba Mungu ni kama wazazi wako ulipokuwa mdogo na kuwa chini ya uangalizi wao.

Mahali pa pili ambapo Mungu hutufunza kujitiisha kwa mamlaka ni wakati anapotuweka chini ya mamlaka ya kibinadamu. Bosi wako, mchungaji wako, afisa wa polisi, na serikali, wote ni mifano ya mamlaka ambayo Mungu anatuagiza tujitiishe kwao.

Nakumbuka familia moja katika kanisa letu ambayo kila wakati walilalamika na kuzungumza kuhusu matatizo yao. Walikuwa karibu kupoteza nyumba yao na walihitaji \$10,000 ili kuifanyia ukarabati wa kisasa na kuepuka kunyang'anywa. Walikuwa wamewaambia watu kadhaa kuhusu hadithi yao kanisani. Hatimaye, familia moja iliamua kuwasaidia na kuwapa dola 10,000. Lakini katika muda wa miezi michache, walirudi palepale walipokuwa mwanzoni na wakapoteza nyumba. Nilikuwa nimezungumza na wanandoa hawa, ambao wote hawakuwa na kazi, kuhusu hali hiyo. Nilipendekeza kwamba angalau wafanye kitu wakati wanasubiri kazi zinazofaa. Wangeweza kufanya kazi kwenye mikahawa popote pale

mjini, lakini walisema hawakupenda kazi kama hizo. Nafikiri ni wazi kwamba tatizo lao halikuwa la kifedha bali la kuelewa mamlaka na wajibu. Kwa sababu moja au nyingine, walishindwa kuona kwamba walikuwa na daraka la kibinafsi la kuchukua mamlaka juu ya maisha yao wenyewe na kufanya lolote lifaalo ili kushughulikia tatizo hilo.

Rick Renner, rafiki yangu, anasema kabla ya kumwajiri mtu, huwa anaomba kuona gari lake, au wakati mwingine huenda nyumbani kwao bila kusema. Anaelewa kuwa ikiwa mtu hajukumikii vyema gari lake, hatawahi kujukumikia mambo yake pia. Ni jambo la muda tu kabla ya ofisi yake kufanana gari lake.

Nilipitia wakati wangu wa mafunzo ya jangwani. Na ninafurahi kwamba Mungu hakuniruhusu niendeleo na mtazamo wangu wowote wa kutojali kuhusu mamlaka. Alininyenyekeza na kunijaribu ili aweze kuniandaa kwa ajili ya kazi yangu.

Nakumbuka wakati ambapo tulikuwa na ugumu mwingi kifedha katika nyakati za kuishi kule mashambani. Kwa bahati nzuri, nilikuwa nimefanya mauzo ya uwekezaji ambayo yangenilipia bili zangu, ambazo zilikuwa zikichelewa kila wakati. Lakini hundi ilichelewa kuja, kwa hiyo nilipata wazo zuri. Kufungua akaunti mpya ya hundi katika benki nyingine na kutumia hundi kukopa kutoka kwa akaunti hiyo mpya nikiwa na matarajio kwamba hundi ile nyingine ingekuwa kutoka kwa benki yangu ya kawaida siku iliyofuata, ili kulipia mkopo huo. Lakini hundi haikuja kwa wiki mbili! Niliendelea kufanya hivyo kwa majuma mawili hadi mkopo wote wa hundi ukafika dola 2,000 maana nilipaswa kuwa na chakula nyumbani. Katika kipindi hicho, kiasi cha fedha kiliendelea kuongezeka.

Lakini yote yaliisha wakati meneja wa benki aliponipigia simu asubuhi mapema, na maneno ya kwanza kutoka kinywani mwake yalikuwa, “Bw. Keese, najua unachofanya, na ninafunga akaunti yako. Utaleta pesa za kulipia akaunti hii, na kamwe hutaweza kufungua akaunti katika benki hii tena.” Niliikuwa nimepatikana! Jambo baya sana kuhusu hali hii ni kwamba nilikuwa nikitumia hundi ambazo zilikuwa na Maandiko juu yake, na nilikuwa nikimshuhudia msimamizi wa benki jinsi Mungu alivyokuwa mkuu. Namshukuru Mungu hundi ilikuja siku hiyo, na niliweza kuipeleka hadi kwa benki ili kufidia deni hilo. Lakini ilinibidi niende katika ofisi ya meneja huyo wa benki, nitubu mbele yake, na kumwambia asimlaumu Mungu maana mimi ndiye niliyefanya hayo yote, na ulikuwa upumbavu.

Kisha kulikuwa na wakati katika miaka yangu ya kwanza kwenye biashara ambapo makamu wa mkoa wa kampuni yetu alikuwa akinifunza.

Alipokuwa akichunguza taarifa ya moja ya mauzo yangu, aliona kwamba haikuwa na saini kwa sehemu moja ambapo ilihitajika. Alisema, “Hakuna shida, ishikilie tu kwa mwanga kisha uighushi saini na kuiandika mahali walipokosa kuandika. Hata hivyo, “alisema, “wanataka bima hii na wametia saini kila mahali isipokuwa hapo.” Hivyo ndivyo nilivyofanya. Takriban mwezi mmoja baadaye, nilipokea simu kutoka kwa wakili wa mteja wangu ikisema kwamba mteja wangu alikuwa akinishitaki kwa \$100,000 kwa kughushi jina lake kwenye fomu ya benki ya kutoa pesa. Kiasi hicho kilipunguzwa hadi \$5,000 walipogundua kwamba makamu wa mkoa wa kampuni yetu alihusika, na akafukuzwa kazi.

Lakini ilibidi nijifunze! Mmoja wa wawakilishi wangu wapya alihitaji kufanya mtihani wa bima na hakuwa na pesa za kununua nyenzo za kusoma, kwa hivyo nilimtengenezea nakala ili aweze kutumia. Aliiacha mahali alipokuwa akifanyia mtihani, kisha nikapokea simu nyingine kutoka kwa wakili ambaye alikuwa akifungua shtaka dhidi yangu kwa kukiuka hakimiliki. Katika nyakati hizo, nilijua vyema kabisa njia ya kwenda kwa ofisi za shirika la serikali la kulipa ushuru. Kila mara nilikuwa nikishughulikia bili na ada ya adhabu kwa kuchelewa kufanya malipo. Ninayatazama hayo yote sasa nikiwa na mchanganyiko wa hisia. Mungu alikuwa akiniwajibisha, na kunifundisha. Alijua kwamba siku moja ningekuwa na mamilioni ya dola, na hangeniruhusu niepuke chochote. Asante Mungu kwa hilo!

Ilinibidi nijifunze kwamba Mungu ndiye mwinuaji wangu, na Mungu hatazami utendaji pekee. Ilibidi uadilifu wangu ujaribiwe pia. Ndiyo maana nasema kwamba Mungu husikika kama bosu wako. Bosu wako ni chombo kinachotumiwa na Mungu kukufundisha na kukufanya ujitiishe kwa manufaa ya kazi yako ya siku za usoni. Je, utafaulu katika mtihani?

*Maana sio mashariki wala magharibi, wala nyikani itokako heshima. Bali Mungu ndiye ahukumuye; humdhili huyu na kumwinua huyu.*

—Zaburi 75:6-7

*Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani.*

—Waebrania 12:11

*Enyi watumwa, watiini wao walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Kristo; wala si kwa utumwa wa macho tu kama wajipendekezao kwa wanadamu bali kama watumwa wa Kristo, mkitenda yampendezayo Mungu kwa moyo; kwa nia njema kama kumtumikia Bwana wala si mwanadamu; mkijua ya kuwa kila neno jema alitendalo mtu atapewa lilo hilo na Bwana awe ni mtumwa au awe huru. Nanyi, akina bwana, watendeeni wao jayo hayo, mkiacha kuwaogofya, huku mkijua ya kuwa Yeye aliye Bwana wao na wenu yuko mbinguni, wala Kwake hakuna upendeleo.*

—Waefeso 6:5-9

Utiifu kwa heshima na hofu! Huu ndio mtazamo unaopaswa kuwa nao kwa bosu wako. Kumtii bosu wako kunafafanuliwa na Paulo kama kufanya mapenzi ya Mungu. Umeshangaa? Ndivyo ilivyokuwa kwangu pia!

Kwa hivyo sauti ya Mungu inasikikaje? Kama ya bosu wako!

## **NI JARIBIO!**

Ninapohitimisha somo hili, ninaamini kwamba umechangamshwa na kutiwa moyo. Roho Mtakatifu kweli ni Mshirika wa ajabu maishani, ambaye kwamba kamwe hatakuacha wala kukutupilia mbali. Imekuwa heshima kubwa kushiriki nawe kweli hizi zenye thamani.

—Gary Keese

## SURA YA 12

# JINSI YA KUOMBA KUPOKEA ROHO MTAKATIFU

Kila kitu tunachopokea kutoka kwa Mungu hupokelewa kwa imani katika yale ambayo Mungu amesema, na kupokea karama hii sio jambo tofauti. Kabla ya kuomba ili kupokea, hakikisha kwamba umesoma Maandiko yaliyoorodheshwa katika kitabu hiki hadi uwe na uhakika kwamba haya ndiyo mapenzi ya Mungu juu yako na kwamba maswali yako yamejibiwa. Mara tu utakapopata ujasiri kwamba Ubatizo wa Roho Mtakatifu upo kwa manufaa yako, basi utaomba maombi haya rahisi:

**“Baba, ninaomba Kubatizwa kwa Roho Wako mkuu leo. Ninapokea SASA, kulingana na Neno Lako, kukiwemo uwezo wa kuomba katika Roho. Naomba haya katika jina la Yesu na kwa utukufu Wako! Amina.”**

Usitazame yatakayotokea, au hisia fulani, lakini kuwa thabiti katika Neno la Mungu, ukiamini kwamba umepokea unapoomba. Baada ya kuomba na kupokea, anza kumsifu Mungu na kumshukuru kwa kukupaka mafuta kwa Roho Wake kama alivyoahidi.

Unapoomba, hakikisha unaelewa umepokea unapoomba, sio lazima kuwe na udhahirisho kwamba umepokea. Ushahidi wako ni Neno la Mungu.

*“Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.”* (Marko 11:24b)

Hakikisha kutumia muda kumwabudu Bwana mara utakapoomba kwamba Roho wa Mungu awe uhuru kujidhihirisha katika maombi yako ya ndimi. Mungu hataufanya mdomo wako usonge! Itabidi uwe wazi kuhusu kuomba katika ndimi. Kwa kawaida, watu huhisi kuhuishwa, au kubanwa tumboni wanapoomba au kuhisi Roho wa Mungu.

Unapoendelea kuabudu, jitoe kwa Roho wa Mungu. Utaanza kuhisi sauti tofauti au silabi kutoka rohoni mwako. Itabidi ukubali sauti hizo katika imani. Unapofanya hivyo, utiririko na kumiminwa kwa Roho wa Mungu kutaongezeka.

Ikiwa kwa sababu moja au nyingine hukuomba kwa ndimi mara moja, usijali kuhusu hilo. Umepokea kwa imani, kwa hiyo endelea kumshukuru Mungu kwa upako Wake. Nimeona watu wakienda nyumbani kutoka kwenye mkutano wa kanisa baada ya kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu wakiomba katika Roho njiani, wanapooga mwili asubuhi inayofuata, au wanapokata nyasi baada ya siku chache. Cha muhimu ni kupokea kwa imani na si kupitia kwa hisia.

Fanya kuomba katika Roho sehemu ya kila siku ya maisha yako, na ukuze maisha madhubuti ya maombi. Mungu atanena nawe na kukuelekeza kwa majibu kuhusu mambo yote! Ninatumai kwamba utatenga muda wa kuomba katika Roho na kufurahia manufaa yote ya Ufalme wa Mungu ambao tayari unamiliki!



# MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA

## Nguvu ya Kuwa na Mkakati

Maisha yamejaa maamuzi makubwa.

*Utajuaje ni nyumba gani unapaswa kununua, ni nani unapaswa kuoza au kuolewa naye, au ni kazi gani unayopaswa kufanya?*

**Ikiwa utafanikiwa, unahitaji mkakati. Lakini utakuwaje na mkakati wakati huna majibu yote?**

Siri za Mungu zimefichwa kwa ajili yako, sio *kutoka* kwako.

**Mungu anataka uwe na majibu unayohitaji—ndiyo maana akakupa silaha ya siri!**

Katika awamu ya tatu ya mfululizo wa kitabu *Mapinduzi Yako ya Kifedha*, Gary Keesee anafichua mojawapo ya vipengele muhimu vya mafanikio yake na siri KUU katika Ufalme wa Mungu: *Nguvu ya Kuwa na Mkakati!* Mtu yeyote anaweza kuvua samaki ikiwa anajua mahali pa kushusha nyavu zake. Mungu ana majibu unayohitaji, lakini unapaswa kuelewa jinsi ya kusikia majibu hayo na kuyatumia katika maisha yako—na hayo ndiyo yaliyo katika kitabu hiki.

Jiunge na Gary kwenye safari hii ya kufumbua macho, na ugundue jinsi ya kutumia *Nguvu ya Kuwa na Mkakati* maishani mwako!



Gary Keesee ni mwandishi, mmenenaji, mjasiriamali, mtaalamu wa fedha, na mchungaji ambaye ana shauku ya kusaidia watu kuwa washindi maishani, hasa katika maeneo ya imani, familia, na fedha. Gary na mkewe, Drenda, wameanzisha biashara kadhaa zilizo na fanaka, na ndio waanzilishi wa huduma iitwayo Faith Life Now, ambayo ina vipindi viwili vya televisheni—*Fixing the Money Thing na Drenda*, kongamano kote ulimwenguni, na rasilimali za vitendo. Wao pia ni wachungaji wa Kanisa la Faith Life karibu na Columbus, Ohio.